ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki

11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera

22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa

38. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake

79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa – Tarehe 27 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, napenda kutoa kwenu na kwa wananchi kwa ujumla taarifa kuhusu miswada ya sheria iliyopitishwa katika mkutano uliopita wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 23 Novemba, 2016 mpaka tarehe 2 Disemba, 2016.

Katika Mkutano wa Nne wa Baraza la Tisa la Wawakilishi hili, ilipitishwa Miswada Minne (4) ya sheria ambayo baadhi ilimeshasainiwa na Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria na nishaitolea taarifa mwanzoni mwa Mkutano huu, tarehe 15 Februari, 2017.

Waheshimiwa Wajumbe, Naomba kuwapa taarifa kuwa, kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 91(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016; Mswada ufuatao sasa umekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mswada wenyewe ni; Mswada wa Sheria ya Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kudhibiti na Kusimamia Fedha za Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo na Kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Nam. 12 ya 2005. *(Makofi)*

Waheshimiwa wajumbe nawashukuru sana. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Maryma Thani Juma: (Kny.Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Spika kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2016/2017. Mhe. Spika naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 68

Maslahi ya Walimu wa Tu-Tu

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza:-

Swala la elimu ni muhimu sana katika maisha yetu na M/Mungu amelisisitiza kwa kulifanya kuwa ni wajibu kwetu katika kulitekeleza wajibu huu katika elimu, tumeshuhudia walimu wetu wa TuTu (Tucheze Tujifunze) Chekechea za mitaani wakitoa elimu kwa watoto wetu ili kupata haki zao za msingi.

a) Je, lini walimu hawa watapewa fursa za kujiendeleza kielimu.

b) Na lini walimu hawa wataongezwa maposho yao badala ya Tshs. 30,000/- tu wanazozipata hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe swali lake Nam. 68 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Fursa ya Kujiendeleza kwa Wasaidizi wa Vituo vya TU-TU inatolewa kwa kiasi kikubwa wasaidizi hao wanahamasishwa juu suala la kujiendeleza ili kukuza kiwango chao cha elimu pamoja na kuweza kufanya kazi zao za kufundisha kwa ufanisi. Baadhi ya wasaidizi hao wameshasomea Ualimu ngazi ya cheti katika chuo cha Kiislam, na wengine wamesomea ngazi hiyo ya Cheti kupitia *"Madrasa Early Childhood Programme"*. Aidha, Walimu 557 kupitia *"Early Childhood Certificate Advancement Programme – ECAP"* chini ya Ufadhili wa *GPE* wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya cheti.

b) Siwezi kusema kuwa ni lini wasaidizi hawa wataongezewa posho lao kutoka kiasi cha TZS.30,000/= wanacholipwa sasa, ila napenda

kuwahakikishia kuwa Wizara inafahamu kuwa kiwango cha posho wanacholipwa ni kidogo na kwamba jitihada kubwa zinafanywa na Serikali juu ya nyongeza posho kwa Wasimamizi wa vituo vya TU-TU. Naomba tu, wavute subra kwani suala hili linashughulikiwa. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali jengine la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwanza nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuinyanyua sekta ya elimu hapa Zanzibar. Mhe. Spika, Naibu Waziri amejibu kwamba amekiri posho hili la elfu 30,000/= ambalo sasa hivi ndio wanalipwa walimu wetu wa TU-TU. Mhe. Rais amesema itapofika mwezi wa nne kuna suala la kuongezewa mishahara kwa walimu wetu wa vyeti ambao watapewa kwa kima cha chini laki tatu (300,000). Je, kuhusu posho lao hawa Wizara yake wamewafikiria vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, kama tulivyojibu katika swali la msingi kwamba suala la posho tofauti na suala la mshahara, serikali itaongeza mishahara hawa wako katika suala la posho na kama tulivyosema kwamba suala hili tunalifanyia kazi ili kuona na wao pia wanaongezewa. Lakini kitu cha msingi ni kuvuta subira kama tulivyosema. *(Makofi).*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa na mimi kumuuliza swala moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa walimu hawa wa elimu hii ya TU-TU ni walimu ambao wamechukua muda mwingi kujitolea katika kufunza elimu hii. Jee ni walimu wangapi ambao mumeshawaajiri ili katika vituo hivi vya *nursery* ambavyo tayari serikali imevianzisha lakini kama hawajaariwa je serikali ina mpango gani wa kuwaajiri walimu hawa ambao wamechukua muda mwingi kujitolea katika kuwafunza watoto wetu elimu hii ya TU-TU.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, ni kwamba kwa sasa hatuna mfumo mahsusi wa uajiri wa walimu wa TU-TU badala yake mfumo wa ajiri uliopo ni kwamba inapotokea nafasi za kazi zinatangazwa na Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Serikali na hapo kila ambaye ana sifa zilizotajwa anaomba. Lakini pia kwa upande wa pili ni kwamba walimu hawa wanatoa mchango mkubwa na pia serikali inafahamu mchango wao kwa hivyo, nafasi zitakapopatikana za ajira zitatangazwa na hawa na wengineo ambao wana sifa wanaojitolea na wasiojitolea wataomba na utaratibu wa kawaida wa ajira utafanyika.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nakushukuru Mhe. Spika na miye kunipa fursa namshukuru Mwenyezi kwa kutuamsha salama kufika hapa salama. Mhe. Naibu Waziri nakuuliza swali langu lenye (a) na (b):

a) Nini maana ya TU-TU

b) Mheshimiwa kila binadamu ana mategemeo katika kufanikiwa walimu hawa mna mkataba nao hata kama hamuwaajiri ili baada ya kumaliza mkataba kuwapatia angalau kifuta jasho.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika.

a) TU-TU hii ni tofauti na ile ngoma unayoijua hayo ni ***Tusome Tujifunze*** ndiyo maana yake tofauti na ile ngoma unayoifahamu wewe.

b) Lakini pia ni kwamba walimu hawa kwa namna fulani ni walimu wa kujitolea na walimu wa kujitolea huwa hakuna mkataba katika kujitolea ni kwamba wameamua wenyewe wanajitolea kusaidia vijana wetu kwa hiyo hakuna mkataba katika kujitolea.

Utaratibu

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Mhe. Spika, natumia kifungu 37. Nilikuwa naomba maana ya TU-TU

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nishamjibu alikuwa hajasikia Tusome Tujifunze, ile TU ya mwanzo Tusome na TU ya pili Tujifunze.

Nam. 46

Kufanya vibaya Timu ya Soka ya Wanawake

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:-**

Matokeo mabaya ya timu ya Taifa ya Wanawake (*Zanzibar Queens*) ya kufungwa magoli 30 –1 yameitia aibu Zanzibar. Lakini tokea matokeo hayo, hakujawa na mipango thabiti na endelevu ya Serikali kuimarisha timu hiyo ili aibu hiyo isitokee tena.

Ni mipango gani Serikali inakusudia kufanya kuimarisha timu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu **:-**

Mhe. Spika, napenda kujibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani wa Jimbo la Jang'ombe swali lake nambari 46. Mhe. Spika kabla ya kujibu swali lake naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, soka la wanawake hapa Zanzibar limekabiliwa na changamoto kubwa katika jamii hata hivyo juhudi kubwa zinafanyika kuhakikisha soka la wanawake linapiga hatua.

Mhe. Spika**,** baada ya maelezo haya mafupi sasa naomba nimjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake namba 46 kama ifuatavyo:-

Ni kweli timu ya wanawake iliyoshiriki katika mashindano ya *CECAFA WOMEN CHAMPIONSHIP* huko Uganda ilifungwa 30 - 1 kwa michezo yote huko Uganda na baadhi ya wadau kusema imetia aibu Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kupata matokeo ambayo yaliwashangaza wadau wengi, Wizara, Baraza na ZFA imekutana na Uongozi wa Soka la Wanawake na wadau tofauti kukusanya maoni yao na kuyafanyia kazi na tayari mikakati imeshaandaliwa ili kuona kuwa aibu hiyo haitokei tena.. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu ya Mhe. Waziri amethubutu kusema kwamba baada ya kipigo hicho walikaa kamati wakaona kwamba matokea yale hayatotokea tena.

a) Je, ni mpango gani au ni ujasiri gani walionao wakati hata hiyo timu yenyewe ya wanawake hazishughulikiwi ipasavyo kwamba kutuletea miujiza ya ushindi katika nchi yetu.

b) Ikumbukwe kwamba nchi yetu katika mwanzo wa mwaka uliopita kuna timu ya Wilaya ya Mjini *under seventeen* ilikwenda kushindana kule *Rolling Stone* kule Arusha na ikachukua ubingwa, siku ya mapokezi nilikuwepo na Mhe. Waziri aliahidi mambo mengi sana kwa wale vijana lakini hadi hii leo hakuna hata mmoja lililotekelezwa kwa wale vijana. Je, wizara yako inatoa tamko gani juu ya kadhia nzima walioahidiwa wale vijana kupelekwa kwa mkuu wa nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

a) Mhe. Spika, kati ya mpango ambao Wizara imechukua kuhakikisha kwamba timu hii inasonga mbele na kuonena kwamba matokea haya hayatokei tena moja kwanza ni kuwaita kama nilivyojibu mwanzo ni kukaa nao hao wadau wa mchezo huu wa *football* wanawake na kuona zile changamoto ambazo zipo za binafsi ambazo changamoto hizi zilisababishwa ni viongozi wa timu na timu na kujionesha kwamba kuwasafirisha kwao wale kila timu ilitaka kwamba mchezaji wangu huyu aende huyu asende kwa hiyo hii ilisababisha pia kutokea hili lililotokea na kwa hivyo, sasa tumelichukua hatua na tutahakikisha kwamba linasonga mbele.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utali na Vijana: Mhe. Spika, naomba suala (b) arejee kidogo sikulisia vizuri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Ahsante sana Mhe. Spika, alivyouliza kwamba alitaka kujua ahadi tulizoziahidi na zipili zilizotekelezeka na ambazo labda nyingi hazijatekelezwa.

Ni kweli kwamba tunaishukuru sana timu ya Wilaya ya Mjini kwa kushiriki mashindano ya *Rolling stone* kule Arusha na kuweza kupata ushindi na kuanza kutuwekea sura njema ya vuguvugu la mpira wa miguu hapa Zanzibar tunaishukuru sana timu ya Wilaya ya Mjini. Miongoni mwa ahadi ambazo ziliahidiwa ilikuwa ni kuletwa hapa Baraza la Wawakilishi kuja kuoneshwa kwamba wameshiriki mashindano kama tulivyowachangia na wamerudi na hiyo jitihada ya kupata ushindi, suala hilo linategemea kukaa kwa Baraza na tayari tumezungumza wakati wowote wanaweza kuletwa hapa wakaja wakaoneshwa.

Kulikuwa kuna ahadi nyengine kwamba wapelekwe kwa Mhe. Rais baada ya kushinda kile kikombe cha mashindano waliyoshiriki lakini kwa vile, timu iliyoshiriki ilikuwa ni sio timu ya Taifa wala haikushiriki mashindano ya kimataifa kwa hivyo, haikuingia katika zile daraja na Wizara imelichukua hilo inaweza kufanya kuwapa hongera Wizara kama Wizara.

Mwisho kabisa washindaji wale tuliwahidi zawadi ambazo tuliweza kuwapa mara pale walipofika na tunaendeleza kuwa nao ilii tuhakikishe kwamba mpira wanauendeleza kuucheza vizuri. Mwisho kabisa Mhe. Spika nashukuru sana sana kwa vuguvugu lillotokea pia nawashukuru sana wapenzi wa Simba kwa ushindi walioupata juzi ulikuwa ni wa dhahiri. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame: Mhe. Spika sababu kubwa iliyosababisha timu ile kufungwa magoli mengi kwamba wachezaji hasa wale wa Timu ya Taifa hawakuchaguliwa kwenda katika ile Timu ya Taifa, uthibitisho upo kwamba wachezaji haswa waliachwa wakachukuliwa wachezaji ambao hata mazoezi hawaendi ndo maana tukasabishwa kufungwa magoli yale, je Mhe. Wiziri Wizara yake imechukua hatua gani kuondosha kitendo kile na kumuadhibu yule mwalimu aliyechagua wachezaji wale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya wachezaji ambao wamechaguliwa kushiriki katika mashindano yake hawakuwa wachezaji wa Timu za Taifa lakini hii kama nilivyoeleza mwanzo ilitokana na wale wasimamizi wa timu zile ambazo tunazo hapa za soka la wanawake kuzozana kwao kwa kila timu wanataka mchezaji wake ashiriki, yule ambaye hakushirikishwa wale viongozi wa timu zile au makocha wa timu wakawazuia wachezaji wale wasishiriki. Lakini kwa upande wa wizara kwanza kwa wachezaji ambao hawakushiriki katika mashindano yale imeamua kuwasimamisha, lakini pia kwa upande wa walimu bado hatua hazijachukulia lakini hili nitalichukua na tutakaa na uongozi tuone kwamba na wale walimu na wao wanawajibishwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri kwa majibu yao kuhusiana na Timu ya Taifa ya Wanawake, lakini kwa vile Zanzibar tunatategemea kupata uwanachama wa Chama cha Mpira wa Miguu Afrika na baada ya kupata uwanachama huu timu yetu ya Taifa ya Wanaume inategemea kushiriki katika mashindano ambayo ya Afrika (*AFCON*). Lakini baada ya kupata uwanachama huo timu yetu itakuwa inashirikia mashiriki hayo. Je, ni maandalizi gani ambayo yanafanywa kuhakikisha kwamba baada ya kupata uwanachama huo timu yetu ya Taifa inashiriki vyema kushiriki mashindano hayo ili kuondokana na aibu hii ambayo tumeipata.

b) Kwa vile imekuwa Zanzibar ni matatizo kupata wadhamini katika timu zetu za Taifa hata vilabu ni sababu gani za msingi ambao ndio zinafanya Zanzibar kukosa wadhamini katika vilabu na timu yetu ya Taifa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, ni kweli kwamba tuna matarajio makubwa ya kupeleka maombi yetu ya kujiunga na uwanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu, Afrika na Mwenyezi Mungu akitujaalia mnamo mwezi wa Machi, inshaallah kwa baraka zake tutapata na Zanzibar tutakuwa ni wanachama kamili.

Katika swali la (a) aliuliza endapo tutapata vitu hivyo sasa timu yetu ya mpira tunaiandaa vipi. Mikakati mikubwa tumeaza kuiweka, Mhe. Spika jana ungekuwa shahidi na yeye alihudhuria ameona namna gani tumeaza kuibua vipaji na kushirikisha vijana wetu kushiriki katika michezo hii ya mpira wa miguu ili vipaji viwe wazi. Tumeaza mashindano hapa ya majimbo, waheshimiwa wote walishirikishwa, wamechangia majimbo, wamechangia kupata zawadi na zawadi kubwa zitatolewa ili kuhakikisha kwamba mpira wa Zanzibar unarudi hadhi yake kama ulivyo zamani.

(b) Aliuliza kwamba wafadhili tunaweza tukawapataje. Nataka nimuhakikishie kwamba tayari tumefanya mikutano miwili ya kuwaita wafanyabiashara wote wakubwa wa Zanzibar na nje ya Zanzibar Dar es Salaam na wote kwa pamoja tumezungumzia namna yakuweza kushiriki kuikuza *football* ya Zanzibar na wao kuweza kufadhili michezo hiyo.

Mhe. Spika, takriban wafanyabiashara wote na tangaza hapa kwamba wamekubali na wamekubailana na wizara kuanza kufanya ufadhili kwa timu zetu za Zanzibar, walichokitaka wao ni kidogo tu yale mababaishaji mambo yaliyokuwa yanatokea kwenye vilabu vyetu na vyama vyetu vya *ZFA* na vyenginevyo tuweze kuyasitisha na hilo tumelikubali. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi mheshimiwa timu zetu zitafanya vizuri na watu watarajie tu makombe huko tunakokwenda. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 63

Utatuzi wa Mgogoro Baina ya Wanakijiji na Hifadhi

Mhe. Asha Abdalla Mussa - Aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu baina ya wanakijiji wa Mchekeni – Kiwengwa na msitu wa hifadhi kwa ajili ya makaazi na msitu.

a) Je, wizara inautambua mgogoro huo.

b) Je, kama inatambua ni lini mgogoro huo utamalizwa ili wananchi wapate kukaa bila ya bugudha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika ahsante sana napenda kumjibu Mhe. Asha Abadulla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa i swali lake Nam. 63 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu inatambua kuwepo kwa wananchi wanaoishi katika Kijiji kipya cha Mchekeni ambacho kimo ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa - Pongwe.

Mhe. Spika, naomba nieleze kwamba wizara yangu kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ilianza mchakato wa kuupandisha hadhi Msitu wa Kiwengwa - Pongwe kuwa Msitu wa Hifadhi kwa tangazo la serikali la mwaka 2002 ("*Notice of Intent*" namba 5671 ya tarehe 25 Oktoba, 2002). Katika kufikia hatua hiyo wizara ilifanyakazi ya kukusanya maoni ya wanajamii wenye madai mbali mbali kutokana na mali zilizomo ndani ya hifadhi hiyo.

Katika kuanzisha hifadhi hiyo, wizara yangu kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ilifuata taratibu zote za kisheria za kuanzisha hifadhi hapa nchini. Tulizishirikisha Taasisi za Serikali za Wilaya, wadau na vijiji vinavyozunguka msitu huo ili kupata maoni yao juu ya kuanzishwa hifadhi hiyo. Bahati nzuri kati ya wananchi walijitokezaa kutoa maoni yao walio wengi walikubali kuanzishwa kwa hifadhi hiyo wakiwemo wananchi wa Shehia ya Kiwengwa ambayo inajumuisha Kitongoji cha Mchekeni.

Mhe. Spika, wizara yangu ilifanya ukaguzi wa maeneo yote ambayo wananchi walikuwa na mashamba au maeneo ya kilimo kwa ajili ya kufanya tathmini ya mali zao ili waweze kufidiwa na serikali. Katika kutekeleza kazi hiyo, Shehia ya Kiwengwa iliorodhesha wananchi wapatao 40 ambao walikuwa na mashamba madogo madogo wakiwemo wa eneo la Mchekeni. Wengi wa wananchi walionesha maeneo yao ya kilimo katika eneo la Mchekeni walikuwa pia wakijishughulisha na kazi ya kuchimba mawe na kuvunja kokoto kibiashara. Kwa wakati huo wananchi wasiozidi watatu walikuwa wamejenga vibanda vya miti na kuishi katika eneo hilo la Mchekeni.

Mhe. Spika, pamoja na kufanya maamuzi ya pamoja na wananchi wa Shehia zote zinazozunguka hifadhi ya Kiwengwa-Pongwe ya kuwataka kuacha kulitumia eneo lililotengwa kama hifadhi, kuna baadhi ya wanajamii

wakiwemo wa Kitongoji hicho cha Mchekeni waliendelea kupanua shughuli zao (kilimo, ujenzi, kukata miti na kuchimba mawe na kokoto kibiashara) licha ya makubaliano ya wao kutofanya hivyo.

Hata hivyo, wananchi wa Kitongoji cha Mchekeni walionekana kuvinjari zaidi kwa kuweka makaazi ya kudumu licha ya elimu kubwa iliyotolewa na wizara yangu kupitia vikao mbali mbali na hivyo kuanzisha mgogoro wa makaazi na matumizi ya maliasili zilizopo katika eneo hilo ambalo limo ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Kiwengwa-Pongwe.

Mhe. Spika, wizara yangu inatambua thamani ya wananchi ambao ni sehemu ya wadau wa usimamizi wa hifadhi hiyo.

Hivyo basi, katika mwaka 2013 mzozo huo wa makaazi na matumizi wa maliasili ziliomo ndani ya hifadhi hiyo, ulipatiwa ufumbuzi kwa kutengwa eneo kiasi cha hekta 30 katika Kitongoji hicho na kuwekwa kama eneo la usimamizi maalum kwa ajili ya makaazi na matumizi ya wananchi hao, eneo hilo liliwekwa mipaka na Idara ya Ardhi kupita Mradi wa *SMOLE*.

Mhe. Spika, kama ilivyo katika vitongoji vyengine jirani na hifadhi hiyo wana jamii hao walitakiwa waishi hapo wakiheshimu taratibu na matumizi ya hifadhi hiyo. Hata hivyo, wananchi wanaoishi katika Kitongoji cha Mchekeni maarufu Mwanza wamekuwa wakipuuza taratibu za hifadhi na badala yake kila kukicha wanataka kuongeza maeneo zaidi na kutumia maliasili za kuni, miti na mawe ambazo zimo ndani ya hifadhi mkabala na eneo walilopewa kwa matumizi yao.

Mhe. Spika, wizara yangu haina lengo la kuwasumbua wala kuwabughudhi wana kijiji wa Mchekeni, ikumbukwe kwamba msitu huu ndio pekee uliobakia katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, kama tutaendelea kuuharibu basi tujue kwamba tunakaribisha majanga ya kimazingira sio kwa Mkoa wa Kaskazini tu bali kwa Unguja nzima. Katika kuwasaidia wananchi hao pamoja na vijiji vyengine vinavyozunguka hifadhi hiyo, wizara yangu imekuwa ikianzisha miradi mbali mbali, miradi mbadala ya kujipatia kipato kwa wana jamii hao badala ya kutegemea kuharibu msitu na maliasili zilizomo ndani ya hifadhi. Miradi hiyo ni pamoja na kilimo cha mboga, mboga, ufugaji wa nyuki mabandani na upandaji wa miti inayotoa mazao ya muda mfupi.

Pia wizara yangu imeanzisha mipango ya makubaliano ya usimamizi wa maeneo ya misitu ya jamii kwa shughuli za kijamii ambapo wana jamii wa Mchekeni ni sehemu ya makubalino hayo. Juhudi hizi zinalenga kuondoa mgogoro wa makaazi na matumizi wa msitu wa eneo hilo. Ahsante .

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Nabu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako umeelezea kwamba msitu ulianzishwa mwaka 2002, lakini 1998 baadhi ya wananchi wapatao 40 walikuwa wakiishi hapo pamoja na hawa wananchi wasiozidi 3 waliojenga vibanda vya miti. Lakini wizara yako kupitia Idara ya Misitu iliorodhesha watu hao kwa ajili ya kulipwa fidia zao, kwa ajili wahame katika msitu wa hifadhi nakwenda kuishi katika eneo lilotengwa. Lakini mpaka sasa wananchi hao hawajalipwa fidia hizo.

Je, ni lini wizara yako itawalipa fidia hizo ili kuondosha migogoro ya kila siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwakilishi nitaomba muda niende nikafanye utafiti kama wamelipwa ama hawajalipwa ili baadae nijue. Kama hawajalipwa basi nakuahidi tutawalipa na kama wamelipwa basi itakuwa ndio tayari wameshalipwa. Ahsante.

Nam. 50

Kukosekana Huduma ya Maji ya Bomba Shehia ya Mtangani

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:-

Shehia ya Mtangani ilikuwa ikipata maji ya bomba kutoka kisima kilichopo Kwapopo Shehia ya Chambani lakini kwa muda mrefu sasa maji hayo hayapatikani hata kwa njia ya mgao.

a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inalifahamu suala hili.

b) Ni lini watu wa Mtangani watapata huduma hii ya maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa wa Kimbo la Kiwani swali lake Nam. 50 kama ifuatavyo lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, wananchi wa Mtangani walikuwa wanapata huduma ya maji kutoka kisima cha Kwapopo kilichopo Chambani. Kutokana na mahitaji makubwa ya maji ndani ya vijiji vya Chambani, huduma hiyo ilianza kupungua na hatimae kutofika kabisa katika Shehia ya

Mtangani. Kwa hivyo, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira inafahamu kwamba huduma ya maji haifiki katika Shehia ya Mtangani.

b) Ili kuweza kuwapatia wananchi wa Shehia ya Mtangani huduma ya maji ya uhakika, Mamlaka ya Maji inatarajia kuchimba kisima katika maeneo ya karibu na Shehia hiyo. Kwa hatua za awali, Mamlaka ya Maji imeshakagua eneo la kuchimba kisima hicho. Hatua zinazoendelea ni kukusanya nguvu za kuchimba kisima hicho, ujenzi wa kituo, vifaa vya *wellhead*, kupata gharama za umeme, bomba, kutoka kilipo kisima kinachotarajiwa kuchimbwa na kuunga mkono bomba lililopo. Kwa hivi sasa, Mamlaka ya Maji inafanya mazungumzo na uongozi wa Jimbo kuona namna utakavyoweza kusaidia ujenzi huo. Kwa upande wake, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imepanga kutekeleza ujenzi huo ndani ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba watu wa Mtangani kwa muda mrefu hawapati maji, na kwa kuwa mpango uliopo wa kuchimba kisima kingine utachukua muda. Je, Mhe. Waziri haoni iko haja ya kuurudisha ule mpango wa mgao japo kwa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa sababu makaazi yamekuwa na wananchi wengi wamehamia katika eneo lile na miundombinu yetu kutokana na uhalisia wa watu kukata maji huku na kule hata ukifanya mgao hayafiki eneo lile la Mtangani. Kwa bahati nzuri Naibu Waziri alikwenda na watu wa maji kulitazama eneo hili lakini ikaonekana hata tukiweka mgao kwa sasa hivi haitowezekana, na ndio maana wizara ikaamua kufikiria kuchimba kisima katika eneo jengine.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa nafasi uliyonipa na mimi ningependa kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwa kuwa Jimbo langu la Tunguu ni katika majimbo ambayo yanapata uhamiaji wa watu kutoka kwenye rika, fikra na mawazo tofauti kwa wingi na suala la maji limekuwa ni mtihani hasa maeneo ya Tunguu yenyewe pamoja na Bungi na pia katika maeneo ya Binguni, Dunga

pamoja na Unguja Ukuu. Je, Mhe. Waziri ni lini hawa wananchi angalau matatizo yao haya yatapata kuondoka.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa inazungumzia katika kuwaondolea umasikini Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla masuala ya maji, elimu na mengineyo. Ni lini Mhe. Waziri utapanga mkakati ambao utaendana sambamba baina ya sisi Baraza la Wawakilishi pamoja na serikali ili mpango huo uweze kuwafikisha wananchi wetu na kuondoa hizi adha na matatizo yanayowakuta juu ya suala la maji. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa serikali inafahamu umuhimu wa kuwa na maji safi na salama kwa wananchi wake, na dhamira ya serikali ni kuwapaStia wananchi wake maji katika maeneo yote na mimi pamoja na yeye tukishirikiana tulishaaza kufanya kazi katika maeneo husika ambayo yeye mwenyewe ameyasema na bahati nzuri tuliaza kufanya kazi hiyo na yeye mwenyewe ana mpango mahsusi ambao ameupanga kwa kushirikiana na Mamlaka ya *ZAWA* ambao yeye mwenyewe binafsi alitaka tushirikiane katika kuhakikisha wananchi katika maeneo hayo wanapata huduma hiyo.

Mhe. Spika, swali la pili sikulifahamu naomba Mheshimiwa arudie.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, nilihisi pia ataniuliza kwa sababu hakunifahamu kwa sishangai. Mhe. Spika, naomba niurudie swali langu. Swali ni kwamba masuala ya maji, elimu na mengi haya yamekuwa yanaumiza serikali miaka nenda rudi ambayo si Tanzania tu au Zanzibar ni maeneo mengi. Suala la maji nauliza hivi, ni lini serikali itafanya mpango rasmi ambao ni kama *stratergy* mkakati wa makusudi ili watu wote baina ya serikali na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukawa katika *frequency* moja yaani tuko katika mawazo sawa ili tukenda sambamba na masuala haya ya maji kuliko sasa hivi maana yake kila mmoja anatafuta njia *pipe*, maji, kisima anachimba huku hatujui baina ya serikali na Baraza tuende vipi. Kwa hiyo, ni lini mtaleta mkakati ili sisi tuwe pamoja sote. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, serikali ina mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata maji safi na salama na ndio maana juhudi na jitihada nyingi serikali inazifanya katika kuhakikisha kwamba inapata *funds* za kuhakisha kwamba mkakati ule unatekelezeka. Na ninaomba nimwambie kwamba serikali hii inawajali sana wananchi wake na huduma ya maji itakamilika ifikapo pale kwenye *Vision*

2020 umejieleza kabisa. Kwa hiyo, mimi ninachotaka kumwambia subra yavuta kheri na serikali itaendelea kutimiza mkakati wake kama walivyojipangia na kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama kama ilivyopangwa.

Nam. 73

Tatizo la Maji Ngwachani

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Serikali imefanya jitihada kubwa kuwasaidia wananchi wake kuwaondoshea tatizo la maji, lakini kama tunavyojua kwamba vijiji vyetu ni vingi sana na hivyo bado tunahitaji msaada zaidi.

Katika Jimbo la Chambani kuna visima vya Ras al Khaimah na visima hivi mpaka leo havijatumika kutokana na matatizo mbali mbali.

a) Je, kisima kiliopo Ngwachani ni lini kitafanya kazi.

b) Ngwachani lipo tangi la maji ambapo nguvu nyingi za wananchi zilitumika katika kuweka tangi hilo lakini tangi hilo halijawanufaisha wakaazi wa eneo hilo. Je, ni lini wananchi hawa watapatiwa tangi jengine.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo wa Jimbo la Chambani swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kisima cha Ngwachani ni miongoni mwa visima vilivyo chimbwa katika mradi uliosaidiwa na Serikali ya Ras al Khaimah. Kwa sasa hivi, Mamlaka ya Maji imeanza kujenga sehemu ya bomba kubwa la maji kutoka kilipo kisima kikongwe kwa kushirikiana na wananchi hadi kufikia lilipo bomba kubwa linalopeleka maji kwa wananchi. Kazi hizi zilitekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017. Kwa hatua ya pili, Mamlaka ya Maji inatarajia kujenga sehemu ya pili ya bomba hilo kutoka kisima kikongwe hadi kilipo kisima kipya. Kazi hii inatarajia kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa bajeti 2016/2017.

(b) Hatua ya tatu ilikuwa ni kujenga *wellhead* sambamba na kufunga vifaa vitakavyowezesha huduma ya maji kuweza kuwafikia wananchi katika maeneo yao mbali mbali. Hatua hii itatekelezwa mwanzo wa mwaka wa fedha 2017/2018.

(c) Mnara wa tangi la kuhifadhia maji uliopo Ngwachani ulijengwa na Mamlaka ya Maji katika mwaka 2003. Taasisi ya *Al-Youseif Charitable Society* ilisaidia tangi hilo la sandarusi *(glass reiforced plastic),* ambalo tayari lilikuta limeshatumika huko lilikotoka. Tangi hilo lilitoa huduma kwa kipindi kifupi na lilianza kuvuja kiasi kilichopitiliza. Kwa hivi sasa, Mamlaka ya Maji haijapanga kuliondosha tangi hilo na kufunga tangi jengine. Hata hivyo, wananchi wataendelea kupata huduma ya maji ya moja kwa moja kutoka kisima *(direct pumping).*

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe Waziri kwa kuwa wananchi wa Ngwachani wanapata shida ya maji na mamlaka haina mpango wa kuliondosha tangi hilo. Je, haoni kwamba wananchi hawa hakuna haja ya kujengewa tangi jengine kwa vile vijiji vimekuwa na maji ya moja kwa moja baadhi ya wananchi wengine wanayakosa kabisa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli wizara yangu bado haijaona haja ya kuliondosha lile tangi kutokana na uwezo, lakini maji katika vijiji vile yanakwenda na wananchi wanapata maji hata kwa mgao kutokana na ile *direct pumping*. Lakini pale wizara itapokuwa na uwezo wa kuhakikisha kwamba wanaweza kuliondoa tangi lile na kuweza kuweka tangi jengine.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa mimi nataka kumuuliza waziri katika kisima kikubwa na kikongwe pale Ukitini kwa Kichwa kinatoa maji ya tofauti ambayo yanakuwa na *iron*. Kisima kile watu walikigomea wakafikiri kitakuwa na maradhi au kuna matatizo ya maji. Lakini wataalamu wamesema maji yale ni muhimu sana na yanasaidia mpaka kwa nguvu za kiume. Je, waziri analijua hilo, kama analijua amechukua hatua gani kutangaza ili maji yale yawe mali.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza naweza kumwambia suala hilo kwa sasa hivi silijui na ninajua athari ya *iron* kwa sababu itakuwa na *fluorine* nyingi, lakini kwa sababu ni suala la kitaalamu

zaidi naomba nilibebe na niweze kwenda kukaa na wataalamu wangu ili tuweze kulifanyia kazi na baadae niweze kumpa matokeo ya kazi hiyo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mheshimiwa mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri lakini vile vile nichukue fursa hii kuipongeza serikali katika mikakati yake ya kuondoa tatizo hili la maji. Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba kuna mfadhili ambaye amemtaja ambaye alifanya ufadhili wa lile tangi ambalo lilikuwa halina kiwango na baada ya muda mfupi likawa halifanyi kazi. Lakini tatizo hili limekuwa likijitokeza katika maeneo mbali mbali kwa wafadhili, kwa Wabunge na Wawakilishi.

Je, kama waziri ana mikakati gani au ushauri gani kuhakikisha kwamba anatoa ushauri ili wale ambao wanatoa misaada yao kuwashirikisha wataalamu wa *ZAWA* ili kuendana na kupata vitu ambavyo vina ubora na uhakika wa kufanya kazi vizuri kuondoa tatizo la maji.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna watu wanaleta msaada lakini mkakati ambao upo sasa hivi mimi nikishirikiana na Mamlaka ya *ZAWA* na Bodi yao nafikiri ndio agizo langu la mwanzo nililotoa kwenye bodi kwamba sasa hivi misaada yote inayokuja kwanza waangalie viwango na ubora wa ile misaada inayokuja. Kwa sababu mara nyingi unaposaidia unapokea lakini unapokipokea unaangalia kile kiwango sio tupkee tu, kwa sababu hata wakati mwengine tunapata hasara unafanya kazi kubwa ya mabomba kama hivyo kuweka matangi lakini ya msaada; lakini baada ya muda mfupi mabommba au matangi yale yanakuwa mabovu ambayo hayaendi wala hayakidhi vigezo. Kwa hivyo, kwa sasa hivi tuna mkakati madhubuti na ninaamini bodi yangu itafanya kazi vizuri ya kuhakikisha kwamba misaada yote wanayoipokea basi wanashirikiana na *management* kuhakikisha kwamba wanapokea vifaa ambavyo vyenye ubora zaidi.

Nam. 70

Ukosefu wa Chombo cha Kupimia Mizigo Mapinduzi II

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza:-

Tumeshuhudia abiria wanaosafiri Unguja kwenda Pemba kwa meli zetu hususan MV Mapinduzi II wakipata usumbufu kwa kutozwa kiwango kikubwa cha fedha kwa ajili ya mizigo ukilinganisha na mzigo yenyewe na kubwa ni

kukosekana chombo cha upimaji wa uzito wa mizigo hiyo na kupelekea kufanya makisio tu.

(a) Je, ni kiasi gani cha malipo ya fedha kinachostahili kulipa abiria aliebeba kipolo cha mzigo, kitanda, charahani, pakacha ya kuku na kadhalika.

(b) Ni lini patakuwa na kifaa cha kupimia uzito wa mizigo midogo midogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe swali lake Nam. 70 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kawaida Shirika la Meli huwa linatoza ada ya mizigo kulingana na hali ya mzigo husika na viwango vinavyotozwa kama ada na Shirika. Mizigo yote inayochukuliwa mkononi *(Hand Luggage)* huwa hailipishwi, kipolo cha kilo hamsini (*50 kgs*) kinatozwa Shilingi 2,000, charahani shilingi 5,000 na pakacha ya kuku hutegemea ukubwa wa pakacha husika.

(b) Shirika la Meli kwa hivi sasa halina mpango wa kuweka kifaa hicho cha kupimia uzito wa mizigo midogo midogo.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali jengine la nyongeza. Mhe. Spika, tumeshuhudia Uwanja wa Ndege tukipita kama begi imekuwa kuna kifaa maalum ambacho kinapima uzito wa mzigo ule, lakini na sisi ni Waisilamu, *Almizanu Hakku* na anasema kwamba wizara yake haina mpango wa kupima pakacha au kipolo cha ndizi na amesema ni shilingi 2000. Je, kwa kutumia macho matupu watajuaje kama mzigo huu umefikia hiyo kilo hamsini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sote tunajua kwamba kuna viwango maalum vya vipolo ambavyo mfano mchele wa kilo 50 tunaweza kutambua na kilo 25 tunavijua. Sasa ndizi kwa kawaida hatutii katika vipolo, ndizi zinakuwa zinachukuliwa kikawaida kwa hivyo, sisi huwa tunautoza ule mzigo kwa mujibu wa ukubwa husika. Kwa hivyo, ndizi hatuzitii katika vipolo na iwapo zitatiwa katika vipolo basi kwanza

kuna tatizo la hiyo ndizi yenyewe kuharibika. Mimi namuomba sana hicho kifaa tutaangalia uwezekano hapo baadae ili tukinunue lakini hata Azam nao hawana vifaa pale bandarini vya kupimia bali wanapima kwa mujibu wa kuangalia ule mzigo. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Mhe. Waziri nataka nimuulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa utaratibu kwenye Meli ya Mapinduzi II halina utaratibu mzuri na inapelekea kuleta msongamano kwa baadhi ya mizigo ambayo haieleweki kama ni mizigo ya kulipia ama sio ya kulipia kupitishwa katika mlango mmoja tu, na kwa sababu meli yetu hii ina mlango mmoja. Nataka kumwambia Mhe. Waziri ni taratibu gani ambazo wizara inahisi ya kuondosha usumbufu kwa kutumia mlango mmoja kwenye meli yetu ya Mapinduzi II.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, tunajua kwamba meli yetu ina changamoto kwamba ina mlango mmoja kwa mujibu wa viwango ilivyotengenezwa, lakini hivi sasa tuko katika mpango kutaka kuhakikisha kwamba bandari yetu ya Malindi, Mkoani na hata Dar es Salaam tunajenga miundombinu maalum na kuhakikisha kwamba ile milango ya pembeni inafunguka ili badae mizigo ipate kuingizwa kwa urahisi zaidi na kuwaondoshea watu matatizo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru kwa kuniona. Mimi nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba katika meli tunabeba watu wengi sana pengine kuanzia watu 1000 na kuendelea ambao ni mkusanyiko wa watu wengi hasa wanawake na watoto kwa kusafiri katika kisiwa chetu.

Je, kuna mtu anayehusiana na wanawake na watoto ili udhalilishaji ukitokea mtu yule aweze kuwasaidia. Kama hakuna je, utaratibu wa kumtafuta mtu na kumuweka pale mnao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sisi katika meli yetu hasa hii ya Mapinduzi II kuna wafanyakazi wahudumu wanawake. Kwa hivyo, kunapotokea tatizo lolote la wanawake wanakuwa wako tayari kuwasaidia wale wanawake kuhakikisha kwamba matatizo au huduma yoyote ya awali wanawapa wanawake wale. Ahsante mheshimiwa.

Utaratibu

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, Kanuni ya 37 nimemuuliza labda hakuifahamu. Nimemuuliza kwamba mtu anayejua haki za mwanamke na

watoto ambaye anatoka katika Wizara ya Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto sio kwamba kuna wahudumu. Je, yupo mtu pale ambaye analinda haki za mwanamke na mtoto katika mkusanyiko ule. Maana yake hawa wafanyakazi wengine wanawadhalilisha wanawake na watoto. Kama hayupo je, kuna utaratibu gani wa kumweka mtu ili kulinda haki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ahsante naomba radhi kwamba sikumfahamu kwa sababu alizunguka sana katika swali lake. Kwa ufupi Mheshimiwa katika meli zetu kunakuwa na *CCTV Camera* kwa hiyo kitendo chochote kinachotokea kinaonekana na hatuna utaratibu sasa hivi wa kuweka watu wa kitengo chengine kwa sababu Shirika lolote la Meli linaajiri wafanyakazi kwa mujibu wa kada husika. *(Makofi)*

Nam. 113

Kuajiriwa kwa Mlinzi katika Mnara wa Kichunjuu – Pemba

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza:

Mnara wa Kichunjuu uliopo Mkoani, Pemba unatumia walinzi wa kukodi.

Je, serikali haioni kuwa kuna haja ya kuwa na mlinzi aliyeajiriwa katika mnara huo

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Shehe Hamad Matar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni swali lake Nambari 113 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mnara wa Kichujuu uliopo Mkoani, Pemba unamilikwa na *ZANTEL*. Hivyo ni uamuzi wa *ZANTEL* kuweka mlinzi wa kukodi au kuamua kuajiri mlinzi katika eneo hilo moja kwa moja, kwani mshahara na mafao mengine yote husika hutolewa na kampuni husika yenye kuajiri.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kujibu swali langu vizuri, lakini naomba nimuulize swali la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi sana wenye minara hii hutiama pahali ambapo imepatikana *network* je, katika sehemu ile hapana minara ya *TTCL* ambayo inahitaji walinzi kama hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, samahani kidogo kuna *echo* naomba aongeze sauti kidogo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kaa karibu na *microphone* ili akusikie.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Kwa kuwa mara nyingi sana wenye kuhitaji minara hutizama pahali ambapo wenzao wamepata *network* vizuri. Je, katika sehemu hiyo hakuna minara ya *TTCL* ambapo inahitaji watu kama hao nilioulizia kwa kuajiriwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo minara yote hii inategemea na taratibu za ajira zilivyo kwa kampuni husika, *TTCL*; *ZANTEL*; *Halotel*; *Tigo* zote wana utaratibu wao na wao ndio wanaotoa mfano ajira au mafao kwa wafanyakazi husika wakiwemo walinzi. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu uliokuwepo na sisi kama serikali huwa tunafuatilia maslahi ya wafanyakazi pale ambapo tunaona kuna haki imekuwa haikutendeka.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi ningependa kuuliza swali dogo tu la nyongeza kuhusu suala la minara. Kwa kuwa hivi sasa makampuni haya ya simu mengi katika eneo wanalolitegemea sasa hivi ni zaidi kutumia data ili kupata kutumia huduma ya mtandao kuliko upigaji wa simu au upokeaji. Katika jimbo langu kuna kisiwa cha Uzi mawasiliano hasa ya kutumia mambo ya mtandao imekuwa ni mtihani. Ni lini Mhe. Naibu Waziri ataweza ataweza kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kupata huduma hii ya mtandao kwa ajili ya faida yao pamoja na vijana wao kujisaidia kwenye masuala ya elimu.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri kama unaweza kulijibu hili swali nitakuruhusu vyenginevyo ni swali jipya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, suala hilo ni kweli ukienda kule Uzi na Ng'ambwa kuna matatizo hasa kwa mtandao wa *Tigo* na pengine *ZANTEL* unapata kidogo unapokuweko milimani juu. Sasa mimi tutakaa na makampuni kwa sababu hii ni kazi ya biashara ili pake wanapoona pana tija basi na kule wapeleke mnara ili kurahisisha mawasiliano. Lakini kwa utaratibu siku hizi makampuni yamekuja na mbinu mpya kila minara ikienda juu zaidi kuanzia mita 60 mpaka 90 basi yale mawasiliano yanafika maeneo ya mbali zaidi na *ZANTEL* wako katika kutaka kurekebisha huduma hizo na *Halotel* nao wamo katika kupeleka huduma hizi mbali zaidi. Kwa hiyo, mimi nina imani kubwa sana ikifika minara hii maeneo

ya Unguja Ukuu basi hata Uzi, Ng'ambwa watakuwa tayari wanapata yale mawasiliano. Mhe. Spika, ahsante.

Nam. 99

Mpango wa Kupata Wataalamu katika Hospitali ya Abdalla Mzee

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali imetoa fedha kwa ajili ya kukodi nyumba za madaktari watokao Unguja kuja kufanya kazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee na kwa kuwa baadhi ya madaktari hao inadaiwa kuwa kwa sasa hawako tayari kukaa Pemba kufanya kazi.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuwasomesha wataalamu kutoka maeneo ya karibu na hatimae kuwaajiri katika hospitali hiyo ili kupunguza gharama za uendeshaji wa hospital hiyo.

(b) Je, serikali haioni kwamba kufungua Tawi la Chuo cha Afya Pemba kunaweza kusaidia kuwapata vijana wengi ambao watakuwa tayari kufanya kazi Pemba kama ambavyo wamefanya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika ahsante, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 99 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, taratibu za utumishi zinamtaka muajiriwa kufanya kazi sehemu yoyote katika Zanzibar na kwa sasa wizara hatuna taarifa ya moja kwa moja kwamba wapo wafanyakazi ambao hawako tayari kukaa Pemba na kufanya kazi huko.

Mhe. Spika, viongozi wa Wizara ya Afya wanafuatilia kwa umakini shutuma hizi baada ya kupata malalamiko na mara utakapopatikana uhakika sheria kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi zitachukuliwa kwa wafanyakazi hao na serikali haitowavumilia.

Mhe. Spika, serikali haina mpago wa makusudi wa kusomesha wataalamu kutoka maeneo ya karibu kwa ajili ya kuwaajiri katika hospitali hiyo, isipokuwa tunajua kwamba wapo wananchi au vijana ambao wamemaliza masomo yao katika Chuo chetu cha Afya basi tunawataka waombe uajiri nasi tutaishauri taasisi inayohusika kuwapa kipaumbele.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mimi kwanza nashukuru kwa majibu yake mazuri lakini kama nilivyosema kuwa tayari habari hizi zimeanza kuzagaa zagaa mpaka zikatufika sisi kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi hasa wataalamu wazalendo kwamba hawako tayari kwenda kufanya kazi pale Mkoani kwenye ile Hospitali ya Abdalla Mzee. Kwa kuwa ameshanijibu Mhe. Naibu Waziri kwamba suala hili wao hawana uhakika nalo, swali langu linakuja.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwadhibiti hawa wafanyakazi ambao watagundulika ili kuendelea kufanya kazi hapo hospitali ukiachilia mbali wale ambao wameomba kwenda kusoma. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali kabla haijawapa uhamisho wa kwenda Pemba katika Hospitali ya Mkoani iliandaa makaazi pamoja na mambo muhimu ambayo binaadamu anastahili kuyapata akiwa yuko pahali na ambayo yatampa utulivu wa kukaa na kufanyakazi zake, ikiwemo maskani yaani makaazi kwa wafanyakazi hao.

Mhe. Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi kwamba baada ya kuwapatia makaazi na kuhakikisha watakaa na kufanyakazi kwa uhakika kama lipo hili ambalo linasemekana lipo basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao. Lakini tayari wizara ina hakika kwamba wapo na wametulia wanafanyakazi linalotokea ambalo tunalitilia wasiwasi kwamba huenda wananchi wanalilalamikia ni ile tabia ya baadhi ya wafanyakazi na hili napenda nitoe wito kwa wafanyakazi wote wa wizara ya afya ambao wako katika Hospitali ya Mkoani na sehemu nyengine vile kujiona wako karibu pale meli ikija haraka haraka wanaweza wakawahi zile siku zao ambazo ni za *off* wale wanaitumia ile Mhe. Spika.

Sasa kama binaadamu siku nyengine anatakiwa arudi kesho anashitukia kesho hakuna usafiri anarudi kesho kutwa kitu ambacho ni kosa na wanaondoka ile bila ya kutoa taarifa katika wizara yao wanachukulia tu kwamba mie siku fulani nna *off* mbili au nina *off* tano basi nawahi kwenda mara moja na nikarudi wakati binaadamu huwezi kuhakikisha wakati ratiba zetu zote zinapangwa na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, nakuhakikishia kwamba hili tutajitahidi wizara kulidhibiti kwa kukaa na wafanyakazi wetu na kuwataka wakae katika sehemu zao za kazi na wakibidi kuondoka basi wawe wanatoa taarifa maalum ili mfanyakazi mwengine asogee katika kitengo kile na kutoa huduma. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kama tunavyofahamu wakati wa kusomesha wanafunzi huchukuliwa Pemba na Unguja basi kwa nini hata wanaotoka Pemba baada ya kumaliza mafunzo hayo, wizara yako ina mikakati gani kuona wale wanaomaliza mafunzo yao kutoka Pemba wakarudi katika maeneo ambayo tayari wamesajiliwa kutoka Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wizara huwa inalizingatia sana suala hilo la kuwarudisha wale ambao wako katika sehemu zao. Lakini kuna tatizo moja kubwa ambalo tunakabiliano nalo na tunaomba mashirikiano yenu Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, mara nyingi tunapomrudisha mtu au mfanyakazi ambaye kaenda kusoma tunapomuweka katika kituo ambacho ni cha karibu yake kwa mfano wale ambao wanatoka Pemba tukawarudisha katika kisiwa cha Pemba, basi mara nyingi tunapata malalamiko na maombi mengi wizarani ya kutaka kuhamishwa ili kuja Unguja kufanyakazi.

Mhe. Spika, nikwambe dhahiri kwamba sijui kuna nini lakini wafanyakazi wengi ambao wanaofanyakazi Pemba wanavutiwa zaidi kufanyakazi katika kisiwa cha Unguja. Tunatafuta ni sababu gani ambayo inasababisha hivyo. Mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi nafikiri bila ya kujitambua mnafanya nini hili mnalisaidia ingawaje baadae mnatulaumu sisi kuhusu kwamba tunawaodosha Pemba tunawaleta .....

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, utaratibu...

Mhe. Spika: Mheshimiwa kwanza mwache Mheshimiwa amalize kujibu naomba ukae. Tuendelee.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hawa wanaopangiwa katika vituo vile mara nyingi aidha huolewa wakaondoka kwenye kituo wakaja Unguja au huomba uhamisho na Waheshimiwa Wawakilishi wakawaomba wafanyakazi wanaohusika uhamisho kuwahamisha pengine ana mzee wake ana tatizo hili au

hili, hutoka visingizio mbali mbali ambavyo husababisha mfanyakazi yule kuhamishwa na kuja Pemba. Lakini wizara mara nyingi inazingatia sana kuwaweka katika sehemu zao ambazo wametoka. Ahsante Mhe. Spika..

Mhe. Spika: Mheshimiwa kuhusu utaratibu inahusiana na hili?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa naomba kidogo kwa nia njema kabisa arekebishe kauli yake Mhe. Waziri asiseme Wawakilishi hatujui tunafanya nini....

Mhe. Spika: Kuhusu kanuni kwanza nipe Mheshimiwa, Kanuni gani unatumia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 37

Mhe. Spika: Inasemaje?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa naomba ukae tuendelee.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi alieleza hapo kwamba hana uhakika hizo shutuma za madaktari kurudi Unguja waliopelekwa Pemba na kwa kuwa vile vile kuna madaktari ambao kuwa ni uhakika walipelekwa Pemba....

Mhe. Spika: Naomba utulivu Waheshimiwa, Mheshimiwa Mpaka basi. Anza mwanzo sasa kuuliza Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi alieleza hapo kwamba tuhuma zilizopo kwa madaktari kurejea Unguja au kwenda masomoni mnalifanyia kazi. Lakini kwa kuwa vile vile kuna madaktari uhakika kwamba wamekwenda kule Pemba na baadae wakenda masomoni.

(a) Je, wizara ilikuwa haijui katika kupanga kwenda kufanyakazi Hospitali ya Mkoani kwamba watu hawa tayari walishakuwa na ruhusa ya kwenda kusoma.

(b) Daktari dhamana na mtu wa ganzi walioko Pemba kwa ajili ya Hospitali ya Abdalla Mzee kuishi mbali na kituo chake cha

Abdalla Mzee Hospitali ni sahihi na lile lililokusudiwa litapatikana baada ya kwenda kuishi pale Chake Chake?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, samahani naomba arudie swali (a).

Mhe. Spika: Mheshimiwa njoo karibu na *microphone* akusikie Mheshimiwa.

Mhe. Shehe Hamad Mattar:

(a) Katika majibu yake ya msingi alieleza kwamba suala la kwamba wafanyakazi waliopelekwa Pemba wamerejea Unguja linafanyiwa kazi. Lakini kuna madaktari kwamba hao waliopelekwa Pemba wengine walirudi wakaenda masomoni. Je, wizara ilikuwa haijui wakati ilipokuwa inapanga kupeleka madaktari hawa kwamba hawa tayari wameshakuwa na ruhusa ya kwenda masomoni?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

(a) Mhe. Spika, kwa ufupi wizara ilikuwa inajua lakini kutokana na haja iliokuwa mbele yetu wakati ule hospitali ya Abdalla Mzee ilikuwa kwa njia yoyote inahitaji wafanyakazi basi tulilazimika kufanya vyovyote itakavyokuwa tuhakikishe tunapeleka wafanyakazi wa kuweza kutoa huduma kwa wananchi haraka iwezekanavyo.

Hivyo, kuna wafanyakazi lakini ni wachache sana ambao walikuwa wako wamemaliza *semester* na wanasubiri kuendelea muda ni mrefu kwa hiyo tukaamua tuwapeleke kwa vile tulikuwa na tamaa mbele ya kupata wafanyakazi wa kutosha na kuwaajiri na baadae kuwapeleka pale kuwepo kwa muda mrefu au kwa muda wote.

Kwa hiyo, hilo tulilifanya tukijua lakini ilibidi tufanye hivyo ili kuokoa wananchi wa Mkoani au wa Kisiwa cha Pemba wasiweze kukosa huduma ya afya kutokana na kukosa sisi wafanyakazi wa kuwapeleka pale.

(b) Linalohusu mfanyakazi wa gani Mhe. Mwakilishi hili naomba nikuombe kwamba liko kwenye utaratibu kweli tuna wafanyakazi wa ganzi pale wawili na kwa bahati mbaya katika makaazi yalipogaiwa wao walichelewa kuripoti kwa hiyo wakapata makaazi Chake Chake. Lakini sasa hivi kuna nyumba ambazo zinafatiliwa wakati wowote

kuanzia sasa watapatiwa nyumba katika Kijiji cha Mkoani ili kuweza kuwa karibu na Hospitali ya Mkoani. Ahsante sana.

Nam. 101

Misaada ya huduma za Kinga na Tiba Kimataifa

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:**

Kwa kuwa si chini ya wagonjwa 600 wa kifua kikuu na *HIV/AIDS* hugundulika kila mwaka kwa Unguja na Pemba hasa kwa rika la kati ya umri wa miaka 15 hadi 34, na kwa sababu Wizara ilikuwa inategemea sana ufadhili kutoka *Global Fund* kwa ajili kupambana na maradhi hayo ambapo kwa sasa misaada hiyo inaonekana kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wake.

(a) Je, Shirika la *Global Fund* bado linaendelea na ufadhili wake kama mwanzo.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaipata huduma ya Tiba na kinga kama kawaida kama ilivyokuwa chini ya ufadhili wa *Global Fund*.

(c) Je, kuna Mashirika mangapi ya Kimataifa ukiondoa *Global Fund* ambayo hutusaidia kwenye kufadhili miradi kama hii na nini mwelekeo wa Mashirika hayo kwetu kwa sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde swali lake Nam. 101 lenye kifungu (a), na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sasa bado tumekabiliwa na ongezeko la idadi ya wagonjwa wanaogunduliwa na maradhi ya Ukimwi na Kifua kikuu ambapo maambukizi yaliyogunduliwa mwaka 2015 kwa Kifua Kikuu yalikuwa ni kwa watu 855 na Ukimwi ni 1,172 na makundi yanayoathirika zaidi ni kundi la vijana. Matokeo mengine yatapatikana mapema mwaka huu mara baada ya kumalizika kwa utafiti mkubwa unaoendelea kufanywa unaoangalia hali halisi ya Ukimwi Tanzania.

Mhe. Spika, **S**erikali imekua mstari wa mbele katika kukabiliana na vita dhidi ya magonjwa haya thakili ambapo imeweka Kitengo maalum kupitia Mradi wa maendeleo wa kudumu wa Ukimwi na kwa hivi sasa tumejumuisha pamoja '*program* mbili' Kifua Kikuu na Ukimwi na kuwa na Mradi Shirikishi wa Ukimwi, Kifua kikuu na Ukoma. Hii imekuja kwa lengo la kuongeza nguvu na kuzifanya kazi hizi kwa pamoja na kwa ufanisi mzuri ikitiliwa maanani kuwa kuna uhusiano mkubwa wa maradhi haya. Mradi huu kwa muda mrefu umekua ukipata msukumo wa wafadhili mbali mbali wakiwemo '*World Health Organization*, *UNICEF*, *PEPFAR* kupitia Tanzania *Health Promotion Support* na *Global Fund*.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumtoa wasiwasi Mhe. Mwakilishi kwamba bado tunaendelea na ufadhili wa *Global Fund* (*GF*) ambapo kwa sasa tunatekeleza Mradi Mkubwa wa Miaka 3 (2015 – 2017). Ndani ya mradi huu kumepangwa Mpango Mkakati na mambo mbali mbali yanayojumuisha kinga na tiba na yanatekelezwa kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa sasa tumo katika maandalizi ya Mradi mwengine wa Miaka mingine mitatu (2018 - 2020) pia kwa UNISEF. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutoa mchango mkubwa wa fedha (*counterpart fund*) kwa Mradi huu Shirikishi wa Ukimwi, Kifua Kikuu na Ukoma kuhakikisha kazi zote za kitengo hiki zinatekelezwa kama zilivyopangwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue nafasi hii nitoe taarifa taaluma maalum niwasihi wananchi waendelee kuchukua juhudi zote za kujikinga kujilinda na magonjwa haya thakili na wajitokeze kupima afya zao mara kwa mara ili kubaini tatizo. Hivi karibuni tutakua na Maadhimisho ya siku ya Kifua kikuu duniani (24th March, 2017) ambapo hapa kwetu tutakua na makongamano pamoja na utoaji wa taaluma pia na upimaji wa afya za wananchi. Hivyo wote mnaalikwa katika shuhuli hii.

Mhe. Spika, kifua kikuu kinaambukizwa kwa njia ya hewa hivyo basi tunawaomba wananchi waepuke misongamano isiyo ya lazima na kukaa katika maeneo ya makundi yasiyo na ulazima. Wanapobaini tu dalili za kifua kikuu waripoti hospitali ili kupata ushauri na kinga. Ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri yenye muelekeo lakini nina swali dogo tu. Kwa kuwa huko nyuma serikalini kulikuwa na mpango ule wa kusaidia zile jumuia kama vile za *ZAPHA Plus* na nyengineyo kwa lengo la kusaidia mpango wa kuwakusanya wale wagonjwa waliopata maradhi haya ya kuambukiza, ambapo ilikuwa ni

rahisi kupata takwimu kwa sababu wengi walikuwa wanakutanika pale. Lakini kwa sasa inaonekana mpango ule umepungua.

Je, ni kwa sababu gani serikali imepungaza ufadhili wake kwa jumuiya kama zile za *ZAPHA plus* na nyenginezo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kweli hadi sasa bado wagonjwa wale wanakutana katika vitengo vyao na wanahudhuria katika *clinic* katika hospitali zetu. Hivyo, serikali ina nafasi nzuri ya kujua takwimu zao wanaongeza au kuongezeka kwa maambukizo mapya au kubaki kwa yale yale. Mpango ule Mheshimiwa upo mpaka sasa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mzuri ya Mhe. Waziri ninaomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa nini madaktari wa Hospitali ya Chake Chake ambao wanaoshughulikia waaguzi wa vifuo vikuu na Hospitali ya Konde wamepata maambukizo ya maradhi ya vifua vikuu pamoja na watoto wao.

Ni kiasi gani mradi huu umewasaidia madaktari hawa katika kuwatibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mimi naomba nimjibu kwamba ni mipango ya Mwenyezi Mungu. Kwa kweli hili hatuwezi kulizuia kwa sababu wale madaktari ni madaktari wamesoma wanajua jinsi ya kujikinga na wao walikuwa wanatoa elimu kwa wananchi au kwa watu wengine jinsi ya kujikinga. Sasa moja kwa moja ikatokezea wakapata wao matatizo haya, moja kwa moja tuseme tu kwamba ni mipango ya Mwenyezi Mungu.

Lakini wizara iko pamoja na wao na inajitahidi kuwapa huduma na kuwashughulikia na tunawaomba kama kuna tatizo lolote ambalo wanahisi kwamba wanahitaji matibabu zaidi basi wao wamo ndani ya wizara na wizara iko tayari kuwashughulikia zaidi na sasa hivi kuna Bima, kwa hiyo wana nafasi pana ya kuweza kupata matibabu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika,...

Mhe. Spika: Samahani Mheshimiwa Mwakilishi kuna Mhe. Waziri ana masuala ya nyongeza hapa. Naomba ukae. Mheshimiwa Waziri tafadhali.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya: (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, naomba nikushukuru naomba nimsaidie Mhe. Naibu Waziri kwa suala hili la kifua kikuu.

Mhe. Spika, ugonjwa wa kifua kikuu unasambazwa na hewa na wale wagonjwa wanaougua nje hawafanyi kazi hospitali na wanaugua. Mfanyakazi wa hopsitali anaweza akaugua husababishwa na mgonjwa au bila ya kuwa na mgonjwa kwa sababu naye anaishi kwenye jamii ya kawaida.

Mimi nimefanya kazi katika sehemu ya kifua kikuu miaka 25 na sikuugua kifua kikuu pindipo kutakuwa na mgonjwa katika eneo ambalo mtu yule anaishi kutokana na hewa kwa hiyo anaweza akapata ugonjwa wa kifua kikuu. Sasa kama kuna mmoja wao hatuwezi kusema kapata pale kwenye kituo cha afya huko nje kwa sababu naye anahudumia mgonjwa wa kifua kikuu. Kinga yake ikiwa kidogo yule anayehudumia wagonjwa wa kifua kikuu na yeye anaweza akapata ugonjwa wa kifua kikuu kwa sababu kifua kikuu kiko tunakwenda nacho sote tumeambukizwa kwa sababu hewa iko.

Sasa inachotakiwa ni kupungukiwa na kinga, sasa kama kinga imepungua yule ataugua si lazima akaambukizwa na mgonjwa ambaye anakuja anamtibu. Lakini kwa vile anakaa ndani ya nyumba na watoto wake hatuelewi mazingira gani ndani ya nyumba pengine nyumba haina hewa, kwa hiyo waliomo ndani ya nyumba wote wataambukizwa. Lakini kama mtoto naye kinga yake ndogo na yeye ataambukizwa.

Kwa hiyo, suala la kusema kwamba wagonjwa wamewaambikiza wafanyakazi hilo halina uthibitisho kisayansi. (*Makofi*)

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsnate Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri na hasa kukiri katika athari wanaopatikana vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 34 kwa masuala ya kifua kikuu pamoja HIV. Mimi nataka kuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa kuwa Mkoa wangu wa Kusini pamoja na Wilaya ya Kati tuna Vyuo Vikuu na vijana wengi ambao wanasoma pale na mikusanyiko na pia uhamiaji wa watu wengi sana. Tatizo tuliokuwa nalo ni kwamba katika njia moja ambayo watu kupata haya maswala ya kifua kikuu ni hasa maswala ya kifua kikuu ni hasa maswala ya ugonjwa wa Ukimwi na kwenye suala zima la Kinga na Tiba imetajwa kwamba njia moja ni matumizi ya upatikanaji wa kondom.

(a) Je, utahakikisheae katika Mkoa wangu na wilaya ya kati suala la kondom linapatikana katika njia iliyokuwa rasmi hasa katika maduka.

(b) Ni lini uhamasishaji utafanywa pamoja na serikali pamoja na sisi Waheshimiwa ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kupima damu

kwa hiari ili wananchi wetu pia waweze kujitambua afya zao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kuhusu suala la upatikanaji wa kondom ni kwamba mara nyinyi kondom zimo katika maduka mengi au niseme yote ya dawa. Lakini hata katika vituo vyetu vya afya katika sehemu ya mama na mtoto ziko kondom zote za kike na za kiume.

Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe nilikuwa nakushauri kwa kupitia wananchi wako kwamba watembee katika vituo hivyo, wale ambao wanakwenda kwenye kliniki ya mama na mtoto wanazikuta na huwa wanaelezwa matumizi yake, na wengine wanachukua kwa ajili ya matumizi. Hapa ndio pale ambapo tunawaomba ndugu zetu wa kiume mushiriki katika kwenda kliniki ya mama na mtoto, pamoja na mama, ile imatajwa mama na mtoto, lakini unaingia moja kwa moja na wewe baba. Utakapomsindikiza mama kwenda kwenye kituo kile cha afya kwenye klini, basi na wewe elimu ile atakayopewa pale ya kutumia njia mbali mbali za uzazi, za kujiepusha na maambukizo mbali mbali basi na wewe utazipata na utapata maamuzi utumie na wewe njia ipi.

Kwa hivyo, tunawashauri kwamba muende muwasindikize akina mama, yaani wake zetu katika vituo na watoto ili kupokea na nyinyi elimu ile na kuchagua njia ipi ya kondom kwa ufupi ya kike na ya kiume, zipo katika vituo vyetu vya afya na zinapatikana bure. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuhusu uhamasishaji wa. Samahani Mhe. Spika, arudie kidogo mjumbe.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Spika. Swali (b) lilikuwa ni nini serikali kwa kushirikiana na sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wataunda mkakati rasmi ili kuweza kuhamasisha kwenda kupima damu kwa hiyari ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu kujitambua afya zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kuhusu suala la uhamasishaji wa kupima damu kwa hiyari. Mhe. Spika, elimu hii kila siku inatolewa na tunatumia vyombo vyetu vya habari pia. Kwa hivyo, kama unataka ifanyike maalum kwa ajili ya wawakilishi, basi nitaishauri wizara ili tufanye aidha semina au kongamano au kitu chochote ili kuhakikisha waheshimiwa nanyi mnapata elimu hii. Lakini kwa kweli elimu hii inatolewa katika vyombo vyetu vya habari mara nyingi tu. Mimi nilifikiri kwamba tayari waheshimiwa mmeshakuwa miongoni mwa ambao wanachangia damu. Lakini kwa kauli yako Mhe. Simai Mohammed ni kwamba wajumbe wengi

hamjajitokeza katika jambo hili. Kwa hivyo, tunawaomba sana mjitokeze, nyinyi ni viongozi na mnapaswa kuonesha njia kwa wananchi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana kwa majibu yako Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa maswali umekwisha. Sasa naomba nitoe tangazo kwa wageni, wageni wetu wa leo ni wageni wa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye pia ni mlezi. Wageni wake wanatoka Baraza la Vijana Shehia ya Miembeni, Mhe. Naibu Spika, pia ni mlezi wa Baraza hilo la Vijana Shehia ya Miembeni. Jumla yao ni 14 na ni kama ifuatavyo, na wengi wao ndio hao ambao wamesimama hapo mbele yetu.

1.	Ismail Abass Mkubwa	Mwenyekiti.
2.	Fatma Yussuf Mkwinda	Makamu Mwenyekiti
3.	Kauthar Mwinyi Aboud	Mjumbe
4.	Asya Mwinyi Mwinshehe	Mjumbe
5.	Hamim Ali Fadhil	Mjumbe
6.	Najma Haji Haji	Mjumbe
7.	Ahmed Ali Mohammed	Mjumbe
8.	Khayrat Iddi Muki	Mjumbe
9.	Kijakazi Haji Haji	Mjumbe
10.	Faharia Soud Mgeni	Mjumbe
11.	Khadija Haroub Ali	Mjumbe
12.	Sheha Gharib Khamis	Mjumbe
13.	Lutfia Rajab Khamis	Mjumbe
14.	Said Mwinyi Aboud	Mjumbe

Karibuni sana kwenye Baraza la Wawakilishi, ili muone namna tunavyoendesha shughuli hizi za wananchi. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2016/2017

Mhe. Spika: Ahsante. Kabla sijamuita Mwenyekiti. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, ili aje aendeshe hizi shughuli Mhe. Shehe Hamad Mattar. Baada ya usomaji wa ripoti na Mwenyekiti, mpaka sasa tuna wachangiaji 9. Kuna wachangiaji ambao ililetwa kama orodha waliomba kwa pamoja, lakini nafikiri utaratibu mzuri ni kila anayetaka kuchangia alete mwenyewe binafsi ombi lake.

Waheshimiwa Wajumbe, mpaka sasa tuna wachangiaji 9 na watatanguliwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa hivyo ajiandae, ili baada ya Mwenyekiti kuwasilisha hiyo ripoti yake yeye ndio atakuwa mjumbe wa mwanzo kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, Shehe Hamad Mattar naomba uje uchukuwe nafasi.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Shehe Hamad Mattar alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, karibu.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo tarehe 27/02/2017, kusoma ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya mwaka 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ripoti zetu hizi mbili ya Wizara ya Habari, Utalii Utamaduni na Michezo na baadae tutakuwa na Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, nitaisoma moja baada ya nyengine kama ifuatavyo.

Kwa kuwa naanza na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo. Kwanza nashukuru kwa kuwa tunaingia katika sekta ya michezo, niwapongeze wana simba wote na klabu ya simba, kwa ushindi mnono walioupata hasa tukiwa katika wachezaji kumi, tuko nyuma kwa bao moja wakati huo. *(Makofi)*

Baada ya hapo, naanza kusoma ripoti yangu kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ni miongoni mwa kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016.

Majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na Wajumbe wa Kamati katika kipindi chote cha uhai wake ni kama yalivyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016. Majukumu hayo ni haya yafuatayo:-

Kamati za Kisekta zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati iliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliyotangulia.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

(iv) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia katika utekelezaji wa ahadi hizo.

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Katika utekelezaji wa majukumu hayo Kamati inatakiwa kusimamia Wizara mbili za Serikali, ambazo ni:-

1. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo; na
2. Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kamati ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu, kuanzia tarehe 29 Agosti hadi tarehe 09 Septemba, 2016 kwa muda wa wiki mbili kwa Unguja, na kuanzia tarehe 31 Oktoba hadi tarehe 11 Novemba, 2016 kwa wiki moja Unguja na Wiki moja kwa upande wa Pemba, na kumalizia na mzunguko wa tatu kwa upande wa Unguja kuanzia tarehe 16 Januari hadi 27 Februari, 2017.

WAJUMBE WA KAMATI

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari Utalii ina wajumbe tisa (9) na Makatibu wawili (2), ambao ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (SHIHATA) Mwenyekiti
2. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma Makamu Mwenyekiti

3.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
4.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Zaina Abdallah Salum	Mjumbe
6.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
8.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe
9.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
10.	Ndg. Latifa Saleh Suleiman	Katibu
11.	Ndg. Makame Salim Ali	Katibu
12.	Ndg. Amina Abeid	Mkalimani

SEHEMU YA PILI

(1) WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina jukumu la kusimamia sekta kuu nne katika nchi yetu. Sekta hizo ni za Habari, Utalii, Utamaduni na sekta ya Michezo.

Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Wizara imeundwa na Idara nne (4), Kamisheni mbili (2), Mashirika mawili (2), Vyuo viwili (2), Mabaraza matatu (3), Tume moja (1), Kampuni moja (1) na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
iii. Idara ya Habari Maelezo
iv. Idara ya Makumbusho ya Mambo ya Kale
v. Kamisheni ya Utamaduni na Michezo
vi. Ofisi Kuu Pemba
vii. Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)
viii. Shirika la Magazeti ya Serikali
ix. Chuo cha Uandishi wa Habari
x. Tume ya Utangazaji
xi. Kampuni ya Usambazaji Maudhui (ZMUX)
xii. Chuo cha Maendeleo ya Utalii
xiii. Baraza la Kiswahili
xiv. Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU)
xv. Baraza la Taifa la Michezo; na
xvi. Kamisheni ya Utalii.

MAPATO:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 2,547,268,000 (Bilioni Mbili,Mia Tano Arobaini na Saba Milioni, Laki Mbili na Sitini na Nane Elfu (Wizara 447,268,000) Mia Nne na Arobaini na Saba Milioni, Laki Mbili na Sitini na Nane Elfu na shilingi 2,000,000,000 (Bilioni Mbili)kwa upande wa Kamisheni ya Utalii. Hadi kufikia Disemba jumla ya shilingi 151,329,062 (Mia Moja na Hamsini na Moja Milioni, Laki Tatu Ishirini na Tisa Elfu na Sitini na Mbili zimekusanywa na Wizara ikiwa ni asilimia 27.65 ya makadirio na kwa upande wa Kamisheni ya Utalii wameweza kukusanya 188,749,809 (Milioni Mia Moja na Thamanini na Nane, Laki Saba na Arobaini na Tisa Elfu Mia Nane na Tisa kati ya 2,000,000,000 (Bilioni Mbili) walizokadiriwa ambazo ni sawa na asilimia 9. Hivyo makusanyo ya jumla ya Wizara pamoja Kamisheni ya Utalii yamefikia asilimia 13.

MATUMIZI:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 16,281,900,000 (Kumi na Sita Bilioni, Mia Mbili na Thamanini na Moja Milioni na Laki Tisa) kati ya hizo Tsh 9,684,400,000 (Bilioni Tisa, Mia Sita na Thamanini na Nne na Laki Nne) ni kwa kazi za kawaida na TSh 6, 597,500,000 (Bilioni Sita, Mia Tano Tisini na Saba Milioni na Laki Tano) kwa kazi za maendeleo ambapo fedha kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Tsh 1,000,000,000 (Bilioni Moja) na washirika wa maendeleo ni Tsh 5,597,500,000 (Bilioni Tano, Mia Tano na Tisini na Saba Milioni na Laki Tano).

Hadi kufikia Disemba jumla ya shilingi 5,536,368,976.46 (Bilioni Tano, Mia Tano Thalathini na Sita, laki tatu na Sitini na Nane Elfu)zimepatikana kati ya Shilingi 16,281,900,000 (Bilioni Kumi na Sita, Mia Mbili na Thamanini na Moja Milioni na Laki Tisa) zilizotengwa kwa mwaka ambayo ni sawa na asilimia 34 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatoa pongezi za dhati kwa Serikali kwa kuipatia Wizara fedha kwa asilimia karibu mia moja kwa nusu mwaka

.

Katika mwaka huu wa fedha, Wizara ilipangiwa kutekeleza programu Kuu Tano zifuatazo:

1. Programu ya Maendeleo ya Habari na Utangazaji

2. Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Utalii na Michezo
3. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii
4. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii; na
5. Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Mwenyekit, mbali ya hizo programu kuu, Wizara inazo programu ndogo saba (7) zifuatazo:-

i. Programu ya Usambazaji na upatikanaji wa Habari
ii. Programu ya Usimamizi wa vyombo vya Habari na Utangazaji
iii. Programu ya Utamaduni na Maeneo ya kihistoria
iv. Programu ya Uendelezaji Utalii na Ukuzaji wa Michezo
v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika sekta za Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
vi. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara
vii. Programu ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi kwa Pemba.

SEKTA YA HABARI:

Mhe. Mwenyekiti, Habari katika jamii na dunia ya leo ni nyenzo muhimu sana katika kuibua, kueleza, kufafanua na hata kuburudisha jamii husika. Upatikanaji wa habari zilizo sahihi na kwa wakati katika nyanja zote za jamii ikiwemo siasa, uchumi, historia na nyenginezo ni msingi thabiti wa kujenga jamii yenye uelewa wa historia yake na mipango ya baaadae kwa nchi na hata dunia kwa ujumla.

Sekta ya Habari kwa ujumla wake bado inakabiliwa na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kuhabarisha, kuelimisha na kuiburudisha jamii. Licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na watumishi waliomo kwenye sekta ya habari, lakini bado utendaji wao wa kazi umekuwa unakumbwa na vikwazo kadhaa kufanikisha majukumu yao kwa ufanisi ikiwemo mazingira magumu ya kufanyia kazi, vitendea kazi vya kisasa, mafunzo katika maeneo yao ya kazi na maslahi yasiyoendana na ukubwa wa majukumu yao kwa jamii na taifa kwa ujumla.

SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*):

Mhe. Mwenyekiti, kamati inalipongeza Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) kwa kuwa linaonekana tayari limeanza kubadilika kiutendaji, licha ya changamoto nyingi tunazokabiliana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri mambo yafuatayo yafanyiwe kazi ili Shirika liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kama kila mmoja wetu anavyotarajia.

i. Uwezeshaji wa kifedha. Kamati inaamini kwamba uendeshaji wa chombo chochote cha habari unahitaji fedha za kutosha ili kiweze kufanya kazi zake vizuri. Masuala ya vifaa, vitendea kazi na shughuli nyengine za kiutendaji zote zinahitaji fedha ili ziweze kwenda vizuri. Utaratibu wa *O/C's* kuendeshea Shirika hautaweza kulikwamua Shirika mahali lilipo. Hivyo, Kamati inashauri kwa Serikali kuangalia njia mbadala ya kuliwezesha Shirika kiudhati ili liweze kufanya majukumu yake kwa uzuri zaidi.

ii. Watendaji wachache wenye ujuzi, ubunifu, uzalendo na ari ya kufanya kazi. Uendeshaji wa Shirika kwa njia ya faida kunahitaji wataalamu katika kutekeleza majukumu yao. Kwa upande wa Shirika la *ZBC* kuna haja ya kufanywa mapitio ya watumishi waliopo pamoja na majukumu wanayoyafanya ili wale ambao wataoonekana hawana kazi za kufanya basi wafanyiwe utaratibu mwengine na Serikali.

iii. Maslahi mazuri kwa watumishi wa Shirika. Waswahili wanasema "mcheza kwao hutunzwa". Hivyo, yeyote anayefanya vizuri hutegemea kupata malipo mazuri. Na kwa kuzingatia kwamba huu ni wakati wa ushindani na soko huria la ajira, tusipoangalia kwa umakini basi Shirika na vyombo vyetu vya Habari vitaendelea kuwa ni vyuo vya mafunzo na kujengea uzoefu kwa watumishi mbali mbali na baadae kutimkia katika ofisi na vyombo vyengine vya habari vinavyolipa zaidi.

OFISI ZA ZBC DAR-ES-SALAAM:

Mhe. Mwenyekiti, Mnamo mwezi wa Septemba 2016 Kamati ilipata bahati ya kutembelea Ofisi za ZBC zilizopo Dar-es-Salaam ambazo zinajumuisha watumishi wa *ZBC TV, ZBC* Radio pamoja na Gazeti la Zanzibar Leo.

Kamati inawapongeza watumishi waliopo kwa kufanya kazi zao kwa ustadi na weledi licha ya changamoto nyingi wanazokabiliana nazo katika utendaji wa

kila siku. Aidha, Kamati hairidhishwi na hali ya kutoonekana kwa *ZBC TV* kwenye king'amuzi cha *Star Times* kwa upande wa Dar-es- Salaam, hivyo inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa changamoto hii inapatiwa ufumbuzi.

Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazowakabili watumishi wa *ZBC* waliopo Dar-es- Salaam ikiwemo idadi ndogo ya watumishi waliopo Dar-es-Salaam, kukosekana kwa habari za mikoani, changamoto ya usafiri, kukosekana/ufinyu wa posho maalumu kwa watumishi waliopo Dar-es-Salaam, kukosa mashirikiano kutoka kwa baadhi ya taasisi za Serikali ya Muungano.

Changamoto za Shirika la Utangazaji Zanzibar *(ZBC):*

Mhe. Mwenyekiti, licha ya juhudi kubwa ambazo Kamati yangu inaamini zinachukuliwa, bado Shirika la Utangazaji Zanzibar linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Ufinyu wa Bajeti katika kutekeleza majukumu yake.
ii. Ufinyu wa vitendea kazi.
iii. Maslahi duni kwa watumishi wa Shirika.
iv. Madeni kwa baadhi ya taasisi za Serikali kutolipia huduma wanazopewa na Shirika.

SEKTA YA UTALII:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inasimamia sekta ya Utalii kupitia taasisi kuu mbili ambazo ni Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Kamisheni ya Utalii.

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea maeneo mbali mbali yanayohusana na sekta ya Utalii ikiwemo mahoteli ya kitalii kama *Manta Resort* iliyopo Makangale Pemba, *Melia Hotel* Zanzibar, *Fruit & Spice Wellness Resort* Mchanga Mle na *Karafuu Beach Resort & Spa* iliyopo Michamvi.

Kamati inawapongeza wawekezaji wote ambao wamewekeza katika sekta hii ya Utalii na inawataka kuhakikisha kuwa wanalipa kodi zote na kwa wakati kwa mujibu wa sheria zilizopo ili Serikali iweze kupata fedha za kufanyia shughuli mbali mbali za kimaendeleo kwa ya wananchi. Lakini pia kamati imewaomba wawekezaji hawa kuwapatia uajiri rasmi au mikataba wafanyakazi hawa ili kuondoa matatizo yanayowakabili katika shughuli zao.

UTANGAZAJI WA SEKTA YA UTALII:

Mhe. Mwenyekiti**,** Waswahili wanasema "Biashara itangazwayo ndiyo itokayo". Ni ukweli ulio wazi kuwa kuna ulazima wa kuitangaza nchi yetu ili wageni wengi zaidi na hasa wenye hadhi ya juu waweze kuja kuitembelea Zanzibar. Tusipokubali kutoa fedha kwa ajili ya kuutangaza utalii wetu basi tujue kuwa tunajinyima wenyewe mapato ya sekta ya utalii.

KAMISHENI YA UTALII:

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamisheni ya Utalii ndiyo yenye dhamana ya moja kwa moja katika kushughulikia sekta ya Utalii nchini mwetu. Lengo la muda mrefu la kuwepo kwa Kamisheni ya Utalii ni kuifanya Zanzibar kuwa kituo bora cha utalii chenye kukidhi mahitaji ya jamii na watalii wanaoitembelea nchi yetu.

Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wote wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa kujitahidi kwao katika kutekeleza majukumu yao kwa uzuri. Hata hivyo, wakati wa ziara ya Kamati katika baadhi ya mahoteli na hasa hoteli/mkahawa wa Peter Obama uliopo Kiwengwa Kamati haijaridhishwa na jinsi mwekezaji huyu anavyofanya shughuli zake kwanza kwa jamii inayomzunguka hasa waislamu kwa kupiga muziki kupita kiasi na kushindwa kutekeleza hata ibada yao wakati unapowadia.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna wageni ambao wanalala katika hoteli/mkahawa huu ambao hautambuliwi/ hauna kibali cha kulaza wageni kupitia Kamisheni ya Utalii. Huu ni mfano mmoja tu kati ya sehemu nyingi ambazo ni kero kwa wananchi kwa uwekezaji wa kupiga miziki kupita kiasi na hata kufanya biashara ya kulaza wageni bila ya kuwa na kibali kutoka Kamisheni ya Utalii jambo ambalo linaikosesha Serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaitaka Kamisheni ya Utalii kuhakikisha hoteli zote (kubwa na ndogo) zinasajiliwa na kutambuliwa kwa mujibu wa sheria zilizopo. Aidha, Kamati inatoa onyo kali kwa baadhi ya watendaji wa Kamisheni ya Utalii ikiwa Makao Makuu au katika ngazi ya Mkoa na Wilaya kuacha tabia ya kutumia nafasi walizopewa vibaya kwa kutoa vibali kwa watu wasiostahiki. Tabia hii ya kuchukua rushwa kutoka kwa wenye mahoteli ili kuwalegezea katika masharti inapaswa kuachwa mara moja, na Kamati haitosita kuchukua hatua zilizo katika mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Kamati inaendelea kusisitiza kuwa kuendelea kufungiwa kwa mwekezaji Peter Obama wa Kiwengwa na wawekezaji wote wanaofanana na yeye hadi pale masharti yote yanayopaswa kuzingatiwa yatakapotekelezwa.

UTALII WA NDANI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa bado nchi yetu haijafanikiwa katika kushajiisha utalii wa ndani kwa wananchi wetu. Juhudi maalumu zinahitaji kuchukuliwa ili kwanza kuwaelimisha wananchi wetu juu ya maeneo muhimu ya utalii na urithi uliomo nchini mwetu lakini pia faida ya utalii wa ndani kwa nchi yetu.

Aidha, Serikali moja kwa moja au kwa kushirkiana na watu binafsi kuhakikisha kuwa maeneo mengi zaidi ya kiutalii au maeneo ya wazi ya kijamii kama vile Forodhani yanakuwepo kwa kuanzia japo kwa kila Wilaya eneo moja. Hii itasaidia kukuza dhana ya matembezi kwa wananchi lakini hata kwa wageni pia.

MAPATO KWENYE SEKTA YA UTALII:

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuwa idadi ya wageni imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka lakini bado Kamati ina wasiwasi kwanza na kodi halisi zinazopaswa kukusanywa kwenye sekta ya utalii, pili utaratibu wa ukusanyaji wa mapato na tatu uhifadhi wa mapato hayo na uwasilishwaji wake Serikalini.

SEKTA YA UTAMADUNI:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo moja ya majukumu yake ya msingi ni kuhakikisha kuwa utamaduni wa nchi yetu unahifadhiwa na kulindwa kwa maslahi ya kizazi cha sasa na cha baadae. Katika kufanikisha hilo zipo taasisi mbali mbali kisheria ambazo zina wajibu wa kuyashughulikia mambo ya mila, silka na utamaduni wetu. Taasisi hizo ni kama zifuatazo:-

BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI:

Kamati ilitembelea Ofisi za Baraza Mwanakwerekwe Zanzibar na kubadishana mawazo juu ya suala zima la Sanaa, jinsi ya uhakiki wa filamu unavyofanyika na njia wanazotumia kuhakikisha kuwa utamaduni wetu unahifadhiwa.

Changamoto kubwa ambayo Kamati wamebaini baada ya kikao hicho ni kuwa kushuka kwa malezi na kuiga kwa mifumo ya maisha ya wenzetu ndiyo sababu kuu ya kushuka kwa mila zetu na tamaduni zetu.

MATUMAINI YETU:

Kamati inachukua nafasi hii adhimu kuitaka jamii kuacha kufuata tamaduni za watu wa nje badala yake tukamatane na tamaduni zetu za asili katika malezi ya watoto wetu ili tuweze kuwa na jamii yenye heshima na maadili kama ilivyokuwa siku za nyuma.

IDARA YA MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ina jukumu la kuyatambua, kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo Zanzibar. Maeneo hayo yanajumuisha majengo kama Beit- Al- Ajaib, Kasri ya Mfalme, Makumbusho mbali mbali, mapango, Visima na kadhalika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii iliyatembelea baadhi ya majengo hayo ikiwemo Kwa Nkama Ndume Pujini, Pemba, Kasri la Mfalme Forodhani, *Peace Memorial* Mnazi Mmoja pamoja na Zanzibar *Natural History Museum* Mnazi Mmoja.

Baada ya ziara hizo Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

i. Kuchakaa kwa baadhi ya maeneo hayo. Kamati ilipofika Mkama Ndume ilishtushwa na hali ya pale kwa athari zote za kuwepo majengo zamani zimekuwa zimeondoka kwa kasi. Nyumba yenyewe haipo, kisima cha wivu pia hakipo tena, mto ambao ulikuwa ukiingiza maji pia nao unatoweka. Kamati inashauri Serikali ifanye utaratibu maalumu au hata ishirikiane na sekta binafsi kupitia miradi ya *PPP* ili suala la Nkama Ndume lishughulikiwe kwa haraka. Kuachwa kupotea kwa majengo yale ni kupoteza kwa historia yetu. Na Nkama Ndume ni jengo pekee la mtawala wa asili *(native ruler)* kwa upande wa Pemba.

ii. Kuvuja kwa majengo yaliyopo. Kamati haikuridhishwa na hali ya jengo la Kasri ya Mfalme kuwa linavujiwa na hali yake kuwa mbaya. Kibaya zaidi ni kuwa wageni bado wanatembelea jumba lile na kuona hali ile huwa wanarudi nyuma kwa kuhofia usalama wao.

iii. Bajeti finyu katika kutekeleza majukumu ya Idara. Majengo ni mengi yanayohitaji kushughulikiwa lakini kikwazo ni fedha za kuyashughulikia na utaratibu wa fedha zenyewe pia kuingia kwa awamu. Licha ya fedha kuwa ni kidogo na uingaiji wake kuwa si wa mara moja, Kamati inashauri majengo yaliyo kwenye hatari zaidi na yanayoiingizia Serikali mapato ndiyo yapewe kipaumbele.

iv. Utaratibu usio mzuri wa kukusanya mapato. Kamati hairidhishwi na mfumo wa risiti sababu hauna uhakika juu ya wageni waliotembelea maeneo husika. Kamati inashauri njia za kisasa zitumike katika kukusanya mapato sio kwenye maeneo ya utalii tu bali katika maeneo yote ambayo yanatoa huduma kwa jamii ili kodi halisi ziweze kukusanywa na kutoingia mifukoni mwa watu binafsi.

v. Elimu zaidi inahitaji kutolewa kwa wananchi ili waweze kuyaelewa maeneo muhimu ya historia ya nchi yetu. Kamati imependekeza kwa *ZBC* kuanzisha kipindi maalumu cha *HAZINA YETU* kujaribu kuionesha jamii yetu na nje ya Zanzibar namna gani nchi yetu ilivyobarikiwa kwa kuwa na mambo mbali mbali ambayo hayapatikani isipokuwa Zanzibar.

Aidha, kupitia vipindi hivyo, Kamati inaamini kuwa itakuwa ni sehemu moja ya kushajiisha Utalii wa Ndani kwa wananchi wetu.

SEKTA YA MICHEZO:

Mhe. Mwenyekiti, Michezo ni moja ya njia muhimu ya kuimarisha afya ya mtu na jamii kwa ujumla. Katika ulimwengu wa leo michezo imekuwa ni ajira na moja ya njia kubwa za kukuza uchumi kwa nchi mbali mbali duniani.

Mpira wa miguu kwa Zanzibar na duniani kwa ujumla ni mchezo wenye mashabiki wengi na unaoingiza fedha nyingi duniani. Ligi mbali mbali maarufu kama Ligi Kuu ya Uingereza (*The Barclays Premier League)*, Ligi Kuu ya Ujerumani (*Bundesliga),* Ligi Kuu ya Hispania (*LaLiga)* na nyenginezo nyingi zimekuwa vivutio vikubwa duniani kwa kuwa na mashabiki wengi, hali hii imechangia wachezaji wa ligi hizo kulipwa fedha nyingi na nchi hizo kufaidika kupitia kodi za mamilioni zinazokatwa kwenye mishahara na mapato yatokanayo na mchezo wa mpira wa miguu.

Kwetu Zanzibar hali ni tofauti, vilabu vinahangaika kupata ufadhili na hata wapenzi viwanjani wamekuwa ni wachache kutokana na wananchi wengi

kutovutiwa sana na mchezo huu na viwango vya uchezaji wa wachezaji wetu. Ule msisimko na hamasa iliyokuwepo zamani sasa imetoweka.

Kamati inaishauri Serikali kuanzisha programu maalumu za kufufua vipaji vya vijana wetu kupitia sherehe za mapinduzi, elimu bila ya malipo, sherehe za Muungano na kadhalika kulingana na mpango kazi utakaopangwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Wizara ya Habari kama Wizara inayosimamia michezo na vyama vyenyewe vya michezo husika katika ngazi za Wilaya, Mikoa na hadi Taifa.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO:

Mhe. Mwenyekiti**,** Baraza la Taifa la Michezo ndiyo mlezi wa vyama vyote vya michezo nchini. Jukumu kubwa la Baraza la Taifa la Michezo ni kuhakikisha kuwa vyama vya michezo vinafanya shughuli zao za kuendeleza Michezo kwa mujibu wa katiba sheria zinazoongoza michezo husika.

Changamoto za Baraza la Taifa la Michezo:

i. Ufinyu wa Bajeti. Kwa kuwa Baraza lina jukumu ya kusimamia vyama vyote vya Michezo, hivyo ni wazi kuwa linahitaji fedha nyingi katika kufanikisha majukumu yake na majukumu ya vyama vyengine vya michezo. Kwa sababu hali ya fedha za michezo ni kidogo na hazikidhi mahitaji ya vilabu mbali mbali vinavyoshiriki michezo ndani na nje ya nchi.

ii. Migogoro kwenye vyama vya Michezo. Kwa kuwa Baraza ndiyo mlezi wa vyama vyote vya Michezo, na kwa kuwa inapotokezea migogoro inabidi mlezi awaite wahusika ili aweze kusaidia kutatua baadhi ya changamoto zao ikiwemo masuala ya usuluhishi, bado jambo hili limekuwa ni kikwazo na ni moja ya changamoto kubwa wanayokabiliana nayo *BTMZ.*

UJENZI WA VIWANJA VYA MICHEZO KWA KILA WILAYA:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa azma yake ya kujenga viwanja vya Michezo kwa kila Wilaya ifikapo mwaka 2020. Hata hivyo, Kamati bado ina wasi wasi na kasi ya utekelezaji wa ahadi hii ya mheshimiwa Rais hasa tukizingatia kwamba hivi sasa tupo mwaka 2017 na muda uliobaki sio mrefu sana kiasi hicho.

Kamati inashauri kwa watendaji kuhakikisha kuwa agizo na ahadi hii ya Mhe. Rais inatekelezwa kwa wakati na kwa viwango vinavyokubalika. Aidha,

Kamati inapenda kutoa wito kwa watendaji wote wilayani kupitia kwa Wakuu wa Wilaya kutoa mashirikiano kwa Baraza la Taifa la Michezo ikiwa ni pamoja na kutafuta maeneo muafaka na kuwasiliana na BTMZ kabla ya kuyaweka sawa ili fedha tu zitakapopatikana kazi ya ujenzi iweze kuanza mara moja.

MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA HABARI, UTALII, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inatoa Maagizo yafuatayo kwa Wizara ya Habari:-

1. Shirila la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) kuhakikisha kuwa linakuwa na utaratibu maalumu na unaoeleweka kwa waunganishaji wa taarifa za habari (*Video Editors*) kuhusisha habari za kutoka Pemba na Unguja ili kutatua changamoto iliyopo ya kutoonekana kwa baadhi ya wakati habari (*news*) kutoka Kisiwa cha Pemba.

2. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kufuatilia kwa ukaribu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali suala la *AGAPE* na hatma yake kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

3. Wizara ya Habari kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuangalia namna gani Serikali itaweza kuwapa kifuta jasho watumishi wa *Z-MUX* waliofanya kazi ziada kipindi ambacho *AGAPE* waliondoka na wao kulazimika kumalizia kazi zote zilizoachwa.

4. Wizara kwa mwaka ujao wa fedha kuongeza fungu la bajeti kwa Kamisheni ya Utalii kwenye Programu ya Uhamasishaji na Utangazaji wa Utalii ili wageni wengi zaidi na wa kiwango cha juu waweze kuja kuitembelea nchi yetu na kuipatia Serikali mapato yanayotokana na sekta ya Utalii.

5. Wizara ya Habari kuhakikisha kuwa Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ) linatengewa fedha maalumu kwa ajili ya kuvisaidia vyama vyengine vya Michezo viliopo Zanzibar hasa pale inapotokea ushiriki wa kwenye mashindano hasa nje ya nchi.

6. Wizara kubuni njia muafaka na nzuri zaidi katika ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo ya kihistoria ili kuhakikisha kuwa yanayokusanywa ndiyo mapato halisi.

7. Wizara kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na masuala ya Utumishi wa Umma kufanya mapitio na maboresho ya maslahi (maposho) kwa watumishi wa ZBC waliopo Dar-es- Salaam na watumishi wengine wote wa SMZ walio nje ya Zanzibar.

8. Wizara kuhakikisha kuwa Studio za ZBC Pemba zinafanyiwa kazi ipasavyo kwa kuwepo watumishi wanaotumia vifaa vile pamoja na vipindi mbali mbali viwe vinafanywa Pemba. Hii itasaidia kuwapa ujuzi watumishi waliopo lakini na itawasaidia katika kujenga uwezo wao.

9. Wizara kuhakikisha kuwa majengo yote ya asili ikiwemo ya Nkama Ndume na mengineyo wakati yanapojengwa au kukarabatiwa usipotezwe uasili wake kwani ile ndo historia yenyewe.

10. Kamisheni ya Utalii kuendelea kumfungia Peter Obama wa Kiwengwa pamoja na wawekezaji wote wenye vitendo vinavyofanana na Peter Obama vya kuwasumbua wananchi kwenye maeneo yao hadi pale atakapokidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

11. Kamisheni ya Utalii kuanzisha *data base* itakayosaidia kuelewa hoteli zote pamoja na nyumba zinazolaza wageni Zanzibar ili kodi stahiki ziweze kukusanywa. *Data base* hiyo iwe na taarifa zote za hoteli ikiwemo idadi ya vyumba na kadhalika.

SEHEMU YA TATU

Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii imeundwa na Idara zifuatazo:

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
3. Idara ya Ajira
4. Idara ya Usalama na Afya Kazini
5. Idara ya Maendeleo ya Ushirika
6. Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii
7. Idara ya Maendeleo ya Vijana
8. Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti kabla sijaisoma taarifa hii naomba niseme yafuatayo. Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake ilikutana na masuala yafuatayo ambayo

yanahusika na wizara hii, suala la kesi ya mtoto Ibrahim. Ili kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi zaidi baina ya mihimili mitatu, Mahakama, Serikali na Baraza la Wawakilishi, Kanuni ya 59(4) inaeleza kwamba ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo linangojea uamuzi wa Mahakama.

Hivyo kwa mujibu wa Kanuni hii Kamati hii isingepasa kulingumzia suala la mtoto Ibrahim Abdalla ndani ya taarifa hii. Hata hivyo Kamati imeamua kwa makusudi kulizungumza kwa sababu zifuatazo.

1) Kuhakikisha kwamba haki ya maslahi ya mtoto Ibrahim yanalindwa na kupatikana
2) Ili kuboresha Mahakama kufanya kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, naomba usite kidogo kama ulivyozungumza kwa mujibu wa Kanuni hii, jambo hili lipo Mahakamani isingepaswa kuzungumzwa ili lisije likaleta mjadala katika Baraza, kwa hivyo hoja hii naomba usiilete hapa. Kwa sababu tayari itakuwa tumeivunja na tutaendelea kuivunja.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Haya nafikiri Mheshimiwa kauli yangu inatosha lililokuwepo Mahakamani liachwe kama kawaida.

Utaratibu

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti nimesimama hapa kwa kanuni ya 63, tunaamini kwamba kitu chochote ambacho kinaingia ndani ya *chamber* hii kinakuwa kimepitia Afisi ya Spika. Sasa tunashangaa utaratibu unakiukwa kwamba unakuja kumzuia Mwenyekiti wa Kamati kuzungumza jambo hapa wakati taarifa imepita kwa Spika. Mhe. Mwenyekiti, naomba utuongoze vizuri ili twende vizuri katika kuongoza hili Baraza.

Mhe. Mwanasheria: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama ambavyo umeeleza na kama ambavyo Mwenyekiti wa Kamati mwenyewe ameeleza ndani ya ripoti yake kwamba Kanuni ya 59(4) inazuia Kamati kuzungumzia jambo ambalo lipo mbele ya Mahakama na Mwenyekiti hilo amelitaja nadhani ilikuwa itoshe kwa kamati kuona jambo hili kama ambavyo amesema limezuiwa na Kamati kulizungumza.

Utaratibu ulivyo na ambao utaratibu unatuongoza humu ndani sote ni Kanuni, lakini Kanuni hizi hizi ikidoms pia zinatoa mamlaka ya Kanuni hizi hizi kutengwa kando na tunafanya mara zote. Kanuni hizi hizi pia huwa tunatoa hoja ya kutenga kando. Lakini Mwenyekiti kalizungumzia jambo ambalo limekatazwa bila ya ku-*move* hoja ya Baraza kutenga kando hiyo kanuni yenyewe. Sasa kanuni ilivyo sasa hivi inakataza kwa sababu Kanuni haikutengwa kando kuzuia jambo hili au kuruhusu jambo hili lizungumzwe.

Sasa hii ndio ufafanuzi ambao ninauutoa kama ilivyo sasa hivi hakuna hoja iliyotolewa ama na Mwenyekiti ya kuomba Baraza kutenga kando Kanuni hii ili jambo hili lizungumzwe. Sasa pamoja na kwamba Mwenyekiti amelieleza lakini ameeleza kwamba akijua kama kanuni hiyo hiyo inamkataza kulizungumza jambo hilo. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanasheria kwa maelekezo yako nadhani tumeshamsikia Mhe. Mwanasheria alivyoeleza. Kama ingelikuwa Mwenyekiti tayari alitaka kuizungumza hoja hii angelitengua Kanuni, lakini kwa sababu hakutengua lazima tusimamie kanuni inavyoeleza.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 34 wakati wowote Mjumbe anaweza kusimama akaeleza kitu nakwenda kwenye Kanuni ya 147 ambayo inasema kwa idhini ya Baraza yoyote kati ya Kanuni hizi zinaweza kutengwa kando kwa madhumuni ama mahususi ama mjumbe yoyote kutoa hoja. Ningeomba tuweke Kanuni kando ili hili suala tulizungumze. Kwa sababu limo katika ripoti hii na nafikiri walipewa na Serikali wakaipitia. Sioni maana kwamba leo inakuja huku ndio tunaambiwa tusizungumze. Tukichukulia kwamba tumeona baadhi ya mambo mengi sana humu hudharauliwa baadhi ya Kamati za Baraza la Wawakilishi, kudharauliwa amri ya Mufti, kudharauliwa hata kauli ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye yeye ni Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali si hiyo tu hata Mkuu wa Mkoa.

Sasa vile vile utaona kwamba wizara yenyewe husika inayosheria Nam. 6 ya 2011 kumlinda mtoto, vile vile imekukwa. Ningeomba sana tuweke Kanuni kando tuwaulize Wajumbe, tutowe hoja ili tuangalie suala hili. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwanasheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani baada ya kumzindua Mhe. Abdalla Diwani ndiyo kasimama kuomba kutenga kando, lakini hili jambo limeshazungumzwa kabla hiyo Kanuni yenyewe haikutengwa kando. Sasa haiwezekani Mheshimiwa kuzungumza mambo kinyume na utaratibu. Utaratibu ni huo kama tayari Kamati yenyewe imeshavunja Kanuni ya

kulizungumza jambo hili la kwanza. Lakini Mwenyekiti, aliposimama kaisoma hiyo kanuni yenyewe. Ilikuwa busara yeye aombe kwamba sasa itengwe kando hiyo Kanuni ili sasa Wajumbe wakubali ama kukataa kutengwa kando kwa Kanuni hiyo.

Lakini kanuni tatu Mhe. Mwenyekiti, zinazungumzia jambo hili, ukisoma Kanuni ya 59, 37,108, Kanuni tatu zinakataza jambo ambalo lipo mbele ya Mahakama kulizungumza ndani ya Baraza. Kwa hivyo jambo hili pamoja na *sentiment* zote ambazo Waheshimiwa Wajumbe wanazi hata sisi tunazo tunazijua lakini ndio kanuni zinavyotuongoza. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanasheria kwa msaada wa maelekezo yako ni mazuri, Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyojua kawaida kwanza tunatengua kanuni baadae ndio tunafanya jambo lenyewe. Naomba utulivu, tunatengua Kanuni mwanzo sio tunaendelea na mjadala halafu baadae ndio tunaamua. Naomba tuelewe kwamba hili jambo tumeanza kulikosea utaratibu, kwa vile utaratibu tumeukosea tukubali na ndio hiyo hiyo Kanuni ambayo tayari inatuongoza. Naomba utulivu Kanuni tumeanza kuivunja kwa pamoja kwa hivyo tukubali kwamba hili tumelikosea.

Utaratibu

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 47 cha Kanuni kinachozungumza shughuli za Kawaida za Baraza. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alikuwa anasoma ripoti yake na hajamaliza na hii imo kwenye *Order Paper* , yeye hicho kifungu alichosema kwamba ripoti ipo Mahakamani, suala liko Mahkamani haliruhusiwi kuzungumzwa anasoma kwenye ripoti yake hajamaliza hiyo ripoti. Kwa hivyo *Order Paper* yetu ya leo imemruhusu kuwasilisha ripoti yake. Ninachoshauri kwa mujibu wa *Order Paper* yako ya leo Mhe. Mwenyekiti, tumruhusu Mwenyekiti aendelee kusoma ripoti yake amalize halafu yatakuja tena hayo masuala mengine. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwinyihaji Makame, maelezo yako ya mwisho sijakupata nini umekusudia yarudie.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Naomba nirudie tena. Nasemaje kwa mujibu wa kifungu cha 47 naomba nikinukuu kinazungumza shughuli za kawaida za Baraza.

"Shughuli za kawaida za Baraza zitatekelezwa kwa njia ya hoja na maagizo mengine yatakayokuwa yamewekwa katika orodha ya shughuli"

Sasa shughuli ya leo ni kuwasilisha Mwenyekiti wa Kamati ripoti yake na anaendelea kuwasilisha ripoti, wala hajamaliza hakuna mjadala ripoti hii ndiyo ripoti yake. Sasa sio sahihi Mhe. Mwenyekiti, kumzuia au unaondoa hoja ya leo kwenye *order paper. (Makofi)*

Ombi langu Mhe. Mwenyekiti, ni busara kiti chako uchukue kumruhusu Mwenyekiti wa Kamati aendelee kusoma ripoti yake amalize. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nimezisikia hoja zenu, lakini kama Mwenyekiti wa Kamati ataendelea kuitoa tayari tutaruhusu kuja kuchangia hoja ambayo iko Mahakamani. Hii ndiyo hijo kama ataendelea kuizungumza hapa tayari tutaruhusu mjadala ndani yake na jambo lipo Mahakamani na jambo lipo Mahakamani, Kanuni inatukataza hilo kwa hivyo tukubaliane hii hoja kama kuna namna nyengine iweze kuletwa kwa namna nyengine. Kama tutaendelea hapo tutakuwa tunaruhusu kwamba wakati wa mjadala italetwa na jambo hili liko Mahkamani.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe.Mwenyekiti, nakuomba tena hii ni hoja ya Mwenyekiti, imo kwenye *Order Paper* yeye anaendelea kutoa ripoti yake mwisho atoe hoja. Sasa kuna tatizo gani katika ripoti yake, au unaondoa leo kwenye *Order Paper* hii hoja yake unaifuta au mwambie aiondoe hoja ya leo twende zetu tukalale tukafanye mengine. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwanasheria nisaidie ufafanuzi wa hili.

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mjomba anaonewa.

Mhe. Mwanasheria: Mhe. Mwenyekiti, hoja inayowasilishwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ina kurasa 29, kinachozungumzwa hapa ni sehemu ya taarifa hiyo ndiyo tunachozungumza hapa, hatuzungumzi kukatazwa kujadiliwa kwa taarifa nzima kinachozungumzwa hapa ni sehemu ya taarifa hiyo ambayo yeye mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati alishaeleza kwenye ripoti yake kama jambo hili kwa mujibu wa kanuni halikutakiwa kuzungumzwa hilo ndio mimi ninalosema. Kama Kamati yenyewe kwenye ripoti yake imeshasema hilo. Sasa hayo mengine yote hakuna mtu aliyetoa hoja kwa kusema kwamba yasizungumzwe. Lakini sehemu ambayo imelizungumza jambo hilo mimi nadhani busara tu itumike kama wao wenyewe kamati wameliona hili na wakasema kama jambo hili kwa mujibu wa Kanuni halitakiwi tulizungumze

ndivyo walivyosema wao wenyewe Mhe. Mwenyekiti, wala sikusema mimi hayo. Ninakushukuru.

Utaratibu

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 65, kufunga mjadala "endapo bado kuna wajumbe wanapenda kuzungumza katika jambo lililopo katika mjadala utaratibu utakaotumika kufunga mjadala ni kutolewa hoja itakayoamuliwa na walio wengi". (*Makofi*)

Sasa suala hili mimi naomba kutoa hoja kwa sababu hili suala alikuwa anatoa maelezo tu halizungumzii kwenye kamati yake na Mjomba mnamuonea. Naomba Mhe. Mwenyekiti, kutoa hoja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuisaidia serikali kidogo kwa ruhusa yako. Kesi inayoendelea Mahakamani haihusu Wizara wala sio *part* katika hili, wala hahusiki na hili, wacha mjadala uendelee, Wizara siyo iliyoshtakiwa wala haihusu Wizara hii kesi mimi ninayo hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekusikia kaa kitako. Waheshimiwa Wajumbe jambo hili tumeshalizungumza sana vifungu mbali mbali tushavitumia, Kanuni tushazipitia zote kila moja kwa namna yake na kwa mujibu wa Kanuni nilivyoiona hivyo hapa na maelezo ya Mhe. Mwinyihaji Makame naamua kwamba Mwenyekiti aendelee. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleima Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mwenyekiti nakupongenza kwa dhati kabisa pamoja na wenzangu wote kwanza nimetanguliza mwanzo kusoma kifungu kile tunalolizungumza hili tuna mihimili mitatu lakini haki yangu ya msingi niendelee kutoa ripoti ya kamati yangu mpaka nimalize. Kwa hivyo, yale mengine nimewaomba wajumbe mambo ya mahkama huko huko wao watajua vya kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea na Idara za Wizara hii:

9. Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
10. Kamisheni ya Kazi; na
11. Ofisi Kuu, Pemba.

Vile vile Wizara hii inazo Taasisi zifuatazo:

1. Idara ya Mikopo (Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi); na
2. Baraza la Vijana.

BAJETI YA WIZARA:

Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na watoto, ni Wizara inayotumia fungu namba (Vote) 01, ambapo kwa mwaka 2016/2017, ilitengewa bajeti ifuatayo:

MAKUSANYO:

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 487,400,000, (Mia Nne Thamanini na Saba Milioni na Laki Nne) ambazo hadi kufikia Disemba jumla ya shilingi 275,570,567 (Milioni Mia Mbili na Sabini na Tano, Laki Tano, Sabini Elfu na Mia Tano na Sitini na Saba) zimekusanywa, ambazo ni zaidi ya asilimia 50.

MATUMIZI:

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 12,104,460,000 (Kumi na Mbili Bilioni, Mia Moja na Nne Milioni, Laki Nne na Sitini Elfu) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, ambapo hadi kufikia Disemba jumla ya shilingi 2,928,112,540 (Bilioni Mbili, Mia Tisa na Ishirini na Nane Milioni, laki Moja Kumi na Mbili elfu mia tano na Arobaini) zimepatikana, kwa ajili ya utekelezaji wa Programu za Wizara. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara ilipangiwa kutekeleza programu kuu zifuatazo:

1. Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
2. Programu Kuu ya Kukuza Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake.
3. Programu Kuu ya Kuimarisha Huduma za Ustawi.
4. Programu Kuu ya Uongozi na Mipango ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.
5. Programu Kuu ya Kuratibu Uzalishaji, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria.

1. **Utekelezaji wa majukumu ya Jumla ya Kamati**: Kamati kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ilifanya kazi mbali mbali za kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Kibajeti, katika sekta

zote zinazohusika katika Wizara hii, yafuatayo ni maelezo ya ufuatiliaji huo kwa kila sekta:

I. Sekta ya Kazi:

Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu inayosimamia na Wizara hii, katika utekelezaji wa kimajukumu ya sekta hii, Idara ya Ajira na Kamisheni ya Kazi, Idara ya Usalama na Afya Kazini, zinahusika moja kwa moja na sekta hii.

Katika kufuatilia Kamati iligundua kuwepo kwa changamoto zifuatazo:

i. Changamoto inayohusiana na Mikataba ya Ajira katika sekta binafsi. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mahoteli mbali mbali yaliyopo Kaskazini na Kusini Unguja na kuweza kuzungumza na Wafanyakazi wa Hoteli hizo. Katika ziara hizo kamati iligundua kwamba kuna idadi kubwa ya Wafanyakazi wa mahoteli ambao wanafanya kazi bila ya kuwa na mikataba ya ajira.

ii. Changamoto ya Mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

iii. Changamoto inayohusiana na kukosekana kwa bima za afya kazini baadhi ya wafanyakazi katika sekta ya umma na sekta binafsi. Hali hii inapelekea waajiriwa kushindwa kumudu gharama za matibabu wakati wanapopatwa na matatizo ya kiafya kazini.

II. Sekta ya Uwezeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta hii ina umuhimu wa kipekee katika kuhakikisha kwamba Wananchi wanawezeshwa katika kujikwamua na hali ya umaskini. Uwezeshaji unaofanyika ni kwa kupitia njia mbali mbali ambazo Serikali kupitia Wizara hii imezianzisha kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo. Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Idara ya Maendeleo ya Ushirika; na Idara ya Mikopo (Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi); ndizo zinazohusika kwa ukaribu zaidi katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa kwa ufanisi.

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu hayo imegundua yafuatayo:

i. Pensheni ya Wazee: Suala la kuwapatia wazee waliotimia umri wa miaka 70, pensheni ya shilingi (elfu ishirini) 20,000 kwa mwezi ni suala la kupongezwa. Katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli hii, kamati imegundua kwamba utaratibu huu ulianzishwa tarehe 15 Aprili, 2016, ambapo hadi kufikia mwezi wa Novemba, 2016, jumla ya shilingi 2,470,140,000 (Bilioni Mbili, Mia Nne na Sabini Milioni, Laki Moja na arobaini elfu) zimepatikana. Hata hivyo Kamati imebaini kwamba, suala hili limegubikwa na utata mkubwa, ambapo bado kuna changamoto ya kujua idadi halisi ya wazee waliosajiliwa. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa hesabu sahihi zinazoonesha fedha zilizotumika,

wazee waliopungua kutokana na vifo na idadi ya wazee walioongezeka kwa kila mwezi. Kamati iligundua tatizo hilo baada ya kutaka ufafanuzi wa kina katika matumizi ya fedha hizo, lakini kwa bahati mbaya majibu yalikuwa yenye kukanganya.

ii. **Suala la Mikopo**: Katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli ya utoaji wa mikopo, Kamati imegundua kwamba, Wizara inafanya jitihada katika kutoa mikopo kwa wajasiriamali, lakini kuna tatizo kubwa katika urudishwaji wa mikopo hiyo. Hii inatokana na kukosa utaratibu mzuri wa kuwa na kumbukumbu za kutosha kuhusiana na taarifa za wakopeshwaji.

iii. **Vyama vya Ushirika:** Kamati imepata fursa ya kutembelea vyama mbali mbali vya ushirika ili kuona ni jinsi gani wananchi wanajikita katika kufanya shughuli mbali mbali za kujiletea maendeleo. Changamoto iliyopo ni kwamba, ukosefu wa masoko kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa na vikundi hivyo bado ni tatizo.

MAAGIZO YA KAMATI:

a. Kamati inaiagiza Wizara, kuhakikisha fedha zinazotumika kwa ajili ya kulipa pensheni jamii kwa Wazee zinawekewa kumbukumbu sahihi, zenye kuonesha matumizi halisi, ikiwemo idadi ya wazee waliosajiliwa, waliolipwa, na ambao wamefariki. Utaratibu huu uwe unafanyika kwa kila mwezi.

b. Kamati imepata taarifa kwamba kuna ukaguzi unafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Pensheni jamii. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuharakisha ukaguzi huo, na Ripoti yake iletwe ndani ya Baraza la Wawakilishi. Vile vile, endapo itabainika kwamba kuna watu wamehusika katika kufanya ubadhirifu wa fedha hizi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

c. Kamati inaiagiza Wizara kuandaa *data base* ambayo itakuwa na orodha halisi ya wahusika wanaopatiwa mikopo, sehemu wanazofanyia kazi, maeneo wanayoishi, taarifa za malipo ya mikopo kwa kila mwezi, n.k. *data base* hii itaiwezesha kutumika katika kuwafuatilia wadaiwa wakati wa kurejesha mikopo, pia kujua biashara inayofanyika baada ya kupatiwa mkopo, lakini pia kuweza kujua hali ya urejeshaji mikopo. Ambapo hii itasaidia Wizara kuwajua wadaiwa sugu na kuweza kuwaepuka wanapotaka kupatiwa mikopo kwa mara nyengine.

d. Kamati inaitaka Wizara kutoa mafunzo kwa wanaotaka kupewa mikopo kabla ya kutoa mikopo hiyo, ili kuwapa muongozo sahihi wa jinsi ya kutumia fedha za mkopo kwa lengo la kupata faida na kuweza kurejesha mkopo.

III. Sekta ya Vijana

Wizara hii pia imepewa jukumu la kuhakikisha kwamba Vijana ambao ndio kundi lenye idadi kubwa ya watu katika nchi yetu, linasimamiwa ipasavyo katika kuhakikisha linafikia malengo yao. Serikali katika kusimamia suala la vijana imeanzisha utaratibu mahususi wa kuwaletea maendeleo katika njia ya kuwashirikisha katika shughuli mbali mbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika usimamizi wa sekta hii, Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana vyote kwa pamoja vinahusika kwa karibu zaidi.

Kamati katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika muelekeo wa kundi hili la Vijana, ilijikita katika mambo mengi yafuatayo:

i. Ajira kwa Vijana: Suala la ajira kwa vijana limeonekana kuwa ni changamoto kubwa inayoikabili Wizara hii pamoja na Serikali kwa ujumla.

ii. Ukosefu wa ajira katika mahoteli kwa vijana wazawa: Kamati wakati ilipopata fursa ya kukagua hoteli mbali mbali za kitalii iligundua kwamba, waajiriwa wengi waliopo katika hoteli hizo ni wageni kutoka nje ya Zanzibar.

iii. Mabaraza ya Vijana: Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara, ilipata nafasi ya kuyatembelea mabaraza ya Vijana, katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia. Changamoto zilizogundulika katika utekelezaji wa kazi zao ni kama ukosefu wa Bajeti, Ukosefu wa Ofisi za kudumu, Uwepo wa Idadi kubwa ya Mabaraza ya Vijana,Mashirikiano madogo baina ya Viongozi wa Mabaraza na Uongozi wa juu wa Wizara pamoja na changamoto ya Kisheria:

Aidha, Baraza la Taifa kutokuwa na uwezo wa kujitegemea. Vile vile ukosefu wa masoko kwa shughuli na bidhaa zinazozalishwa katika Mabaraza mbali mbali. Kamati imegundua kwamba vijana wengi wamehamasika na suala la kujikusanya na kujiunga katika Mabaraza, hivyo, wameanza kujishughulisha katika uzalishaji wa bidhaa mbali mbali za kilimo, ufugaji, ujasiriamali n.k. Hata hivyo wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosa masoko.

IV. WAZEE

Mhe. Mwenyekiti, **k**undi jengine la kijamii ambalo Wizara imepewa majukumu ya kulishughulikia ni kundi la Wazee. Ili kuhakikisha Wazee wanakuwa katika hali nzuri ya kimaisha, jitihada zimewekwa na Serikali katika kuimarisha mazingira yao. Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii ambayo ipo chini ya Wizara hii inahusika kwa ukaribu zaidi. Kamati katika kufuatilia kwa kiasi gani Wizara inawashughulikia wazee, ilipata fursa ya kuzitembelea nyumba za wazee zilizopo Unguja (Sebleni) na Pemba (Limbani) na kupata fursa ya kuzungumza na wazee waliopo katika nyumba hizo, changamoto zifuatazo ziligundulika na Kamati:

i. Huduma dhaifu za chakula wanazopatiwa wazee wa Sebleni: Kamati haikuridhishwa na huduma ya chakula wanayopatiwa wazee wa nyumba ya Limbani pamoja na ile ya Sebleni, ambapo kiuhalisia haiendani na gharama za fedha zinazoingizwa na Serikali. Uchanganuzi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo, shilingi milioni 700,000,000 kwa nyumba ya Sebleni, ambayo ina wazee 31, shilingi milioni 5 kwa nyumba ya Welezo ambayo ina wazee 34 na shilingi milioni 1.5 kwa nyumba ya Limbani Pemba ambayo ina wazee 8, kwa kila mwezi.

ii. Wahudumu wa nyumba za wazee kutolipwa posho la mazingira magumu, Idara hii ilipokuwa Wizara ya Afya walikuwa wakipewa.

iii. Utofauti wa kiwango cha huduma wanazopewa wazee katika nyumba hizi.

iv. Ukosefu wa uzio katika nyumba ya Limbani Pemba, hali inayopelekea kutokuwa na usalama wa uhakika.

v. Hali ya mazingira hairidhishi, uchafu, baadhi ya swichi za umeme ni mbovu, vyoo vichafu, nyumba chafu n.k.

Mhe.Mwenyekiti, Kamati inaitaka Wizara kuandaa utaratibu maalumu, ambao utakuwa na usawa wa huduma zinazotolewa kwa nyumba hizi, katika ubora, ili kuondosha dhana ya utofauti, hasa ukizingatia kwamba wazee hawa wote wana haki sawa sawa mbele ya jamii.

WANAWAKE NA WATOTO:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara pia inahusika kwa kiasi kikubwa katika kusimamia suala zima linalohusu ustawi wa wanawake na watoto, nayo ikiwa ni sehemu kubwa ya jamii yetu. Katika utekelezaji wa kazi zake Kamati, ilijikita zaidi kuangalia suala zima la unyanyasaji wa kijinsia na udhalilishaji wa watoto linashughulikiwa kwa kiasi kikubwa.

Ili kujua undani wa suala hili, kwa sababu limekuwa likikuwa siku hadi siku, Kamati iliandaa Kikao cha pamoja na wadau wote wanaohusika na usimamizi wa suala hili wakiwemo, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na watoto, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka akiwemo Mkurugenzi mwenyewe, Kamishna Mkuu wa Polisi, Mkemia Mkuu wa Zanzibar, Wizara ya Afya, Mahakama n.k

Kamati iligundua changamoto zifuatazo ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia katika kulifanya tatizo hili liendelee kukuwa:

i. Ukosefu wa kifaa cha DNA, ambacho kina nafasi kubwa ya kutambua vielelezo vya ushahidi kwa njia ya kitaalamu, hasa ukizingatia kwamba matukio haya hufanyika kwa njia ya siri, hivyo ni muhimu na ni lazima kuweza kutumia njia za kisayansi kuweza kutambuwa vinasaba vya muhusika.

ii. Suala la maadili: Imegundulika kwamba ukosefu wa maadili kwa wahusika wanaosimamia kesi hizi yamepunguwa kwa kiasi kikubwa. Wenye dhamana kushughulikia masuala haya ikiwa watakosa uadilifu ikiwemo Polisi, Ofisi ya DPP, Mahakama, Madaktari na wengineo mmoja tu kati ya hao akikosa uadilifu kwenye kazi zake basi kazi ya kuwatia hatiani mtuhumiwa inakuwa ni ngumu.

iii. Ukosefu wa uelewa wa jamii jinsi ya kulishughulikia suala hili, kwa kujikita zaidi katika kutibu matukio haya wakati tayari yameshatokea, badala ya kushughulika zaidi na jinsi ya kuyakinga yasitokee.

iv. Uwepo wa sehemu nyingi za starehe ambazo zinaruhusu watoto wa umri mdogo ambao bado ni wanafunzi, bila ya kuchukuliwa hatua stahiki.

v. Suala la muhali kwa jamii yetu fulani na fulani tukae tuzungumze ili lishe na hii ni kasoro.

vi. Kubadilika kwa utaratibu mzima wa malezi ya watoto kwa wazee wao, ambapo watoto wamekuwa na uhuru uliopita mipaka, mapenzi yaliyopitiliza kwa watoto, maadili na dini kutozingatiwa tena, n.k.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kufanya utaratibu wa haraka, ili kuwezesha kupatikana kwa mashine ya DNA, ingawa suala hili linajulikanwa kuwepo katika mradi wa *Legal Sector Reform*, ambao DNA imepangwa kuwemo kununuliwa katika awamu ya pili ya mradi huo, lakini Kamati inaona ipo haja ya kutafuta njia mbadala na ya haraka kwa sababu kwa sasa hali ni mbaya na inazidi kuwa mbaya. Kamati inapendekeza katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kutenga fungu maalumu la kununulia kifaa hichi, na ikishindikana njia hii basi Serikali ipunguze baadhi ya vifungu vya fedha za Bajeti kwa kila Wizara ili kifaa hichi kiweze kununuliwa kwa haraka kunusuru maisha ya vijana wetu.

MASWALA YA JUMLA YALIYOJITOKEZA WAKATI WA KAZI ZA KAMATI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilikutana na maswala yafuatayo ambayo yanahusika na Wizara hii:

1. Suala la Kesi ya Mtoto Ibrahim Abdalla.

Nimesema mwanzo ili kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji wa majukumu ya ufanisi zaidi baina ya mihimili mitatu (Mahakama, Serikali na Baraza la Wawakilishi) ya dola. Kanuni ya 59 (4) inaeleza kwamba, “Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo langojea uamuzi wa Mahakama…”. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni hii Kamati hii isingepaswa kulizungumzia suala la mtoto Ibrahim Abdalla ndani ya taarifa hii.

Hata hivyo, kamati imeamua kulizungumza kwa sababu zifuatazo:-

i. Kuhakikisha kwamba haki na maslahi ya mtoto Ibrahim yanalindwa na kupatikana.

ii. Ili kuiwezesha Mahakama kufanya kazi yake kama inavyotakiwa, kutokana na ukweli kwamba kwa sasa Mahakama inashindwa kutoa maamuzi juu ya kesi hii kwa sababu wizara imeshatoa hukumu kabla ya Mahakama, kwa kumtorosha mtoto huyo Ibrahim Abdalla na kumpeleka kusikojulikana..

Maelezo ya kesi:

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, ya Baraza la Wawakilishi hii sio ya Mahakama hii kamati katika kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba, Kisheria pamoja na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ilipokea maombi ya barua kutoka kwa Bi Mashavu Kombo Maskini (Mlezi wa Mtoto Ibrahim) ya tarehe 24/08/2016 ya kuomba kusaidiwa katika kutekelezwa Agizo la Mufti wa Zanzibar la kukabidhiwa rasmi mtoto Ibrahim Abdalla.

Agizo hilo lilitolewa na Mufti wa Zanzibar baada ya kutokea mgogoro baina ya mlezi wa mtoto huyo na mtu anayedaiwa kama ni baba (Bw. Johnston Silas Mkala) wa mtoto ambaye anadai apewe mtoto wake, ambaye alimtelekeza kwa mlezi huyo tokea mama mzazi wa mtoto huyo alipofariki wakati mtoto akiwa na umri mdogo.

Ili kuweza kujiridhisha juu ya kadhia hii na kupata ufafanuzi wa kina kabla ya kuchukuliwa hatua yoyote, tarehe 29/08/2016, kamati ilifanya kikao na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuhusiana na kadhia hii ambapo aliieleza Kamati kwamba, mtoto Ibrahim alichukuliwa na Uongozi wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii na kuhifadhiwa katika nyumba ya serikali ya kulelea watoto iliyopo Mazizini. Baada ya kutokea mzozo baina ya mlezi na anayedai baba wa mtoto huyo, mzozo uliopelekea anayedai baba wa mtoto kumuiba mtoto na kwenda naye kusikojulikana mpaka pale Jeshi la Polisi lilipoingilia kati na kumpata mtoto huyo.
Hivyo, hatua ya kumuhifadhi mtoto huyo katika nyumba ya serikali ni kwa sababu za kiusalama, na Katibu Mkuu aliahidi mbele ya kamati kuwa hawezi kumtoa mtoto kumpa mtu yeyote hadi pale mzozo huo utakapopatiwa ufumbuzi wa kisheria.

Baada ya kamati kupata maelezo ya wizara, ilifanya ziara katika nyumba ya kulelelea watoto Mazizini na kupata nafasi ya kuzungumza na mtoto Ibrahim, ambaye aliiomba kamati imsaidie arejeshwe kwa mlezi wake ili akaendelee na masomo ya skuli na madrasa.

Mnamo tarehe 31/08/2016 kamati ilimuandikia barua rasmi yenye kumbukumbu namba BLW/K.10/17 VOL.III/16, Katibu Mkuu kuhusiana na kadhia ya mtoto Ibrahim ambapo ilitoa maagizo manne, yakiwemo kutekelezwa kwa agizo la Mufti la kumrejesha mtoto kwa mlezi wake (Bi Mashavu Kombo Maskini) na kumpa onyo kali la maandishi Ndg. Johnson

Silas Mkala aache tabia ya kuingilia uhuru wa mtoto Ibrahim na asirejee kitendo cha kumuiba kutoka kwa mlezi wake.

Baada ya kutotekelezwa kwa maagizo ya kamati yaliyotolewa kwa barua iliyotajwa hapo juu, na baada ya kamati kupata taarifa kwamba mtoto Ibrahim ameondoshwa katika nyumba ya kulelea watoto na kukabidhiwa kwa Ndg. Johnson Silas Mkaka na uongozi wa wizara, tarehe 20/11/2016, kamati ilifanya kikao na Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri ili kutaka kujuwa ni sababu zipi zilizopelekea kutotekelezwa kwa agizo la Mufti na maagizo ya kamati. Pia kamati ilitaka kujuwa utaratibu gani wa kisheria na kiutawala ulitumika kumtoa mtoto na kukabidhiwa kwa Ndg. Johnson Silas Mkaka.

Baada ya kamati kutopata maelezo ya kujiridhisha juu ya kilichotokea, ilitoa maagizo kupitia barua ya tarehe 21/11/2016 yenye kumbukumbu Namba BLW/K.10/17 VOL.III/28, ikiwemo kumtaka waziri ndani ya muda wa siku saba kuanzia tarehe 20 hadi tarehe 26 Novemba 2016, mtoto awe amesharudishwa katika Nyumba ya Kulelea Watoto - Mazizini, na kumuwasilisha mbele ya kamati, ili taratibu nyengine ziweze kuendelea.

Katika hali ya kushangaza na kusikitisha, tarehe 24/11/2016 kamati ilipokea barua ya majibu ya waziri kuhusu maagizo ya kamati ya tarehe 21/11/2016 ambapo pamoja na majibu mengine wizara ilieleza yafuatayo:
“
Kuhusu suala la kumrejesha mtoto na kumuwasilisha mbele ya kamati yako naomba kukufahamisha kuwa suala hili tayari limeshafikishwa Mahakamani na hatua yoyote kuhusu shauri hilo linapaswa kutolewa na muhimili wa Mahakama na sio wizara”

Kamati imesikitishwa na majibu haya, kwa sababu maelezo ya barua ya terehe 24/11/2016 yenye kumbukumbu Namba MMK/424/2016 iliyotoka kwa Mrajis wa Mahakama kwenda kwa wizara, inaonesha kwamba kesi hiyo imefunguliwa tarehe 21/11/2016, ambayo ni siku ya pili baada ya Kikao cha Kamati na Waziri kilichofanyika siku ya tarehe 20/11/2016 na kumtaka waziri amrejeshe mtoto ndani ya siku saba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kamati kupata mashaka kuhusu kesi hiyo kuwepo Mahakamani, tarehe 25/11/2016 kamati ilifanya kikao cha pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambapo ilishauriwa na kukubaliwa na kamati kwamba ni vizuri kushirikisha taasisi nyengine ambazo zinahusika na kadhia hii, ili kupata msimamo wa wizara juu ya suala hili.

Tarehe 28/11/2016 kamati ilikutana pamoja na taasisi mbali mbali zikiwemo, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Afisi ya Mufti na kadhalika, kauli ya mwisho ya wizara ni kwamba haina uwezo wa kumrejesha mtoto. Kauli ambayo iliwasikitisha wajumbe wote waliokuwepo katika kikao hicho, hasa ukizingatia kwamba lilitolewa mbele ya Mwenyekiti wa Kamati na viongozi mbali mbali wa serikali, kama Makatibu Wakuu wa Wizara, Mufti Mkuu wa Zanzibar, Mkuu wa Mkoa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa mjini Mjini Magharibi na kadhalika.
Na kwa kupitia barua ya tarehe 28/11/2016, wizara ilieleza kwamba:

“

"Wizara haina mamlaka ya kushinikiza baba mzazi kumrejesha mtoto. Hata hivyo, kama kamati inaona ina mamlaka ya kumrejesha au kumnyang'anya mtoto kwa mzazi wake, wizara haina pingamizi".

Mhe Mwenyekiti, mbali na barua hiyo wizara iliwasilisha kwa kamati nyaraka tofauti zinazohusiana na kadhia hiyo. Baada ya kamati kupitia nyaraka hizo, ilibaini yafuatayo:

1. Barua zinaonesha kesi (Mdai ni bi Mashavu Kombo Masikini, Kesi Namba 14/2016) imefunguliwa terehe 21/11/2016, kwa mujibu wa barua ya Mrajis ya tarehe 24/11/2016 ambapo inaonesha ni siku moja baada ya kamati kumtaka Mhe. Waziri kumrudisha mtoto na kumfikisha mbele ya kamati.

2. Tarehe 14/11/2016 waziri alimwandikia barua yenye kumbukumbu namba (WKUWVWW/2016/VOL.1/30/W.12), Ndg. Johnson Silas Mkaka kumtaka amrejeshe mtoto katika nyumba ya watoto Mazizini, ambapo tarehe 16/11/2016, Ndg. Johnson Silas Mkaka anajibu kwa kusema hawezi kumrudisha mtoto huyo kwa sababu kesi ipo Mahakamani, na haitakiwi kuingiliwa na muhimili mwengine. Hivyo, kamati imebaini kuna utata kuhusiana na tarehe hasa iliyofunguliwa kesi Mahakamani, ambapo baadhi ya barua zinaonesha kesi ilifunguliwa tarehe 21/11/2016, lakini maelezo ya anayedai baba mtoto yanaonesha kesi ilifunguliwa kabla ya tarehe hiyo. Hali hiyo inaifanya kamati kuwa na wasiwasi wa kuwepo hujuma inayofanywa ili kuifanya kamati isiweze kulishughulikia suala hili kwa kisingizio cha kuwepo kesi Mahakamani.

3. Udhaifu kwenye barua ya Ndg. Johnson Silas Mkaka pamoja na wizara kwa kusema kwamba suala hili lipo Mahakamani wakati kumbe kama ni kweli lipo huko ni kuanzia tarehe 21/11/2016 baada ya kamati kukaa na Mhe. Waziri na si kabla ya hapo

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI:

1. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na yote yaliyotokea, kamati inapenda kueleza masikitiko yake kutokana na kukosa mashirikiano kutoka kwa wizara, pamoja na kupuuzwa kwa maagizo ya kamati, hali iliyopelekea suala hili kukosa ufumbuzi hadi hii leo. Kutokana na hali hii, kamati inaona kitendo hicho ni kwenda kinyume na maadili ya utumishi wa umma, hivyo inashauri hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wahusika, kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

2. Kamati inaomba uanzishwe utaratibu maalumu kama haupo, wa jinsi ya kuwatoa watoto kwenye nyumba ya Mazizini ili kunusuru watoto kudhuriwa au kujikuta wameingizwa kwenye mikono ya wahalifu, kutokana na ukweli kwamba, wizara hutumia maagizo ya mdomo kwenda kwa Mkuu wa Nyumba hiyo, utaratibu ambao unaweza kutumika vibaya endapo mtu amekusudia kutekeleza uovu dhidi ya watoto waliopo hapo.

3. Kwa kuwa kamati haijuwi sehemu alipo mtoto Ibrahim kwa sasa, na haijui usalama wa maisha yake uko katika hali gani, kamati inaiomba serikali kutumia uwezo na nguvu zake kuhakikisha mtoto anarudishwa Zanzibar ili kumuepusha na kuzidi kuathirika kisaikolojia kwani mazingira anayoishi kwa sasa hajawahi kuyaishi katika umri wake wote. Kuendelea kuweko huko kunamkosesha haki zake za msingi ikiwemo ulinzi, amani, usalama wake binafsi, elimu.

4. Kwa kuwa nyaraka zilizowasilishwa kwenye kamati zina utata juu ya lini kesi hii imefunguliwa Mahakamani, kamati inaomba suala hili lifuatiliwe kupitia Ofisi ya Mrajis wa Mahakama Kuu Zanzibar, na ikiwa kuna udanganyifu wowote umefanyika wa kuipatia kamati taarifa ambazo si sahihi, basi hatua za kisheria (Kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Wajumbe namba 4, 2007) na za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya wahusika.

5. Kutokana na kuwepo kwa agizo la Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuitaka wizara kumrejesha mtoto katika nyumba ya kulelea watoto – Mazizini, na kwa kuwa agizo hilo halijatekelezwa hadi leo, kamati inaona hiki ni kitendo cha kukiuka maadili ya uongozi kilichofanywa na watendaji wa wizara hii.

6. Mwisho, kwa kuwa lengo la kamati si kuingilia suala liliopo Mahakamani, bali ni kuhakikisha mtoto anarudishwa kwenye Nyumba ya Kulelea Watoto na taratibu nyengine za kimahakama ziweze kuendelea, hivyo bado kitendo cha wizara cha kumkabidhi mtoto kwa anayedaiwa kuwa ni baba

wa mtoto Ibrahim si sahihi na kimekiuka utaratibu wa kiutawala (Agizo la Mufti na Maagizo ya Kamati). Lakini pia kitendo hicho kimekiuka taratibu za kimahakama kwa kuwa Mahakama ndiyo ilipaswa kutoa maamuzi juu ya nani mwenye haki ya kupewa mtoto na sio wizara. Kamati haiungi mkono kitendo hiki na inaomba sana arejeshwe haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imesikitishwa na hatua iliyochukuliwa na wizara ya kumtorosha mtoto Ibrahim, na kumpeleka kusikojulikana kitendo ambacho kilitarajiwa kifanywe na mtu mwengine na sio wizara inayosimamia maslahi mema ya watoto, na inaitaka wizara kutorudia tena kitendo hicho ambacho kinakiuka Sheria za nchi.

Suala la kuhamishwa Bi Saada Aboubakar Abdi:

Mhe. Mwenyekiti, Bi Saada ni mfanyakazi wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ambaye alikuwa ni Msimamizi Mkuu wa Nyumba ya Kulelela Watoto Mazizini. Wakati kamati ikiendelea na kazi zake za kawaida ililazimika kumwita na kutaka atowe ufafanuzi kuhusu suala la mtoto Ibrahim Abdallah ambaye alikabidhiwa kwa mtu anayedaiwa kuwa ni baba yake bila ya kufuata taratibu za kisheria.
Kamati ilibaini kwamba, hiki kilichotokea kimetokana na hatua ya mama huyo kutoa ushirikiano kwa kamati wakati wa kufanya kazi zake.

MAAGIZO YA KAMATI:

i. Kamati haikuridhishwa na hatua hiyo iliyochukuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara na inaiagiza wizara kumrejesha mama huyo katika eneo lake la kazi kama kawaida.

ii. Kamati inaitaka wizara kuacha vitendo vya kuwadhalilisha watendaji wanaotoa mashirikiano kwa kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, kwa kuwa kamati ipo kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za nchi hii.

iii. Kamati inaitaka wizara kumuandikia barua ya kufuta shutuma zote zilizotolewa dhidi yake kwa kuwa hazina ushahidi wowote.

HITIMISHO NA SHUKURANI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi inapenda kuchukua nafasi hii adhimu kuipongeza kwa dhati Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mashirikiano makubwa

waliyoipatia kamati hii kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake katika mazingira yote tuliyokwenda nayo.

Aidha, kamati inatoa pongezi maalumu kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid Ali Juma, Naibu Waziri Mhe. Chum Kombo Khamis, Katibu Mkuu Ndg. Omar Hassan Omar (King) mtani wangu wa jadi, Manaibu Katibu wakuu wote, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa mashirikiano yao ya dhati wakati wote kamati hii ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, kamati inampongeza Afisa Mdhamini wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Pemba Ndg. Khatib Juma Mjaja kwa juhudi yake nzuri tumefanya nae kazi kwa moyo wote bila ya kujali wakati na kujali shida ya usafiri waliokuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inawapongeza, watendaji wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, wakiwemo Naibu Waziri Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara, Wakurugenzi, Afisa Mdhamin Pemba na wafanyakazi wote tulioshirikiana nao.

Mwisho, na kwa umuhimu mkubwa kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wetu, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati Ndg. Ramadhan Khamis Masoud kwa kuiwezesha vyema kamati kutekeleza majukumu yake na leo kuweza kuwasilisha ripoti yake kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya yote hayo kwa heshima na taadhima kwa niaba ya kamati yangu naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Simba ilishinda kidogo nimepatwa na mughma. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wako kwa umakini bila ya kutetereka, hoja imeungwa mkono mjadala unaendelea.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru, lakini kwanza naomba kusimama na Kanuni ya 147. Mwanasheria leo katupa darasa kubwa hapa, naomba kuisoma kwa ruhusa yako.

Kanuni ya 147 inasema kwamba:

"Kwa idhini ya Baraza, yoyote kati ya Kanuni hizi yaweza kutengwa kando kwa madhumuni mahsusi baada ya Mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo".

(3) "Maelezo ya Hoja yote ya kutaka kutenga kando Kanuni yoyote yatakuwa ni pamoja na maelezo kuhusu madhumuni ya kutaka Kanuni hiyo itengwe kando".

Sasa madhumuni, viongozi wetu akiwemo Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wamepiga kelele sana kuhusu kadhia hii mpaka jana sisi sote mashahidi. Muda wa dakika 15 hautatosha kwa mjadala huu muhimu naomba baada ya dakika 15 ziongezwe 10 ziwe 25.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Kanuni hii uliyosema kwamba tuitengue namuomba Mhe. Mwanasheria alitolee maelekezo zaidi kuhusu kanuni hii, kwa sababu tulishaliogelea sana suala hilo hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hoja ya Mhe Jaku Hashim inahusiana na kanuni ya muda ya kuchangia mjadala, kama kanuni inasema mjadala utajadiliwa kwa dakika 15 Mhe. Jaku Hashim yeye anaomba kutenga kando Kanuni hiyo ili mjadala ujadiliwe kwa dakika 25. Nadhani ndio hoja yake kama nimemsikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nimekuelewa lakini kulingana na ratiba zetu za hili jambo dakika 15 kama zilivyo zinatosha. Mwisho ni dakika 15 tu, naomba ujitahidi kwa mjumbe yeyote kutumia muda ambao tumeuweka. Ahsante endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, siwezi kushindana na kiti chako, lakini baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nami nikupe pole wewe kwa bahari ilivyotaka kuchafuka kidogo na kiti chako kikatumia hekima na makatibu wetu kwa umakini wao wa hali ya juu wametumia busara zao. Niwapongeze sana makatibu wawili hawa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mhe. Rais kwa ziara yake ya jana aliyoifanya na baadae ikazaa matunda na tukayaona kwa pale aliposema:

"Kulu Hakku Wakanu Murwa", alipowaambia mawaziri na manaibu waziri. Baada ya hapo sasa nijikite kwenye hoja iliyokuweko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kifupi na kwa kirefu maelezo yangu niwasilishe kwa maandishi kwa mtoa hoja ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 58(7)(8). Naomba maelezo hayo ya maandishi yawasilishwe kwa Katibu wa Baraza na yenyewe kwa mujibu wa Kanuni yawasilishwe *Hansard* kwa sehemu ya mchango wangu. Mheshimiwa mchango wangu utakuwa mkubwa pengine dakika 15 hazinitoshi itabidi mengine niyalete kwenye meza nimpe katibu na mengine nitaomba hata kwa Mhe. Rais yaende.

Pia naomba nakala ya mchango huu wa maandishi ipatiwe kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa umuhimu wa suala lenyewe linalohusu udhalilishaji wa watoto. Naomba pia ifikishwe kwa Mhe. Rais ambaye anakerwa sana na yeye yuko mstari wa mbele kwa kupinga na kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa watoto, nami niko pamoja naye namuunga mkono. Madhumuni yangu ni kuisaidia serikali kukubaliana na kila kikwazo katika vita hivi na kupambana na udhalilishaji ikiwemo vikwazo vinavyobainishwa kwa watu waliopewa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hili la mtoto lililotajwa kwenye ripoti ya kamati naomba nieleze yafuatayo. Kwanza ninatambua kuwa suala lipo mahakamani nami sitazungumzia chochote kuhusu mambo yaliyo mahakamani kwa kuwa kanuni zetu haziruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kuhusu jambo hili ni mambo ambayo yapo kabisa na mambo ya mahakama, lakini nataka Baraza lako hili tukufu litambue na wananchi wajue, serikali ijue kuwa yapo mambo lazima tuambizane ukweli na tusipoambizana ukweli wananchi watatudharau, wataidharau serikali, watamdharau Rais, watawadharau mawaziri, zitadharauliwa mamlaka za nchi na mwisho wenyewe tutadharauliana. Chombo hiki kitadharauliwa kwa kuwa wananchi wanajua ukweli wa mambo hayo. Miongoni mwa jambo hili tusidhani kuwa huko nje wananchi hawajui kinachoendelea wanatuuliza sisi kwa dhamana tulizopewa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kwenye kadhia hii nataka nizungumzie ulinzi wa watoto kuhusu nyumba ya Mazizini. Mheshimiwa naona hapa kidogo patakuwa pana mtihani, hivi karibuni amebakwa mtoto katika mikono ya serikali nyumba ya Mazizini, jina ninalo na nimelihifadhi ndani ya mikono ya serikali. Sasa tutafika hatua gani ikiwa ndani ya mikono ya serikali mtoto anabakwa

tutachukua hatua gani? Ndio niliposema hii wizara ishashindwa kusimamia majukumu yake.

Kwanza waziri na katibu mkuu wake wameingilia uhuru wa Mahakama na wameidharau, kitendo hiki ni kinyume cha katiba katika hii kesi iliyozungumzwa hapa, waziri na katibu mkuu wameingia kinyume na Katiba ya Zanzibar, hii ni kuidharau Mahakama na kitendo walichokifanya wao kesi iko Mahakamani haijaamuliwa leo unamchukua mtoto kupoteza ushahidi. Katibu mkuu huyo anasema mtoto huyo hatoki kwenye kamati, mimi Mjumbe wa Kamati kwanza *declare interest,* hii ni dharau tena ya mwisho. Katibu kaja kaomba radhi kwenye kamati sijui wajumbe wenzangu wamekubali au hawakukubali, lakini kwa ubinadamu wangu mimi na mimi ni muungwana nimemsamehe katibu mkuu wala sina tatizo naye kaniomba radhi wenzangu watajua wenyewe. Lakini leo itafika wakati watoto wote watatoroshwa pale katika nyumba ya kulelea watoto, serikali haijui ni kitu cha aibu, mtoto analelewa ndani ya mikono ya serikali huku tunapiga vita, ndio nikasema huu mchango wangu itabidi nakala moja iende kwa Mhe. Rais baada ya kumkabidhi Makamu wa Pili wa Rais itakwenda na kwake.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein hapa naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti. Tarehe 9/02/2017 amesema, "Nashukuru mimi siingilii Mahakama wala sitawahi". Hayo jana tumeyasikia akazungumza, leo waziri au katibu mkuu au wawajibikaji leo Rais amekuwa mdogo kuliko watendaji wa wizara hii kuingilia Mahakama. Katika maadhimisho yake ya sheria Mhe. Rais amesema hivyo na jana alitwambia maneno hayo leo mtoto kahifadhiwa. Kamati imekwenda mtoto mwenyewe akalia akasema mimi sitaki kwenda kwa baba yangu ninasoma, utalia Mhe. Mwenyekiti, huyo hapo Mhe. Ali Suleiman Ali analia hivi sasa machozi yanataka kumtoka. Tumekwenda hatukutaka ushahidi wa Kinyamwezi tumekwenda kushuhudia, si makosa ya unyamwezi. Siwezi kufuta radhi mimi nikaambiwa muhindi ni kabila, Unyamwezi kabila, Mzungu kabila, Muhindi kabila siwezi kuomba radhi kwa hili mtu hawezi kukataa kabila lake tunachokizungumza tuna uhakika nacho.

Kwa hiyo, hiki ni kitendo ambacho hatuwezi kufika tunapiga kelele siku zote. Lakini kama hilo halitoshi waziri na katibu mkuu ndio hayo ninayosema wamevunja sheria, leo kesi iko Mahakamani mtoto yupo tumemuona leo unakuja kumtorosha kwa mlango upi, kwa maana na wale wengine watatolewa watapelekwa kwengine kokote serikali haijui, ndio nikasema kuna mtoto kabakwa sasa hivi.

Waheshimiwa Mawaziri serikali inasemwa vibaya na watu huko nje kwenye mitandao ya jamii kwamba inamuogopa waziri na katibu mkuu jamani ni kweli? Dkt. Ali Mohammed Shein ni shupavu katueleza jana haya, hawezi kumuogopa mtu wala kumstahamilia yeye ndiye mamlaka ya nchi hii, hawezi kuyumbishwa na mtu lakini hivi hatuwezi kwenda na wizara inaonekana bado haijawa *serious*.

Leo Bi Mashavu mwisho inawezekana ikawa kwa umasikini wake ndio afanyiwe kitendo hiki? Mhe. Waziri yasingefika haya kama angeyataka, amekataa amri ya Makamu wa Pili wa Rais.

Utaratibu

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 59(3) kinasema hivi:

"Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kutamka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitsho wa usemi wake unaohusika". Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ueleze hoja yako nini.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Naomba uthibitisho wa maneno yote anayosema na mambo yote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ni mgeni kwa humu ndani ya Baraza si mgeni kwengine aa, anataka ushahidi gani na tumeshakaa naye kwenye kamati na maelezo amesema kwenye kamati, uwezo wa kumrejesha mtoto hawana sasa uthibitisho gani. *(Makofi)*

Wajumbe hawa hapa ninao mimi niliofanyanao kazi, mtoto yuko tumekwenda kumhoji sasa nithibitishe kitu gani anieleze tu, kipi nimthibitishie.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kamati humu haina mengi ambayo ni ushahidi naomba awasilishe mezani.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakuelewa, Mhe. Waziri hebu nyanyuka uelezee suala lako vizuri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Sipendi niendelee kuzungumza kwa sababu suala hili liko Mahakamani ni masuala ya uthibitisho mengine yote hayataweza kufanyika hapa Mheshimiwa samahani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi muda wangu unapotezwa kinjia lakini naomba unilinde kwa muda wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante. Mheshimiwa kiongozi wetu mkuu wa serikali humu ndani ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ametumia nasaha maneno ya hekima, mawaidha mazuri kwa wizara hii lakii ikishakufikia kwamba anadharauliwa Rais, Makamu wa Pili wa Rais tutakwenda wapi. Kabembelezwa, tumeshafanya vikao zaidi ya sita lakini tusingefika hapa, maneno mazuri ni sadaka, maneno mazuri humtoa nyoka pangoni, lakini hiki kiburi na jeuri sijui imetokea wapi tunafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna bibi Bi Saada kaondoshwa. Ee Mwenyezi Mungu mkubwa Mhe. Mwenyekiti wee, baada ya kuondoshwa ndio kukatokea tukio hili. Mwenyezi Mungu anamlinda huyu Bi Saada kubakwa mtoto mle ndani baada ya kuondoshwa yeye na huku wizara sijui inatafuta utaratibu gani wa kumuwekea Bi Saada akaondoshwa akaambiwa kuwa kashirikiana na kamati imekuwa makosa. Tumesema katika ripoti yetu arejeshwe leo limetokea hili Mwenyezi Mungu kamlinda ya kubakwa mtoto katika mikono ya serikali au na hilo waziri anataka nithibitishe pia, tunafanya kazi kwa niaba ya wananchi mimi simchukii mtu wala sitoweza kumchukia mtu. Mimi sijesha kuumbwa na kama hujafa hujaumbika, naweza nikaanguka wakati wowote akaniokota mtu hapa.

Sasa hapa mfano unaondoka unakwenda zako...

Mhe Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako bado dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, muda wangu umepotezwa kwa njia za ufundi naomba uulinde muda wangu. Unakwenda zako Italy au Urusi utawaambia watu wale mazingira gani maneno kama yale si unatafuta ugomvi, wengi wape. Wewe unakwenda kukaa Italy au Urusi watu utawafahamisha lugha gani pale, tusingefika haya ni mambo ya ajabu mno.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza usije ukamaliza muda ni-*sign* hizi *document* nilete kwako huko kwenye meza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako umemaliza anayeendelea ni Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Jaku hashim Ayoub: Aa naleta *document* kwako. Naomba ikitoka kwa katibu ije kwa Katibu wa Baraza iingie *hansard* hii. Namaliza ndio sina muda.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubui ya leo ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa ripoti yake nzuri ijapokuwa imebanwa kidogo na vifungu vya katiba ya nchi yetu kifungu cha 5A(1),(2) na (3) kuna mambo sisi yametufunga kuyajadili, lakini Mhe. Jaku Hashim Ayoub kidogo kapenyeza penyeza yamekaa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende kwenye habari huko kwenye uwezeshaji leo naondoka kabisa. Naomba niende katika ripoti hii kwenye *ZBC*, ukurasa wa sita Kampuni za Uunganishaji Maudhui *ZMUX*. Nimepitia kwa makini ripoti hii lakini kuna kifungu cha ripoti hii katika maeneo ya changamoto imeeleza kuwepo kwa kampuni hii ya *ZMUX* ndani ya Wizara ya Habari kiutendaji kwao ni mgongano na waandishi hawataweza kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Kipengele hiki ukikipitia vizuri utakuta *ZBC TV* yenyewe ina taratibu zake za kuendesha taasisi au shirika lake na ina bodi yake, lakini kwa maelezo ya mwenyekiti hapa maelezo yake ametuwekea kuwa kuna kampuni inaendeshwa na wizara ambayo nayo inabeba maudhui makubwa katika kuisukuma hii *ZBC*. Sasa napata mashaka sana tukifika kampuni hii yenye kubeba maudhui ya *ZMUX* tukiweka wizarani ina maana kuna mikataba itafungwa na wizara siku hawa wakauza hata ving'amuzi vitauzwa na wizara, mana hii kampuni iko kule. kuna changamoto zipi ndani ya *ZBC* zinazofanya mpaka *ZMUX* hii ikabaki katika wizara isibaki ikasimamiwa na mkurugenzi mwenyewe na bodi ya *ZBC*? Sasa kuna mashaka hapa, lakini chombo hiki kinatiliwa pesa na serikali katika *investment* yake.

Mimi nakumbuka katika mikataba iliyojazwa kuna *twenty percentage* za kusaidia *ZBC*, kuna *twenty percentage* ambayo inakwenda kwa huyu *expert* ambaye alikuwa anaendesha hii kampuni, lakini kuna *sixty percentage* hii ni *capital investment.* Toka kuanzishwa hapa na chombo hiki kipo na kwa sababu kinasimamiwa na wizara mimi naomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati katika

ripoti yake basi pia ibaki katika sehemu ya maadhimio kuonekana hii *twenty percentage* ambayo *ZBC* itasaidia kuendesha shughuli zake kama ni faida ya kuwekeza katika chombo kile inapatikana na imepatikana kiasi gani.

Hata hivyo, hii *capital investment* ambayo ilikuwa inarudi kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali nayo imeanza kurudi au kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali nayo imeanza kurudi au tunaingiza fedha tu na shughuli zinaendelea lakini hakuna kinachorudi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti hasa wa kamati hapa napo katika moja ya majukumu yako ya kamati pasimamie vizuri sana. Kwa nini kwanza tuone *ZMUX* inasimamiwa na wizara mikataba yake inakwenda kule wakati *ZBC* ni taasisi ambayo imepewa Mkurugenzi lakini taasisi ambayo imepewa bodi. Sasa kwa nini maana hata ukija kuangalia ile nguvu ya taasisi hii imetokana na *ZBC* unawahamisha wafanyakazi wale unahamisha na mishahara yao unaenda kuiundia taasisi yake juu.

Kwa hiyo, serikali imepeleka waziri jembe lakini bado watu wananganganiana sehemu hizi za majukumu wizara ina majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuisimamia taasisi hii lakini si kuiendesha, maana haya ni mazingira ya kuiendesha sisi tunapata mashaka sana. Kwa hiyo, ripoti yako Mhe. Mwenyekiti mimi naiopongeza sana kunako eneo hilo. Eneo hilo mmelichambua vizuri jambo kuwa na sisi tulikuwa na taarifa za kina.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende sasa Kamisheni ya Utalii. Kamisheni ya Utalii nilizungumza juzi tu kwa ufupi katika masuala ya nyongeza. Lakini leo humu katika ripoti yako Mhe. Mwenyekiti umeieleza vizuri na nikushukuru sana kamati yako imefanya kazi vizuri inaonesha sasa uwezo wa kamati yako umepeya pamoja na Mwenyekiti kuwa mzoefu.

Mhe. Mwenyekiti, kunako eneo hili juzi mimi nilizungumza uwepo wa vikao vya bodi ambavyo vinaisaidia Kamisheni hii, havipo na havikuwepo katika mwaka huu wa fedha 2016/2017. Havikuwepo katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, bodi hii ya Kamisheni ndio inayo uwezo wa kusaidia kuratibu shughuli za Kamisheni ya Utalii kwa sababu kuna taasisi mbali mbali uundwaji wake katika ile bodi Wajumbe wake wanatokea katika taasisi mbali mbali ambazo zinasukuma maendeleo ya utalii nchini.

Sasa leo vikao vya bodi vikiwa havifanyiki na Wajumbe wa bodi waliteuliwa tunapata mashaka sana. Kwa sababu bajeti katika mwaka wa fedha bodi hii imetengewa na Baraza hili lakini vikao havifanyiki. Sasa kama Wajumbe

waliteuliwa wamekaa miaka mitatu hawajafanya kazi hata siku moja sijui kuna uhai gani Mhe. Waziri baada ya miaka mitatu wakimaliza muda wao utawateuwa tena maana hawajafanyaka kazi hata siku moja, waendelee na hii au unafukuza wale unawapeleka wengine kwa sababu wao hawakukukaa hata siku moja na huwawezesha kukaa maana tunapata mashaka kidogo. Kwa hiyo, tuone Mhe. Waziri na Mhe. Mwenyekiti katika kushughulikia Sekta ya Utalii chombo hiki kiwepo kwake ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nilisema nichangie maeneo hayo tu mawili, hili eneo moja nilikuwa nasubiri kwa hamu lakini katiba ya nchi yangu na kanuni ya 108 (17) hairuhusu naomba nikae kitako naheshumu Katiba na naheshimu kanuni ya chombo hichi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Nassor Salum Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ambayo imesomwa na Mwenyekiti Mhe. Ali Suleiman Shihata na leo hii amethudhihirisha kwamba yeye ni kiongozi imara na ndio wakamchangua katika Kamati ile Maalum ya Ushindi, hongera sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Mwenyekiti, aidha pia nichukuwe fursa hii kusema ule msemo wanaosema "Kelele za mlango hazimzuii mwenye nyumba kulala" nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kazi nzuri anayoifanya na jana hotuba yake wakati anazindua mashindano ya majimbo kule CCM Mkoa hotuba ambayo imezihisha kwamba Mhe. Rais ni kiongozi imara mwenye kujali na ambaye amesimama kuwaletea wananchi wote kwa ujumla maendeleo na kuhakikisha kwamba CCM inasonga mbele na ule msemo unaosema "Hapa kazi tu".

Mhe. Mwenyekiti, yale ambayo yalikuwa yamesemwa yakizungumzwa kwenye mitandao jana mwenyewe ameyajibu na sote tumesikia na tumuombee Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu aendelee kutuongoza katika kipindi hichi mpaka 2020 ili kutuletea maendeleo kwa wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu niende katika Sekta ya Michezo. Mhe. Mwenyekiti kama alivyozungumza Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati hii kwamba mchezo wa mpira wa miguu ni mchezo ambao unapendwa hapa Zanzibar na ulimwengu kwa ujumla na mchezo huu ni mchezo ambao unachukuwa mashabiki wengi na ambao unaleta ajira na faida kubwa ya mapato ya kinchi kwa nchi mbali mbali ulimwenguni.

Mhe. Mwenyekiti, mchezo huu unaingiza mamilioni mengi ya fedha na ajira nyingi kama nilivyotangulia kusema. Lakini hali ya Zanzibar katika mchezo huu bado ni tete hasa katika kipindi hichi kilichopita, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita hali ilikuwa mbaya zaidi. Lakini nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Rais na kumpongeza sana kwa kuweza kumchagua au kumteua Mhe. Ali Rashid Juma kuwa Waziri wa Habari, Utalii na Michezo na kwa kweli kwa juhudi zake na kazi kubwa ambazo anazifanya matunda yake yanaanza kuonekana kwa kushirikiana na Katibu Mkuu wake.

Lakini kwa kweli kumekuwa na tatizo kubwa sana ambalo bado na changamoto kubwa kwa Zanzibar kuendeleza mchezo wetu huu wa mpira wa miguu hususan ni kukosekana kwa udhamini wa vilabu vyetu pia na Timu yetu ya Taifa "*Zanzibar hiroes* "**.**

Mhe. Mwenyekiti, mchezo wa Mpira wa miguu bila ya kuwa na mdhamini au kupata fedha za kuweza kuendeleza michezo ni tatizo kubwa na hii inatokana na migogoro mbali mbali ambayo inakuwa inaikabili vyama vyetu vya michezo hususan Chama chetu cha Mpira wa Miguu *ZFA*. Lakini kwa juhudi kubwa ambazo amechukuwa Mhe. Waziri hali ya migogoro imepungua kwa kiasi kikubwa na nina imani kwamba huko tunakokwenda mambo yatakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Baraza la Michezo la Taifa BTMZ. Mhe. Mwenyekiti Baraza la Michezo la Taifa ndicho chombo ambacho kinasimamia vyama vyote vya michezo na ndicho chombo ambacho ndio mlezi wa vyama vyote. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli aliyoyazungumza Mwenyekiti wa Kamati ni sahihi kabisa ukizingatia kwamba hali ya ufinyu wa bajeti inasikitisha sana. Lakini vile vile hali yenyewe ya uongozi wa Baraza la Michezo nimuombe sana Mhe. Mwenyekiti wa Baraza la Michezo awe karibu sana na vyama vya michezo hususan chama cha Mpira wa Miguu na vyama vyengine ili kuhakikisha kwamba anavisaidia kwa hali na mali ili kuweza kukuza michezo yetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais amefanya kazi kubwa katika kipini chake hichi katika kuinua hali ya michezo hasa ukizingatia kwamba katika kuboresha hali ya michezo Zanzibar ana mipango mizuri ili kuhakikisha kwamba Zanzibar tunasonga mbele katika sekta hii ya michezo. Nimshukuru sana kwa kuwa maamuzi yake ya serikali kuhakikisha kwamba kinajengwa tena kiwanja chetu cha mpira ya Mao tse tung.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanja chetu cha Mao tse tung ni kiwanja ambacho cha historia kubwa cha miaka mingi serikali imefanya maamuzi mazuri kuweza kuujenga tena uwanja ule na nina imani kwamba wananchi wa Jimbo la Kikwajuni wataweza kufaidika na ujenzi ule kwa kupata ajira mbali mbali na wananchi wengine ambazo zitaweza kuzifanya kwa kazi ambazo zitakuwa zinafanywa pale.

Kubwa ambalo nina imani kwamba katika kuinua michezo Zanzibar mbali na kujenga hivyo vya Mao na viwanja vyengine kamati imezungumzia pia suala la kujenga viwanja katika wilaya. Mhe. Rais alikuwa na maamuzi makubwa na mazuri katika kujenga viwanja katika kila wilaya. Niombe serikali kwa kupitia wizara hii kuhakikisha kwamba kila wilaya inakuwa na uwanja wa mpira ili kuhakikisha kwamba Zanzibar tunasonga mbele katika kudumisha michezo yetu na kukuza vipaji kwa Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Wizara ya Uwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuweza kuwajali na kuwaenzi wazee wetu ambao wanaanzia miaka 70. Mheshimiwa hili jambo ni jambo ambalo kwa kweli tunastahili sote kama viongozi kama Wawakilishi na Wabunge na wananchi kwa jumla kumpongeza Mhe. Rais kwa maanuzi yake na mapenzi yake kwa kuweza kuwasaidia wazee angalau posho kidogo kwa kila mwezi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii pia kuwapongeza viongozi wa Jimbo la Kikwajuni akiwemo Mbunge, Mwakilishi pamoja na Madiwani wake na uongozi mzima wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuweza kumuunga mkono Mhe. Rais kwa kuweza kuwakatia Bima wananchi ambao wanatimia miaka 70 na kuendelea ili kuweza kupata matibabu bila ya matatizo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii pia kuwaomba Wawakilishi wenzangu pamoja na Wabunge ili kuweza kumuunga mkono Mhe. Rais kuwaenzi wazee wetu katika majimbo yetu, kwa sababu kuwaenzi wazee ni baraka kubwa kwa faida yetu na faida ya nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kazi kubwa ambayo inafanywa na Mhe. Rais ni wajibu wetu sisi kuyaunga mkono. Kwa sababu maendeleo ambayo tumeyapata Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla inatokana na uongozi bora wa viongozi wetu chini ya serikali cha Chama cha Mapinduzi ambayo Mhe. Rais anaongoza serikali yake. Mheshimiwa bila ya CCM Tanzania haiwezi kuleta Maendeleo. Lakini chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi maendeleo mengi ambayo yamepatikana katika nyanja mbali mbali sisi tukiwa kama viongozi ambao tumetokana na Chama cha Mapinduzi ni wajibu wetu

kuwaunga mkono viongozi wetu na kukiunga mkono Chama chetu cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nije katika Shirika la Utangazaji *ZBC*. Shirika la Utangazaji *ZBC* limekuwa na changamoto kuwa sana hasa ukiangalia katika kipindi cha nyuma kulikuwa na changamoto kubwa lakini vile vile imekuwa ikipiga hatua siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, *ZBC* imeanza kubadilika mbali na kuwa na matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili ikiwemo mambo ya ufinyu wa bajeti, vitendea kazi lakini vile vile kuna tatizo ambalo Mheshimiwa maslahi ya wafanyakazi. Maslahi ya wafanyakazi imekuwa changamoto kubwa kwa watumishi ya *ZBC*, kwa hiyo nimuombe Mhe. Waziri kulifanyia kazi ili mbali na uboreshaji wa *ZBC* lakini maslahi ya wafanyakazi wa *ZBC* yaweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikupongeze sana, nimpongeze Mhe. Spika, pamoja na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kazi kubwa ambayo umefanya Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kulipa *ZBC* maslahi yote bila ya kuwepo na deni, hii ni pongezi kubwa ambazo ni kazi nzuri ambayo mmeifanya Baraza la Wawakilishi ili kuweza kutoa maslahi kwa *ZBC*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimpongeze sana Mkurugenzi wa *ZBC* kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa kuibadilisha *ZBC*. *ZBC* sasa hivi si ile ya mwaka jana iliyopita. Amefanya kazi nzuri ni wajibu kumpongeza ili aendelee na juhudi hizo ili kuhakikisha *ZBC* inaenda na wakati.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii. Mheshimiwa nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii adhimu kukushukuru kunipa fursa ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijanza kuchangia nataka nitoe indhari ndogo kwa wenzangu Wawakilishi kila mtu ana haki ya kuchangia kwa mujibu anavyohisi. Lakini naomba na mimi niwaelekeze tu kwa sababu tunaongozwa na taratibu na vyombo vya sheria ninukuu kanuni ya Baraza kifungu cha 66, 1 (b) ili kuwatanabahisha tu kuwa pamoja na michango yao tunatakiwa kutumia Vikao vya Baraza au Kamati kulinda haki na maslahi ya wananchi kwa mujibu wa maamrisho ya Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na maadili ya taifa.

Sasa lazima tujue kwamba kuna vyombo ambavyo vinatuongoza katika kulinda haki na maslahi kila mtu ana haki yake na fursa yake. Kuna wengine walihisi jambo hili kwao wao labda haliko kihaki haliko sawa wameanza kukumbilia katika Vyombo vya Kisheria vya Kimahakama na sheria zinaturuhusu. Kwa hiyo, naomba sana tunapochangia tuangalie pande zote mbili katika uchangiaji wetu Mheshimiwa. Sitaki kuwazuia katika hili lakini pia tutizame fursa za sheria na katiba ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo naomba nianze kuchangia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii kwa umahiri wake Mhe. Ali Suleimana Ali (Shihata) ni Mwenyekiti mzoefu hata sisi ametulea katika maeneo mbali mbali ametufunza mengi hadi sasa hivi tunapata muda wa kuweza kujitanua.

Mhe. Mwenyekiti, michango yangu mimi inakwenda katika maeneo matano. Eneo la kwanza Mhe. Mwenyekiti, ni katika eneo la Pencheni ya wazee ya shilingi elfu ishirini. Nimshukuru Mhe. Rais kwa maamuzi yake ya busara katika namna bora ya kuwaenzi wazee wetu wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa napitia kamati taarifa ya kamati hii kuna mambo ambayo nimeyaona kamati wameweza kuyaelezea kwamba inaonekana kwamba kuna mkanganganyo wa uandikaji wa taarifa nzuri katika kuwapata hao wazee na kunajitokeza matatizo mengi sana wakati wa malipo ya wazee hawa kwa sababu hawa ni binaadamu na binaadamu anakuwa na maisha na baadae anafariki.

Inaonekana kwamba hakuna taarifa nzuri kwa wale ambao wazee wanafariki katika suala zima la uhakiki wa kutunza fedha hizi za serikali. Kamati imeeleza mengi sitaki kuyachambua moja baada ya jengine. Lakini inaonekana kwamba taarifa hazipatikani kwa usahihi kwa wale watu ambao wanafikia muda wa kufariki na pesa zao zinakuwa zinakwenda katika maeneo kwa ajili ya malipo.

Lakini katika hili taarifa pia imeelekeza au imeonesha kwamba hakuna utaratibu mzuri pia kwa wale wazee ambao wanatimia umri wa miaka 70 kwa sababu umri unakuja kila wakati leo inawezekana nina miaka 69 na siku 20 kesho inaendelea na siku 25 maana yake kinchoonekana kila mwezi kutakuwa na wazee ambao wanafikia miaka 70. Sasa mimi niungane na kamati ya kuiomba wizara kuangalia namna bora ya kuandaa kitengo cha *data base* katika kuwapata wazee wataotumiza miaka 70 na ni vyema basi kungeweka angalau tukaingiza wazee kuanzia miaka 65 katika *data base* tukajua kwamba kila

baada ya mwaka wazee hawa ikifika mwakani tayari wana miaka 70, wazee hawa ikifika baada ya miaka miwili wana miaka 70.

Kwa hivyo, litatupa wepesi sisi ndani ya miaka mitano kujua kwamba tuna wazee wangapi ambao watatimia umri ili kupata haki za msingi na wale ambao wanafariki basi kuwa na wepesi wa kuwaondosha katika *data base* ili kuweka umakini na matumizi bora ya fedha za serikali. Mhe. Mwenyekiti, hili lilikuwa langu la kwanza.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nizungumzie suala zima katika suala la taarifa ya kamati hili katika suala la ajira kwa vijana. Mhe. Mwenyekiti, wizara imeanda mipango mizuri katika suala zima la kuweza kuajiri vijana wale ambao hawatakuwa na muda wa kuweza kuajiriwa katika serikali hii kutokana na uchache wa nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba wizara sana hususan katika hii Idara ya Ajira kwa Vijana. Kwa bahati mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati hii katika awamu iliyopita tuliona mipango wa wizara lakini pia tukaona baadhi ya matatizo ambayo yanatokana na huu mfuko.

Kuna maeneo mawili nataka niyatolee mfano Mhe. Mwenyekiti. kulikuwa kuna eneo la shamba la Tunguu la mboga mboga, lakini pia kulikuwa kuna shamba la mradi la umwagiliaji maji kwa vijana wasomi maeneo ya Bweleo. Mhe. Mwenyekiti, maeneo haya kutokana nakutokufanya utafiti waliweza kuingiziwa fedha za serikali kwa muda mrefu, lakini mafanikio yakawa hayapatikani. Lengo langu Mhe. Mwenyekiti ni kumuomba Mhe. Waziri kabla ya kuvisaidia vikundi au kabla ya kutoa sadaka kwenye vikundi, ni kuanza kufanya utafiti kuangalia namna bora ya kuweza kuwasaidia. Kwa sababu tunapowapa pesa haraka haraka matokeo yake fedha inakwenda na maji faida haipatikani na kweli hatupati hasa lile lengo la serikali la kuwasaidia vijana. Maana lengo la serikali leo tuchukuwe vijana 100, keshokutwa tupate vijana 100 ili tuondoshe hasa lile wimbi la vijana la kutokua na ajira. Sasa kama tutakua tunazitoa fedha tu bila ya kuangalia uhalisia au bila kuwa na taarifa au bila ya kutoa elimu kwa vijana katika masuala mazima ya kujiajiri, basi hii ni hatari kwa wizara kuweza kupoteza fedha pasipo na mpangilio.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aangalie kabla ya kutoa fedha au kabla vikundi hivi hajavishajihisha kuangalia namna bora ya kuweza kuwapatia elimu na mafunzo mbali mbali ili pale ambapo serikali inaamua kutoa fedha zake, basi fedha ziweze kutumika kwa vizuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kukusaidia hapo katika taarifa ya kamati ni suala la ujasiriamali. Kama nilivyogusia katika suala la vijana Mhe. Mwenyekiti, bado inaonekana maeneo mengi matatizo haya yanaikumba wizara, ni kuanzisha jambo kwa haraka na matokeo yake tukakosa ufanisi na suala lile kuwa endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati mambo yanaanza ya ujasiriamali tulianza na mambo mbali mbali, na tulianza na masoko mengi sana. Kulikuwa na soko la Bwawani pale, tukaondoka Bwawani tukaja zetu kwenye Mnara Kisonge. Kisonge pale palianza na vurumai kubwa mashamiana mengi, lakini mwisho wa siku unakuta hali inakuwa inarudi nyuma, sasa unajiuliza tatizo liko wapi. Tunarudi nyuma kwa sababu kama tungekuwa tumeanzisha kikundi cha watu mia moja ya masoko yale kwa watu wengi, lakini baada ya muda mdogo unakuta masoko yale yanapwaya na yanakosa ufanisi.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kutafuta namna bora ya kuweza kujifunza kuwa wenzetu wanafanikiwa vipi hata yale masoko yanakuwa endelevu na wajasiriamali wanakuwa wanapata nguvu za ziada ili kuweza kujiokoa na masuala haya ya ajira isiyokuwa rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mambo makubwa ambapo tulipokuwa tukipita huko nyuma nilipokuwa mjumbe wa kamati, walikuwa wanazungumzia suala la soko. Suala la soko linahitaji wataalamu, mbinu na mikakati. Kwa hivyo, niiombe wizara kwamba wajaribu kutafuta mbinu mbadala ambazo zitawasaidia hawa wajasiriamali wetu kuweza kupata masoko kwa wepesi kwa zile biashara zao wanazozipeleka katika yale maeneo. Kwa sababu maeneo mengi au nchi nyingi zinakuwa zina mafanikio makubwa katika masuala mazima ya wajasiriamali katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingienataka niingie katika sekta ya michezo. Nimeona katika taarifa ya mwenyekiti hapa alipokuwa anazungumzia dhana nzima ya serikali kwa jumla, na dhana hii nimshukuru Mhe. Rais ndio aliyokuja nayo na akaipigia kelele sana katika suala zima la ujenzi wa viwanja vya mawilaya. Mhe. Mwenyekiti, mimi kama ingekuwa sio michango ya taarifa ya kamati basi ningemuuliza Mhe. Waziri, ili uwe mtendaji mzuri Mhe. Mwenyekiti, unahitaji ufuatiliaji. Maana yake kama leo ningemuuliza Mhe. Waziri hivi anavijua viwanja vinavyochezewa ligi la daraja la pili ngazi ya taifa vyote, na anaweza kunitajia kimoja baada ya kimoja, kwenye swali ingekuwa matatizo, maana yake nakusudia Mhe. Mwenyekiti, kusema kwamba kama utafuatilia viwanja vinavyochezewa ligi daraja la pili ngazi ya taifa, basi ningekuwa waziri ndio mimi ningesema hii ligi isichezwe.

Mhe. Mwenyekiti, ningesema isichezwe kwa sababu za msingi, ligi ya mzunguko haimalizi kama hujapata majeruhi ambao wanatokana na hali halisi ya uhalisia wa viwanja. Mhe. Mwenyekiti, viwanja hivi havichezeki, na ninamuomba Mhe. Waziri ajaribu kuvipitia hivi viwanja. Kuna kiwanja cha Mwanakombo, Bumbwisudi, Maungani, Ndijani hivi ndio viwanja ambavyo vimechezewa ligi daraja la pili ngazi ya taifa, havistahiki, havina ubora na havifai kabisa kuchezewa ligi. Sasa nilikuwa najaribu kumuelezea ile hali halisia na sio kama ubora wa kucheza tu, lakini hata ule ubora wa kimichezo kwa sifa ya viwanja havina. Leo tunakimbilia *CAF* huko, *CAF* tunakwenda na utaratibu, kwanza hayo maeneo yenyewe pia hayastahiki, usikimbilie uanachama wakati michezo yenyewe haina ubora katika kuendesha.

Kwa hivyo, sasa nimuombe Mhe. Waziri, najua serikali ina dhamira nzuri sana na ndio maana ikaleta jambo hili la kujenga viwanja vya mawilaya, atafute jitihada mbadala ya kuweza kusaidia kutafuta namna gani ya kuweza kupata fedha ili viwanja hivi viweze kujengwa na baadae kuondosha matatizo kwa vijana wetu ambao wanategemea viwanja hivi. Sio lazima tukaanza na *presure* ya kujenga maeneo yote mpaka majukwaa, kutia mataa na maeneo mengine. Japo *pitch* tu tukaanza kiwanja kimoja kimoja, tukasema tunaanza wilaya hii tunawatengenezea *pitch* iliyokuwa nzuri, magoli yanakaa katika *standard*, uwanja unakuwa umetimia mita mia moja. Lakini viwanja mita mia moja vyengine havitimii, magoli utakuta la Kaskazini na la Kusini, hili liko juu na hili jengine liko chini, alimradi kwa kweli hatujajipanga. Sasa suala hili namuomba Mhe. Waziri, namuamini kutokana na umahiri na uhodari wake, atafute njia ya haraka na ya mbadala kuweza kuvisaidia viwanja hivi.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, nakuja katika suala hilo hilo la sekta ya michezo, kwa sababu nataka nimsaidie Mhe. Waziri kwa sababu ameanza na kazi, na tumeona jana ni namna gani anavyoanza kuboresha masuala ya michezo katika nchi yetu hii. Kwa hivyo, kama tuna dawa ya michezo basi tuna haja ya kumsaidia ili sekta hii iweze kupata maendeleo kwa haraka katika nchi yetu.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la kurejesha hadhi ya michezo mashuleni. Mhe. Mwenyekiti, michezo hii hatuipati kwenye vilabu tu, michezo inaanzia mashuleni, nguvu zimepungua haionekani taswira yake, tumejifunza sana huko nyuma tunakotoka, tumewapata wachezaji mahiri kutoka mashuleni, tuliwapata kina Ubwa Makame, Dua Said, Omar Kingi. Hawa walikuwa kweli wanafunzi wa Haile Sellasie, wakati huo mashindano yalikuwa yana nguvu, lakini mashindano sasa hivi yanakwenda tu alimuradi yafanyike yamalizike

basi, lakini ule umahiri hasa wa mashindano katika mashule umekufa, na mtoto unaambiwa umlee tangu mchanga, sijui udogo uufinyange ungali mbichi.

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniwashia ishara ya kumaliza. Mimi nimemaliza najua nakwenda kwa wakati Mhe. Mwenyekiti, sichukui wakati wako wala siumalizi. Naunga mkono hoja hii ya Mwenyekiti mahiri Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata, nawaomba na wajumbe wenzangu tuunge mkono hoja hii. Lakini kama nilivyoanza kusema mwanzo lazima tunapochangia tuangalie mustakabali wa nchi yetu, mustakabali wa sheria na kanuni na katiba nchi yetu inavyotuongoza, tusianze mivutano ya kutaka kuchukua fursa za mahakama na kuzileta ndani ya Baraza, tukaanza kuhukumu kabla kesi haijahukumiwa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mnadhimu. Kulingana na muda wetu uliobaki atakuwa ni mchangiaji wa mwisho Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata.

Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata: Bahati mbaya mimi ni Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya kamati Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Awali ya yote napenda sana kwanza kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kweli natangaza kwamba Wazanzibari tumepata bahari kubwa sana ya kuwa na kiongozi msikivu, mwenye busara na hekima, busara zake, usikivu wake na hekima zake tunaona Zanzibar tunavyopiga hatua siku hadi siku, napenda sana kumpongeza Mhe. Rais kwa hilo. *(Makofi)*

Baada ya kumpongeza Mhe. Rais niende katika ripoti. Kwanza naipongeza sana kamati Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kwa ripoti nzuri kabisa walioleta na ikawa muda huu kidogo inaleta mzozo tuichangie au tusiichangie iende au isiende, na hatimaye kwa busara zako ukatupa fursa ya kuchangia.

Kwa hivyo, mimi nakwenda kuchangia moja kwa moja katika Shirika la Utangazaji ZBC, ambapo ni katika ukurasa wa nne. Shirika la Utangazaji (ZBC). Najua imefanya mabadiliko makubwa sana na inapiga hatua kubwa sana katika hicho, inafaa tuwapongeze kuanzia Mhe. Waziri na watendaji wake, katibu na hata wale wakurugenzi wa ZBC, namuomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu waje kufanikiwa katika lengo lao, wana azma nje ya kuibadilisha ZBC. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hongera sana na watendaji wako.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mabadiliko hayo kuna changamoto ndogo ndogo ambazo zinaweza kurekebishika. Ripoti tumeisoma hapa, tunaona kwamba ina uhaba wa usafiri, vitendea kazi havikidhi. Lakini hata hivi juzi tu kuna baadhi ya vijana muda mrefu walikuwa wamejitolea pale ZBC, lakini sijui katika kuutengeneza muundo mpya imethubutu kuwasimamisha. Ni kweli nafikiri kidogo hawakutendea haki katika hicho, kwa sababu wale vijana wameshafanyakazi pale kwa muda wa miaka minane au zaidi ya hapo au chini ya hapo walikua na lengo zuri tu katika kuisaidia nchi hii, hata hao walioajiriwa walitoka mule mule wengine. Tulikuwa nao wengine kina Denis Bilal walianza kwa kujitolea tu na hatimaye leo hii wamekua nafikiri waajiriwa wa ZBC. Nafikiri pale kidogo serikali au ile taasisi ya ZBC ilikuwa iangalie kwa jicho la huruma kuwaangalia namna gani wale vijana wataweza kuendelea nao.

Niende katika ukurasa wa 7 kuhusu magazeti. Tunajua kwamba Zanzibar tuna gazeti moja tu la Zanzibar Leo, pamoja na maboresho mbali mbali yanayopigiwa kelele yanaboresheka, lakini hata juzi tulipokuwa tukichangia Ofisi za Viongozi Wakuu, tulizungumza kwamba kadhia nzima ya magazeti yale kuchapishwa Tanzania Bara, wakati tuliambiwa kwamba Zanzibar kuna mtambo wa kisasa kabisa na wenye uwezo. Sasa ningeomba sana Mhe. Waziri na hili uliangalie haraka iwezekanavyo, ili tuondokane na kulipa pesa nyingi kule Tanzania Bara wakati *press* ya taifa iko hapa ya uchapaji, ambayo nathubutu kusema kwamba inayo uwezo wa kuchapisha magazeti yale. Lakini kama kuna matatizo watendaji hawapo, basi muombe ruhusa serikalini ili muajiri watu wenye sifa wafanye ile kazi, ili zile fedha ziwe zinazunguka katika nchi yetu hii au katika serikali yetu kuliko zile pesa kwenda sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa wakati Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alitoa tamko kwamba hatoruhusu au haitokuwa tayari serikali kulipa pesa ya uchapaji nje ya Zanzibar. Sasa sijui kama mpaka dakika hii tunachapisha magazeti yetu huko Tanzania Bara, wakati *press* tunayo hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 14 Baraza la Michezo *BTMZ*. Naomba kulipongeza sana Baraza la Michezo, pamoja na changamoto mbali mbali wanazozipata kwa sababu moja kwa moja wanahudumia vijana, vijana wana jazba zao. Unajua changamoto nyingi wamezipata, hususan mama yangu Mwenyekiti pale kapata malalamiko mengi sana kwa kupitia ngazi mbali mbali kwa watendaji wa wilaya wa chini na hata hiyo *ZFA* taifa yake.

Lakini ningeomba tu kuuiliza *BTMZ* sijui imejipangaje katika kuanzisha mashindano ya *FA* kwa ajili ya mpira wa miguu, tunaona nchi nyingi sana duniani, hata huko tunakokopia baada ya ligi ya nchi, kunakuwa kuna ligi ndogo ambayo inashirikisha vilabu vya ngazi mbali mbali, kuanzia ngazi ya chini kabisa kama ngazi ya nne, daraja la tatu ya kanda na hatimaye *primer*. Sijui hili kwa upande wa *BTMZ* imewapa maagizo kiasi gani ZFA ili kukaa na kuona kwamba wanaanzisha mashindano haya ya FA, kwa sababu mashindano ya FA tunajua ni mashindano ya nchi, kila mtu ana uwezo wa kuonesha kipaji chake pale, ningeomba sana na hilo Mhe. Waziri kwamba lazima mashindano ya FA yawepo. Nakumbuka tulianza kufungwa hapo nyuma mara moja mara mbili, lakini mpaka dakika hii mashindano yale hayapo tena. Kwa hivyo, ningeomba sana kiwanja hicho hicho tulichokuwanacho cha amani tukacheza mara mbili au mara tatu. Hivyo viwanja vyengine mwenzangu aliyezungumza habari ya viwanja, lakini hakuna ubaya. Mtu anashona koti kwa mujibu wa kitambaa chake alichokua nacho. Viwanja vyetu tunavyo hivyo hivyo, basi yale mashindano ya FA ningeomba sana yaendelee.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa 22, lilizungumzwa suala la wazee, kwa sababu wazee ndio waliotufikisha hapa tulipo, nguvu zao, uwezo wao na hekima zao hatimaye Zanzibar imefikia hapa ilipo kwa kupitia kwa wazee. Wazee wetu wale sasa hivi wapo katika nyumba mbali mbali kama Limbani, Sebleni na Welezo. Nashangaa sana kuona hii ripoti ya humu kuhusu hawa wazee. Wazee walioandikwa humu katika kukudhi mahitajio yao au huduma zao, inatofauti kubwa sana. Unaambiwa Limbani kuna wazee 8 wanatumia milioni moja na laki tano, wazee wako Sebleni 31 wanatumia milioni 7.5, na wazee wa Welezo wako 34 wanatumia milioni 5. Kulikoni hawa 34 wako wengi lakini wanatumia pesa kidogo kuliko hawa wazee waliokuwa kidogo wanatumia pesa nyingi. Sijui kuna jibu gani la serikali, hapa nafikiri kuna watu ambao sio wema au hawawatakii mema kuwatunza wazee wetu lazima wanafanya mambo yao ambayo yanapigwa vita na kila mmoja. Nathubutu kusema kama kuna kitu cha ubadhirifu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani wazee 34 watumie milioni 5 kwa mwezi, halafu wazee 31 watumie milioni 7.5. Ukiangalia chakula chenyewe kwa siku nzima mlo wao mmoja kwa siku walipwe elfu 80,000, ukienda mule chakula chenyewe wanapigwa pembe au haragwe, jamani tusemeni ukweli katika hiki, ni lazima tuangalie hawa wazee wetu wanahitaji sasa hivi watunzwe vizuri, wapate matunda, mboga mboga na samaki ili na wao waone kwamba nguvu zao walizozitumia katika nchi hii wanufaike nazo. Lakini haiwezekani leo unakwenda na bajeti ya milioni 7.5 kwa mwezi, ukipiga hesabu haifiki hata milioni 4 kwa mwezi kwa mlo wa shilingi 80,000. Jamani tunafanya nini,

nathubutu kusema maneno kama haya ni lazima tuwe na uchungu, wale wazee wetu wamehangaika sana katika nchi hii, kuna wengine mule walikuwa walimu wetu zamani, wazee wetu walinzi wetu. Sasa leo wazee pale unamuamsha asubuhi unampa chai ya mkandaa na boflo halina hata siagi, au kapata siagi, unampa mchana ubwabwa na haragwe, tena wali wenyewe mapembe, jamani tuwaonee huruma sana wazee. Usiku chai ya mkandaa na mkate mwisho wa mwenzi mnatuambia milioni 7.8 ni pesa nyingi sana ambazo hazistahiki yaani kuwemo katika kadhia hii. Kwa hivyo, ningeomba tu hilo suala lichukuliwe kimakini. Hata masuala ya makazi yao, tumekwenda Limbani kule, jengo limekarabatiwa utaambiwa milioni 100 haifiki, mabati saba yaliyotiwa mapya, imepigwa plasta kwa pesa hizo jamani tunafanya nini tuwe na uchungu kidogo na nchi hii. Ifike wakati ukweli ubakie ukweli bwana, lazima tuambizane katika hicho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikiendelea mbele vile vile naomba ninukuu katiba ya Chama cha Mapinduzi, Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nanukuu ibara ya 18 ni mwiko kwa kiongozi, naomba niseme;

Ibara ya 18

"Ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume ya lengo lililokusudiwa na madaraka hayo".

Nimethubutu kusema hayo ili katiba ya chama inanisaidia kwa kadhia nzima iliyosomwa, japo suala lipo mahakamani. Lakini kuna mambo mengine ambayo yalizungumzwa hapa yalikuwa hayapo mahakamani yapo katika kamati.

Kipengele cha mwisho kamati imesisitiza hapa, kamati imesikitishwa na hatua iliyochukuliwa na wizara kumtorosha mtoto Ibarahim na kumpeleka kusikojulikana, kitendo ambacho kilitarajiwa kifanywe na mtu mwengine, na sio wizara inayosimamia maslahi mema ya watoto na inataka wizara kutorudia tena kitendo ambacho kinakiuka sheria.

Mmetuambia kesi iko mahakamani, leo nyuma yake mtoto anatoroshwa, ina maana nani aliyeingia mahakamani. Kama mahakama, tuliacha Mahakama ichukuwe nafasi yake, kesi izungumzwe mahakamani na itolewe hukumu mahakamani. Lakini kesi haijatajwa ndio kwanza imepokelewa tu mahakamani huku mtoto unamtorosha unampa bwana Mkaka. Sasa nini unafanya, tayari unamkosesha mtoto haki zake za msingi, kama ilimuhoji mtoto na akasema kwamba anataka kukaa kwa bibi yake ili apate kusoma shule na apate elimu ya

madrasa. Jamani haya ndio ule uharamu wa miko ya viongozi. Tulitamka kwamba kiongozi katumia madaraka yake kwa maslahi yake mwenyewe ambayo ni kosa, hata katiba yetu ya chama inatuelekeza hivyo. Sasa kama kiongozi wa chama cha mapinduzi anafanya mambo kama hayo na yeye ni kiongozi ambaye ni kiyoo, anatupeleka wapi sisi huko nyuma, inasikitisha sana na mimi nimesikitika sana katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante muda wetu umemaliza, naomba niahirishe kikao hiki hadi jioni saa 11:00 *Inshaallah*. Ahsanteni.

(Saa 7:00 mchana Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji wetu ambaye alikuwa hajamaliza Mhe. Abdalla Maulid Diwani nitakupa dakika tano za mwisho ya kumalizia. Baada ya Mhe. Diwani atafuata Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunimalizia dakika zangu zilizobakia nakushukuru sana.

Wakati nikiendelea na mchango wangu nilifikia katika ukurasa wa 22 ambapo ilikuwa suala la wazee nikaruka pale nikaenda Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto, nimesoma kanuni ya Chama, mwenendo mzima na baadae kufikia mbele hili suala la kuhamishwa Bi. Saada Abubakar.

Nathubutu kusema kwamba inasikitisha sana kuona kwamba mtu aliyesaidiana na Kamati ya Baraza la Wawakilishi kutoa maelekezo mazuri sana ya kina bila ya kuficha neno akaonekana kama mchochezi na baada ya muda akahamishwa katika sehemu husika kule. Kwa kweli hatujamtendea haki, pamoja na magizo ya Kamati naiomba sana Wizara ya Wanawake na Watoto iliangalie kwa jicho la kawaida ambalo jee, kweli alistahiki hii adhabu huyu mtu au ndio yale ambayo tuliyazungumza katika Katiba yetu ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 18, naomba niisome tena ili nikazie hapa.

"Ni mwiko kiongozi kutumia madaraka aliyopewa ama kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo aliyekusudiwa"

Inongozwa na katiba ya Chama cha Mapinduzi tayari haimpi mtu fursa hiyo mtu kufanya mambo kwa hamu zake ama shauku aliyokuwa nayo, mambo mengi yanakwenda katika sheria na taratibu, nilitaka niseme hayo kwa kweli huyu mama kwa mujibu wa mustakbali hajatendewa haki kwa sababu ya kushirikiana na kamati ile ambayo Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi au Kamati ya Kudumu ya Uwezeshaji, Habari, Utalii na Mifugo. Kwa kweli lazima tumuangalie na nitamuomba sana Mwenyekiti wa Kamati hii alishupalie lile suala na alipigie kifua hasa kwamba lazima yule mama arudishwe kwenye sehemu yake pale kama hajavunja sheria wala kanuni za taasisi ile. Vyenginevyo kwa hamu tukumuondosha kwa sababu amewapa ukweli watu wa kamati ikaonekana kwamba ka-*base* pamoja na kamati, ina maana hajatendewa haki.

Basi ilikuwa nisipoteze muda sana nichangie hapo tu niwaachie wenzangu nakwambia ahsante sana naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia zote zilizokuwepo.

Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashkuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata fursa ya kuchangia kidogo.

Mimi Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze viongozi wote, Mawaziri wetu, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na wote waliokuwa wamechangia kwa hatua moja ama nyengine, au Maafisa Wadhamini wetu walioko Pemba pia nao tuwashukuru sana kwa kazi kubwa wanazozifanya. Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze kwa dhati shukurani zangu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa hali ambayo anafanya jitihada zake za kuendeleza maendeleo ya watu wa Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nikija kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nilikuwa natoa kama wazo kwamba nimeangalia katika kipengele humu, suala hili la mambo yetu ya kale ambayo tunayo, ni kwamba mimi nafikiria tu kwamba bado kuna haja kwa Wizara kutafuta zaidi mambo ya kale ambayo yamejificha katika historia ambayo naamini kwamba mengine bado. Sasa ningeshauri kwamba Waziri akatangaza hasa ikiwezekana kwamba wale watu ambao wana rekodi au wana jambo katika vijiji vyao havijatambulika, basi wakaweza kuvifikisha katika maeneo husika, lakini pia kama kutakuwa na

mtu ambaye anaijua historia basi ni bora akarikodiwa ili historia ile isiweze kuondoka, kwa sababu nahisi sasa hivi muda umekuwa mdogo, mtu akifika miaka sitini anakufa historia zitakuwa hatuwezi kuja kuzipata. Sasa ningeshauri sana kwamba suala hili lifanyiwe haraka ili na hili kwamba halitaki gharama kubwa, ni *just* kutangaza na kuweza kuwatafuta wale watu ambao wana historia ambazo zimejificha.

Mimi humu katika kusoma historia zote nimeziangalia kule kwetu upande wa Chake Chake upande wa Birikau na Ndagoni kuna historia ambazo sijaziona humu. Kuna kaburi la mwanamwari mimi sijaona hata siku moja huku, nimesoma vitabu vyote Kaburi la Mwanamwari sijaliona. Sasa ambayo ni historia kubwa sana iliyofanyika kule. Ningeshauri Waziri akazitafuta hizi na kuziweka katika rekodi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye *Digital* mambo yetu haya katika Wizara ya Habari bado Wizara hii katika kupitia sehemu yake ya Shirika la Habari la *ZBC* bado ni mtihani, bado ni kitandawili, bado tunazunguruka sana. Mhe. Naibu Spika, tulilitolea maelekezo zaidi Shirika letu hili tukalipa nguvu ili liwe ni Shirika ambalo linaweza likajiendeza vizuri na likasukuma msukumo wa habari zake.

Mhe. Naibu Spika, hichi chombo ni chombo cha huduma, ukiachia biashara, Serikali ya Zanzibar na watu wake wema na watu wote wanaoiombea dua Zanzibar basi masikio yao ili kupata kitu ambacho ni cha uhakika, basi lazima akuulize imetoka *ZBC* au Redio Zanzibar. Vyenginevyo vyovyote vinaweza kupotosha. Sasa ningelishauri sana Shirika akajua hilo kwamba sisi upande wa Zanzibar watu wema na watu wote wanaoiombea wema Zanzibar, Shirika lile ndio tunalisikiliza kitu kikitoka pale ndio kinakuwa cha uhakika na ukweli. Sasa wasifanye masihara hata kidogo, watutafutie vyombo ambavyo vitakwenda sawa na wakati lakini pia kiweze kupatikana popote, ukenda Kengeja kipo, ukenda Konde kipo, Micheweni kiko inakuwaje unapata Mjini/Magharibi tu. Sasa Mhe. Naibu Spika, ningeshangaa kwamba chombo cha zamani kikongwe lakini bado hatua zake za kusikilikana hazijafika mbali. Sasa nashauri sana ikawa hiyo *Digital* ambayo sasa hivi tunakwenda katika mtindo wa *Digital*, usije ukawa na mbwembwe, usiwe ukawa na *catalogue*, huo ukiufungua tu basi habari tunazipata. Ningeshauri sana iwe hivyo kutokana na matatizo tunayoyaona kwamba lazima habari zake nzuri tuzipatie pale.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine tuagalie hasa hata hili Shirika la Habari ambalo ni dogo maskini, bado Wizara wanalikopa. Mhe. Waziri wa Fedha ungefanya kama Waziri wa Muungano alipoona Shirika lake la Umeme

linakufa kule kwa madeni ya Serikali na mengine, ameamua kuchukua jitihada za kukata pesa za umeme zote kuzipeleka kwenye mashirika husika. Ningemuomba Waziri wa Fedha hapa haya mambo mengine Shirika la Habari na Mashirika mengine basi fedha zao zikapelekwa moja kwa moja kule kwenye Wizara husika kuliko kumpitishia Waziri kwanza akatizama hali halisi ilivyo na kama mambo magumu ndio akamsahau ikawa tena ni kitandawili.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimeona kwenye taarifa humu kwamba *ZRB* nayo ilifanya mambo ya kwenda kumfungia umeme, mimi sifikirii kama kilikuwa kitu chema, kilikuwa sio kitu kizuri. Kwa sababu Shirika la Umeme ni Shirika ambalo linatoa huduma ambalo ukimfungia yule hunifungii mimi unawafungia watu wote wasipate huduma na yeye umeme akikasirika akifunga kompyuta itawaka, sasa itakuwa tunaonyeshana makarama. Sasa ningeshauri muamuzi wa huyu ni Waziri wa Fedha, maana yake hapa tena wamesema hatua za kudai washachoka labda nao wafanye mengine sasa tusifike huko. Kwa hivyo ningeshauri Waziri wa Fedha wewe ukiona kwamba kuna ulakini wewe tafuta mpango pesa zao walipe hawa ili tuweze kwenda na wakati.(*Makofi*)

Lakini la tatu Mhe. Naibu Spika, nanukuu tu Mhe. Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kusema kwamba, "ukitaka kula lazima na wewe uliwe". Sasa Mhe. Naibu Spika, hakutegemea hilo kulisema wazi lakini alisema kwamba ukitangaza au ukijitangaza sana, basi na mapato yatakuwa makubwa. Mhe. Naibu Spika, bado Wizara yetu ya Habari na hata hizo redio zake *ZBC,* mimi sijaona hata gari moja limetiwa ata ma-*slogan* tu ya *ZBC,* maana yake hiyo gari yenyewe kama inajificha na matangazo mengine. Kwa hivyo ningeshauri kwamba hili Shirika likajitangaza. Kule Pemba unaweza ukamtafuta mtangazaji wa *ZBC* hajulikani, hawana usafiri, hawako *active*, maana yake hawana nyenzo. Sasa Mhe. Naibu Spika, habari watazipataje.(*Makofi*).

Kwa hivyo ningeshauri sana tukajitahidi kutafuta nyenzo na kujitangaza zaidi. Nimeona humu kwamba bado tuna wakala yuko India anatutangaza, mimi sifahamu Wakala wa India anatusaidia nini. Maana yake hawa Wahindi kuja huku hawaji kuja kutalii. Sasa hili kidogo nilikuwa sijalifahamu vizuri wakala wa India kule anafanya nini kututangaza. Kwa hivyo ningeshauri Waziri atizame tu kwamba kuna haja ya kuendelea naye tuendelee naye, hakuna haja tusipoteze mambo tuangalie hali halisi itakavyokuwa.

Mhe. Naibu Spika, hapa mumesema historia ya Mkamandume. Mkamandume ukimtafuta mtu yeyote sasa hivi historia yake hakupi kwa sababu haipo. Huyu Mkamandume alikuwa na historia kuanzia makazi yake mpaka mwenyewe, yeye mwenyewe historia. Sasa hakuna mtu wa kurekodiwa hata mmoja

akaeleza matatizo ya Mkamandume yalikuwaje, mtawala huyu anapotea hivi hivi, majengo yake yanapotea hivi hivi kule Pujini kule hata mtu haendi. Leo tutakuja kumtafuta tena baadae tukiulizwa Mkamandume hata ile asili yake haipo. Sasa ningeshauri mambo haya yaende.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye michazo. Katika jambo ambalo linarudisha nyuma ni michezo ni Baraza letu la Michezo. Mhe. Naibu Spika, maamuzi yao yanakuwa ya mtu anavyoona mwenyewe, tunaziua timu watu wanakasirika, marifarii wanaua timu hata ukenda Baraza la Michezo halisaidii kitu, matokeo yake timu zinakufa kutokana na kuchoka na yale madhila ambayo michezo yetu inakufa. Sasa ningeshauri sana kwamba hali halisi tunayoiona basi isiwe ya kuwa tunaifumbia macho. Mhe. Naibu Spika, mambo haya yanatuuliza michezo sana. Sasa baadae tuangalie mustakbali ambao unasikia zogo saa zote hapo Yanga, Simba tunafurahia timu za watu. Miaka ya nyuma hapa Small Simba na Malindi zilikuwa kidedea barabara hazipitiki siku ya mechi leo ziko wapi, tunashangiria Simba na Yanga sijui na Manchester na wapi, kwetu pamekufa.(*Makofi*).

Sasa kwanza wewe Mhe. Waziri wa Elimu, kwanza rudisha timu zako usishabikie Simba rudisha timu zako Zanzibar. Hizi timu za hapa zifanye kila jitihada Zanzibar hapa. Malindi ishakwenda kuchukua kombe Mwanza tumeyasahau hayo. Sasa leo tunakaa tu hapa Waheshimiwa mara Simba mara Yanga nini, hamna Malindi, hamna timu gani mnazishangiria timu za watu na nyie ndio wa kuonesha mfano waheshimiwa. Tuchangie zile timu zije juu, tupige *donotion* kidogo tuchangie Waheshimiwa. Kwa hivyo nilikuwa nashauri tuzifanye Mhe. Waziri wewe kidogo una nafasi ya kuzivuta vuta angalau tujue tunafika wapi hili tuangalie.(*Makofi*).

Sasa Mhe. Naibu Spika, niache huko kwenye michezo naiende kwenye hii Afisi ya Wanawake na Watoto, ofisi hii naipenda sana. Kwa sababu mimi bwana kuonewa mtoto na mama sipendi, sipendi kabisa. Sasa Mhe. Naibu Spika, jambo la kwanza niseme kwamba malalamiko yamekuwa mengi, suala la wafanyakazi ama mahotelini ama maeneo mengine tumezidiwa na wageni, wala hakuna kiwango hata kimoja cha kumlazimisha mwekezaji kwamba lazima utachukua watu wangapi kwanza, halafu chukua wageni kama taaluma hiyo haina. Lakini Mhe. Naibu Spika, ajira zetu zimekwenda ovyo ovyo. Mimi nataka nikwambie hapa ukipiga msako hapa basi kuna watu wanaka hapa bila ya kibali, watu wanapitishana tu. Kwa hivyo tunapigishana kelele ajira hatuna tunapanua, halafu tunaleta watu wanachukua nafasi. Hivyo ningeshauri sana Mhe. Waziri ukaweza kuangalia hali halisi ya hili suala la wafanyakazi ambalo

ukitaka kutizama lete kibali chako cha kufanyia kazi utakamata tele huko, watu wanajikalia tu sasa hivi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye wazee ambapo Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa nia njema amefanya kuwasaidia wazee wa Zanzibar wanaofika miaka sabini wote, marika yote, jinsi yote kike kiume, aliyefanya kazi, asiyefanya kazi. Hili ni moja la kusifiwa sana na dunia iliwahi kumsifu sana katika vyombo vya habari. Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa ya Kamati inaonekana huu mfuko unakwenda shaghala baghala. Kwanza haurudishi matokeo kila siku ni wale wale, aliyekufa hayumo wala anayefanya vipi hayumo. Huu Mfuko utizamwe, anayekufa nani atolewe apate mwengine wa kusonga mbele, lakini huu unafika unaendelea tu lakini kufa hakuna na kila siku watu wanakufa. Lazima huu Mfuko utizamwe kweli kweli, watu hapa watacheza kweli kweli, ndio hiyo ukisikia mishahara hewa mmoja ni huo. Kw hivyo ningeomba utizamwe vizuri ili ulengwa ukubalike.(*Makofi*).

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kutokana na matatzo ya wazee wetu. Mhe. Naibu Spika, watu walipotaka kuandikishwa vile vitambulisho vya Mzanzibari, alikuwa akikwambia wewe niandike tu hata arubaini, thalathini ati mtu kapinda hivi kaandika miaka 40 hee!, ndivyo vilivyokuwa vikitizamwa vitambulisho kwa sababu mtu alikuwa akikisia tu akimuandikia tu anavyotaka, alikuwa hajui maana na faida yake, ukifanya sensa sasa hivi watu waliokuwa hawafaidiki na Mfuko huo inawezekana hawa walioko kidogo kuliko wanaopata. Sasa watu wanalalamika lakini bila ya sheria, mimi sijui toka azaliwe nani lakini Mheshimiwa toka azaliwe nani, lakini kauli ya kitambulisho chako kinakutaka wewe usilipwe. Kuna watu wengine waliowahi ni wadogo wadogo wana miaka 70, utajua kwamba huyu ndio kwanza ana miaka 60 lakini ndiyo mambo yalivyokwenda. Sasa ningemshauri Waziri ukajitahidi kulitazama hili neno ukatumia Masheha, ukatumia Mabalozi ukafanya ziara hasa yako mwenyewe, wale wazee wanaojikisia ili na Mfuko huu nao uweze kuwafikia kwa nia njema ufanye vikao uende kule Pemba kwenye mashamba huko Kiwengwa, uwatafute hao wazee kwa sababu hii ni haki yao, hii ni sadaka ya Dkt. Shein itakwenda kumfaa mbele ya haki huko labda ningesema kwa hali hiyo sawa.

Lakini nije kwenye suala gumu sana maana yake tushaliwacha limeshakuwa mbali sana. Mhe. Naibu Spika, suala la vijana *under 18* bado ni tatizo zito sana hili pamoja na kwamba Waziri wa Habari naye hayumo katika Wanawake na Watoto ingawa yumo lakini atusaidie kutangaza sana. Mheshimiwa watoto wameshatushinda, mzee hawawezi, Serikali imemuachia mzee na mzee hawawezi taifa linapotea. Sijui huku nyuma kulikuwa na vigezo gani maana siku moja mlinijibu hapa mkanambia kwamba hakuna Sheria ya Mtoto kulala

saa mbili au kufanyiwa hivi au mavazi ya hivi. Lakini hebu tizameni huyo aliyekuwa akifanya mwanzo akiwapiga bakora watoto na kuwatia ndani, yeye alitumia sheria gani angalau tupunguze hili wimbi litakalopotea.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda madisko wewe kaa hapo usiku kuanzia milango ya saa nne za usiku, simama tu, pikipiki ina watu sita, watoto wadogo wadogo, halafu leo uje umng'ang'anie mtu umwambie kabaka wakati yeye mwenyewe anataka kubakwa. Maana yake anamlazimisha mtoto, anamlazimisha mtu kwa kwa hali aliyovaa nguo zile umri alionao na matatizo yaliyompata, hii ni dunia maumbile hatuwezi tukayaepuka, Mhe. Naibu Spika, tukae tukubali maumbile hatuwezi tukayaepuka, sisi wenyewe tunasema akifika mtu miaka ishirini hujampa mke huyo? Unamwambia nimpe mke wa nini? si kwa sababu kuna jambo na jambo lile liko wazi sasa hivi matatizo haya yanatufika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakupa hadithi moja ndogo tu naomba uniruhusu ya Kidini. "Kulikuwa na mtu ambaye katika Mitume enzi hizo basi akaomba kwamba huyu Bilisi wa nini…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa dakika zako zimekwisha. Naona sasa unaanza kutoa hotuba, unatoa hadithi, dakika zako zimekwisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa basi naomba, basi Mheshimiwa nakushukuru sana naunga mkono hoja Mheshimiwa.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnajua na mimi mnanipa *headache* sana, hapa nina watu 27 wanataka kuchangia na tunataka tumalize ripoti hii leo kwa sababu naomba mkumbuke sana ripoti moja siku moja.

Kwa hivyo ikiwa kama tutaendelea kuzungumza kwanza tutarudia vitu vile kwa vile, hilo moja. Lakini kila mtu akitaka muda wa ziada haupo. Sasa nakuombeni sana hapa inabidi nimuombe Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tukubaliane dakika kumi kumi wale ambao watafanikiwa kuchangia kwa maneno watachangia kwa maneno, wengine watachangia kwa maandishi au laa mimi niko tayari hapa kukaa mpaka saa tano ya usiku. (*Makofi*)

Wajumbe: Ndiyo, ndiyo, ndiyo! (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Lakini muda tuupunguze ni dakika kumi kumi nakuombeni sana, namuomba Mhe. Waziri akubali hilo ehee! kwa sababu

nyinyi mnatoka, mimi niko hapa nimekaa tu, nyinyi mnaranda. Mhe. Waziri nakuomba.

KUWEKA KANUNI YA MUDA KANDO

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli iliyokuwepo mbele yetu bado ina wajumbe wengi kuchangia na naamini itafika muda wa kumaliza bado wachangiaji watakuwepo. Hivyo niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tupate nafasi ya kumalizia ripoti hii iliyokuwepo mbele yetu na wachangiaji wapate nafasi ya kutoa mchango wao. Baada ya maelezo hayo naomba sasa niwaombe Wajumbe tuweke muda wa kanuni kando ili tuweze kuchukua muda zaidi wa kumaliza shughuli iliyombele yetu. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa nawauliza Mheshimiwa ametoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Tunaendelea.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed Said na atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif na baada ya hapo atakuja Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Simai Muhammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hii ripoti yetu leo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2016/17.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze pia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kuwashukuru wananchi wangu wa jimbo la Tunguu ambao wao pia mimi nikiwepo hapa kama msemaji wao na mtetezi wao. Lakini pia nimshukuru Mhe. Spika, pamoja na wewe Naibu Spika kwa Baraza letu la Wawakilishi kwa kutujali kutupatia fursa pamoja na watendaji wote na kumkubalia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuja kukaa na sisi kuweza kutusikia mawazo yetu, fikra zetu kwa maslahi ya wananchi wetu pamoja na kujenga uchumi wetu imara kwa miaka ya mbele.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme hii ripoti kwa kweli ni nzuri nimeipitia niwapongeze viongozi wote walioshiriki katika kuandaa ripoti hii. Na ningependa nianze kwa kuchangia juu ya Ofisi ya *ZBC* Dar-es-Salaam. Ukisoma katika ukurasa namba 5 (v) inasema hivi

"Kukosa mashirikiano kutoka kwa baadhi ya taasisi za Serikali za Muungano hali hii husababisha na baadhi ya watendaji wa Taasisi za Muungano ambao huwachukulia watumishi wa shirika waliopo Dar es Salaam kama sio watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar"

Mhe. Naibu Spika, mimi nipo katika Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na tulipata nafasi ya kufanya ziara katika Ofisi hii. Moja ambalo tulilolikuta pale pia mbali ya changamoto zilizotajwa katika ripoti hii, lakini pia watendaji katika Ofisi ile inayoshughulikia masuala ya Uratibu wote ambao wanashirikiana pamoja na *ZBC, studio* yao kwa kweli mazingira yake bado ni duni, lakini pia watendaji wanatumia fedha zao za mfukoni kufanya kazi za serikali hadi kufika wanaidai serikali.

Mimi ningemuomba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili Mhe. Mohammed Aboud, suala hili kwa kweli halistahiki mtendaji wa serikali kuikopesha serikali. Kama sikosei wanaidai serikali karibu shilingi milioni 18 pale Ofisi ya Dar-es-Salaam ya Uratibu na hawa *ZBC* wanashirikiana kwa pamoja. Kwa kweli nimesononeka sana pamoja na Wajumbe wenzetu tulipokwenda siku ile wakatwambia fedha zao hizo ni za muda mrefu. Ningeomba kwenye ripoti hii naunganisha kabisa kwamba wafuatilie.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ni *ZBC* au *Television Zanzibar*. *TV* yetu kukosekana au kutoonekana katika *DSTV* ambayo umiliki wao ni *multichoice Africa* au Tanzania. *DSTV* ni *Digital Satellite Television* ambayo huduma hii unaweza kuipata kwa nchi zote duniani na maeneo tofauti hapa Barazani Afrika. Unapoonekana pale maana yake wewe tayari unapata kuitangaza nchi na mambo mengi. *ZBC* imekosekana kuonekana kwenye *DSTV* muda mrefu na mawazo yangu hapa niliyatoa mwaka jana wakati wa bajeti na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili pamoja na Waziri mwenyewe husika wa Habari alinisikia.

Sababu kubwa niliyofanya utafiti nilipata kuongea na watu tofauti. Moja ya sababu kwa nini *ZBC* haionekani, ni kwamba wanatakiwa wao wapate *up link* na *Satellite*, ina maana wanatakiwa wanunue walipe *fee* ili wapate kuonekana ndani ya *Satellite* waunganishwe kule. Sasa ukiangalia kwa upande wa Azam. Azam wao wanatumia Fiber aiba ambayo ni ya *Internent* hiyo. Sasa

transmission ambayo inayofanyika kutoka *DSTV* ipo kutoka *South African*. Sasa ili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waweze kuonekana kupitia *ZBC* ndani ya *DSTV,* wanatakiwa wao walipe hii *fee* kwa kununua nafasi kwenye *satellite* na gharama yake kama unataka *normal TV* ni kati ya dola elfu tatu mpaka elfu dola elfu tano (5,000) kwa mwezi, ambayo ni sawa sawa na milioni 7 au milioni mpaka 10 kwa mwezi, lakini utakuwa unaonekana duniani kote. Na kama unataka upate *HD* ambayo ni *High Definition* inakwenda mpaka dola elfu tano.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa mwezi wa Septemba na huko mbele afanye utafiti wa kina, lakini katika mwaka huu tungependa sasa na Rais wetu na yeye anze kuonekana kimataifa na Wazanzibari ambao wanaishi Mabarani Afrika katika maeneo tofauti waweze kuona nchi yao na mambo yanayofanyika mazuri hasa katika masuala ya taarifa ya habari na mambo ya maendeleo.

Suala jengine ninalotaka nilizungumze juu ya Mabaraza ya Vijana ambayo yamezungumzwa katika ripoti hii. Kwa kweli Mabaraza ya Vijana ukiangalia katika utekelezaji ukurasa wa 21 kwenye namba (d) inasema

"(d) Mashirikiano madogo baina ya Viongozi wa Mabaraza na Uongozi wa juu wa Wizara: Kamati baada ya kuyatembelea mabaraza imegundua kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa Vijana, yanayotokana na ushirikiano mdogo wanaopata kutoka kwa Wizara hasa wanapokuwa na shida inayohusiana na fedha na ushauri."

Haya Mabaraza kwa kweli yameundwa kwa mujibu wa sheria na sisi kwa upande wetu viongozi na ndani ya majimbo Wawakilishi na Wabunge ni kuwaongoza na kufanyakazi nao kwa karibu. Lakini unakuta mzigo huu unawaangukia sana Wabunge na Wawakilishi, lakini tayari kifedha hakuna bajeti ambayo waliyoekewa wao. Mimi kwa mfano jimboni kwangu nina Shehia 13. Shehia 13 si kidogo kwa Mwakilishi na Mbunge kwenda kusimamia haya Mabaraza na mbali bado inabidi tusimamie vijana wetu ndani ya Chama cha Mapinduzi kutoka kwenye Matawi na maeneo mengine pamoja na Wadi zetu.(*Makofi*).

Kwa hivyo lazima upatikane muafaka mzuri kuweza kujua, kwa sababu sasa hawa vijana wapo lakini inategemea na nguvu na kasi ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa jinsi gani wanaweza kuwasaidia. Lakini mzigo ni mkubwa kwa wakuu wa Wilaya na hata viongozi wa majimbo. Kwa hivyo serikali itafute njia jinsi gani ya kuwapatia Wizara fedha ili jambo hili lijulikane vipi tutaweza

kuwasaidia kwa pamoja. Ni aibu sana ukiangalia ukisoma kwenye ripoti kwamba wanapozungumza hapa kwa shida inayohusiana juu ya fedha na ushauri. Ina maana hata wizara viongozi wanawakimbia kuwapatia ushauri. Hili ni jambo ambalo linalotakiwa lisifanyike. Mimi ningeshauri sana chonde chonde viongozi vijana wetu hawa ni nguzo muhimu kwetu sisi. Kwa hivyo tunaomba sana, tumeanzisha haya Mabaraza kwa ajili ya kuwasaidia. Hivyo Serikali ikae na ifanye utafiti wake wa kina ili tuhakikishe hawa fedha wanazipata. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa nitakwenda katika eneo la utalii. Mambo mengi nimekuwa nikizungumza katika miezi ya nyuma na mengine nilikuwa nikiyazungumza kabla sijawahi kuwa Mwakilishi. Nataka niipongeze serikali kwa upande moja suala la usalama. Kwa kweli suala la ulinzi na usalama kwa wageni limeongezeka. Nitatoa changamoto ambazo zipo kwenye masuala haya. Kwanza ni suala la taka taka. Maeneo yetu na Wilaya zetu sasa hivi hasa wanaokwenda pwani pamoja na fukwe taka zinazidi kuongezeka. Hivyo, nashauri sana kwa Mhe. Waziri hebu aangalia utaratibu gani juu ya hizi taka utaweza kufanya ili kuhakikisha kwamba hatuandikwi kwenye mitandao *Zanzibar is beautiful but Zanzibar is dirty.* Yaani hii ni aibu kweli kusikia kisiwa chetu cha Zanzibar tunaandikwa ni kichafu. Yaani Wazanzibari ni wasafi, tunaoga mara tatu, tunakaa vizuri lakini tunaambiwa kisiwa chetu kina takataka. Haipendezi kabisa kwa nchi yetu hasa pale tunaposema kwamba utalii ni nguzo ya Taifa, pato letu kubwa sana sasa hivi asilimia zaidi ya asilimia 80 ya pato tunapata kutoka kwenye biashara ya utalii hasa katika suala *foreign exchange*.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nataka nilizungumze ni suala la *general tourism education*. Mkakati wa Serikali unapozungumza kwamba utalii au hii utalii kwa wote au utalii kwa sote, ukiliangalia hii *strategy* niliwahi kulizungumza mwaka jana kwamba ipo juu, ukija chini bado haijaunganika pamoja na wananchi wetu. Bado utalii unaonekana kwa sababu hata ukiongea na vijana wetu, mtu unapozungumza suala la utalii anafikiria utalii ni hoteli. Hoteli ni kitu tofauti kabisa na *tourism. Hotel management* ni sehemu tu katika *tourism education*.

Sasa mimi ningeshauri suala la *general tourism education* lianze kuwa *introduced* katika maskuli angalau vijana wetu wafahamu kilichopo nje. Unapomkuta kijana anafika miaka 15, 16 mpaka 17 bado hana uelewa, sio anatakiwa ajue nini maana ya hoteli, afahamu kuhusu mambo ya *laundry, department* za kwenye hoteli, afahamu kuhusu *front office* au afahamu maana ya *maintenance account, marketing*, aelewe utalii na umuhimu kwa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri sana Mhe. Waziri wa Elimu upo hapa leo pamoja na Mhe. Naibu Waziri upange mkakati mzuri ili kuwasaidia vijana wetu hasa wale wanaoanza *form one* kwenda juu, waanze kufahamu maana ya t*ourism education* japo kwa wiki saa moja wapate kuelewa na hili litawapa matumaini katika lugha ya kiingereza, bado tupo nyuma sana kwenye lugha ya kiingereza. Vijana wetu bado katika kujieleza wanachangamoto hata utayarishaji wao wa *CV* bado upo nyuma. Hili ni muhimu hasa katika ajira huko tunakotaka kuwaelekeza.

Mhe. Naibu Spika, tunalalamika kwenye ajira lakini bado tunachangamoto kwa upande wa pili. Kwa hivyo hata kianzio hichi, Wazungu wanasema *a tree does not know what a life thinking* narudia tena "jani halijui mzizi unafikiria nini" Mzizi wa hili lote ni kumtayarisha mtoto juu ya malezi ambayo tulikuwa tunaongea sote. Kama tutawepa kidogo wapate kuelewa kwenye masuala ya elimu na utalii, angalau utayarishaji wa mandhari na mazingira yake huko anakokwenda mbele atakuwa na kianzio kizuri.

Suala jengine ambalo nitaligusia ni suala *taxation*, ningefurahi kama Waziri wa Fedha angalikuwa yupo, lakini bahati mbaya ametingwa na kazi. Kwa kweli mimi bado nasikitika sana wawekezaji bado wana matatizo kwenye masuala ya *taxation* pamoja la *license*. Hili limekuwa la muda mrefu sana yaani ni aibu kwamba kuna mtu anachajiwa *hotel levy* ambayo inastahiki kwa mujibu wa Sheria ya *VAT* ya mwaka 1998 asajiliwe katika *VAT* anabakishwa katika *hotel levy*, hoteli moja iko hapa nyengine iko hapa. Sasa hili kwa kweli sio sawa hatuwezi tukatenda haki lakini mmoja anapewa sawa mwengine hapati. Hili lina umuhimu wake kwa sababu mwisho wa mwezi anapopeleka mapato yake *return* zake za mapato anashindwa ku-*claim* kwenye *return* yake *in put* na *out put* ya *VAT* na ni mbaya sana, kwa sababu tayari unamkuta mtu sasa serikali inachukua fedha nyingi kwa mwekezaji ambaye anastahiki na yeye pia apate unafuu katika hili.

Mimi nawapongeza sana *ZRB*, ukiangalia *trend* ya *ZRB* walipotoka hata katika elimu, hata katika mazungumzo sio kama zamani. Sasa hivi Wazanzibari wanaingia *ZRB* kama wapo nyumbani. Hili kwa kweli nawapongeza sana zamani ukimsikia mtu anaingia *taxman* mtu wa *ZRB* ulikuwa unatetemeka, unaona ni adui lakini siku hizi unapewa elimu, wanakusaidia wanafanya *assistance* au *guidance* ambalo hili jambo nimelipigania na ninalisema siku *ZIPA* hakuna *assistance and guidance*.

Mhe. Naibu Spika, ukenda katika taasisi ya *ZRB* hata *ZSSF* wanawashinda hao wenyewe *ZIPA* ambao wanatakiwa wafanye, wanafanya kwa wale ambao wanaostahiki wanawataka wao. Kwa hivyo suala la *taxation* bado kwa Zanzibar kuna changamoto kubwa sana. Hata ukenda kwa wafanyabiashara wadogo inakuwaje mtu anaku-*charge* Dola 30, anataka ulipe kwa kichwa kimoja Dola 9, (9x2 =18). Sasa 30-18= 12, anabakiwa na dola 12 hajamlisha mgeni *breakfast*, hajalipa umeme, hajanunua *bed sheet* jipya, kweli ndio tunawatendea haki wafanyabiashara wetu?

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nenda Mji Mkongwe kule ukaangalie wanalipishwa leseni na Manispaa, wanalipishwa leseni pamoja na Utalii. Lakini mtu anatakiwa awe *license* na *tourism* analazimika alipe kwenye Manispaa. Hatuwafanyii haki wafanyabiashara, kwa hivyo lazima tuangalie na mkakati, tuliondoe. Mara nyingi nimesema hapa *licensing is a regulatory board is not avenue to make money*, kwamba leseni unam-*regulate* mtu kumtambua, sio wewe ufanye ndio sehemu ya kupata mapato yako.

Jengine nataka nizungumze suala la Unguja Ukuu, Bungi na Mwera Ponge. Kuna maeneo mazuri kule Bungi ambayo ya kale yanatakiwa yatambulike na vijana wanatakiwa yaingizwe. Kihistoria hapa Zanzibar tunasema, *Prison Island*, *Spice Island*, hizi sehemu za kihistoria zinataka ziingizwe katika maeneo ili katika maeneo hasa ya utalii mnaosema kwa wote tuweze kuwapelekea vijana wetu na wao wapate kufaidika na hili lina umuhimu wake, kwa sababu ni historia yake pia na pia tutakuwa tunaweza ku-*preserve* historia yetu na tunatumia *culture* na *history as avenue* kupata fedha. Sasa haya yote tunatakiwa tuyafanye.

Lakini pia kwa ujumla kwenye suala la utalii na jinsi gani tunawa-*guide* wawekezaji na wafanyabiashara wadogo wote kwa pamoja. Ili ukiaangalia Wizara yetu ya Habari Utalii, Utamaduni na Michezo huko nyuma walikuwa na Hoteli ya Bwawani ambalo juzi nimesema lile jumba sasa hivi limejaa limekuwa ni chaka la mashetani, ukiangalia zamani ilikuwa ni Chuo cha Maruhubi, ukiangalia sana mambo ya *Prison Island* ...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika moja kumalizia.

Mhe. Simai Muhammed Said: Ahsante, ukenda sasa hivi ukiangalia hii Wizara maeneo yote muhimu waliyokuwa nayo yameshachukuliwa. Mimi ukisema utalii bado upo kwenye wizara ukiangalia kwa kweli hawana lolote pale la kusimamia isipokuwa Kamisheni. Sasa ukiangalia ili paweze kufanyika mkakati madhubuti ni vizuri pia sasa tuwaelekeze nguvu zatu kwenye Wizara

hii wapatiwe bajeti ya kutosha kwenye suala la *marketing* ili wainyanyue Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, juzi namuona Waziri wa Utalii Mhe. Najib Balala, Waziri wa Utalii wa Kenye anafanya *sky diving* ana *introduce a new execution* Mombasa, anaruka kwenye ndege kutoka karibuni futi elfu 10 anakuja chini, unapanda unalipia Dola 800, 600. Lazima tufanye tu- *introduce new execution* tutabaki mpaka lini *Prison Island* tuwe *introduce* hivi vitu mambo ya *water sport* tunaogopa nini. Fungueni sehemu za *hellcopter*, fanyeni mambo ya *hot air ballon* tuweni wabunifu, *creativities is needed* ndani ya *tourism*, mnachukulia utalii kama biashara tu za muhogo, haiwezekani tufanyeni kazi kwa mpango sisi tukifanya vizuri tunamuweka Rais wetu anapaa.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache ambayo niliyozungumza, nakushukuru sana, nawashukuru Wajumbe pamoja na Mawaziri na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe nakushukuru sana.

Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Sasa anakuja Mhe. Nadir Abdu-latif, akimaliza atakuja Mhe. Omar Seif Abeid atafuata Mhe. Hidaya Ali Makame. Mhe. Nadir una dakika kumi.

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Bismillahi Rahman Rahim.

Mimi nitaanza kuchangia ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Lakini nitaanza kwenye Wizara ya Habari kwa sababu dakika ni kidogo nitaanza huko.

Jambo la mwanzo suala la michezo Mhe. Naibu Spika, michezo bado Zanzibar ipo nyuma sana ukitoa suala la mpira wa miguu na *netball*, michezo iliyobakia ndani ya nchi yetu imewekwa chini sana hasa mambo ya michezo ya baiskeli, mambo ya *tennis*, mambo ya *swimming* na mambo ya *king boxing*. Bado Zanzibar haijatoa wapiganaji nje ya Zanzibar kutambulika zaidi kwenye masuala hayo.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana, nimemshauri sana Mhe. Waziri kwenye masuala ya michezo angalau akaweka michezo karibu aina 15, kwa sababu

kuna nchi kama Russia, Amerika, UK na European *countries*, michezo ndiyo inayofanya moja ya kutangaza nchi. Ndio maana ukakuta katika *olympic* Kenya inashiriki sana na inakuwa maarufu sana kwa sababu tu ya wale ambao wanakimbia *marathon* mita 100 mita 500 imekuwa maarufu sana kwa sababu ya michezo. Watu wanaoweza kwenda mbio Zanzibar tunao wengi hasa vijana.

Jengine kwa upande wa Baraza la Wawakilishi tuna mchezo wa mpira tu. Mhe. Waziri mimi ningekuomba sana ungekaa na uongozi angalau na upande wa Baraza la Wawakilishi ukaunda basi timu nyengine ya watu wa kuogelea ya Wawakilishi au ya kupigana *king boxing* Wawakilishi na Mabunge mengine kuliko suala la mpira tu. Hayo ni mapendekezo yangu kwenye suala la michezo.

Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye suala la *ZBC.* Mimi nitoe pongezi tu kwamba sasa hivi mpo *more advance* tofauti na zamani mambo ya kukatika-katika mambo ambayo yalikuwa yanajirudia rudia matatizo yameondoka nawapongeza baadhi ya viongozi ambao wanajitahidi kwenye masuala haya. Lakini pia ambacho nimekusudia kukwambia kwenye suala la *ZBC* hawa watendaji wa chini wako katika mazingira magumu na mazingira yenyewe ni kama tunavyoona wanasimama hapa ndani ya ukumbi hawana hata kiti ambacho waweza kukaa cha kupanda na kushuka ambacho wataweza kuendesha wenyewe mambo yao ya kamera, lakini wanasimama kuliko mapolisi wakati hao waandishi wa habari si mapolisi. Mimi naomba sana wapatiwe viti kwa sababu wengine wanaumwa unaweza kuwakuta wamechokaa kukaaa baridi ndani humu nyingi, wapate sehemu ya kukaa nzuri lakini sio viti hivi ambavyo vilokuwepo kutokana na kamera zao ziko juu viti vya chini watafutiwe viti vya kupanda na kuchuka.

Lakini jengine wanapata vile vile kwenye masuala ya changamoto, masuala ya baridi wanapata macho yao yanangalia sana darubini, lakini mimi ningeomba hata kama wana posho ya ziada wazidishiwe basi kwa sababu kazi zao nzito kama tunavyoziona *(Makofi)*

Nchi nyingi tunaona kwamba waandishi wa habari ni matajiri wanakuwa na fedha nzuri tu mbali ya malipo wanayopata na zile posho zinakuwa kubwa kubwa ili ziwawezeshe pamoja na usafiri ya kwenda kutafuta utafiti habari, na wao kuna habari nyengine wanapozichukua wanalipia hawa, wanalishia mtu awambie habari nzuri wapewe wanatumia. Sasa mimi ningeomba kwa suala hili nichangie kidogo upande wao.

Likini kwenye suala la utalii Mhe. Waziri, Zanzibar ukizungumza peke yake tayari ni utalii na ukizungumza utalii sio kwamba alivyosema Mhe. Simai Mohammd Said kwamba ni mahoteli tu, kuna watalii ambao wao wanaweza kwenda nchi kwa ajili ya *snorkelling* tu, wanaweza kaja Zanzibar kwa *diving* tu, wanaweza kuja Zanzibar kwa masuala ya kuona *local village* tu masuala ya vibanda vibanda na masuala ambayo ni ya *culture*.

Lakini kuna wageni ambao wanakwenda nchi kama Zanzibar kuja kuona *historical site,* mambo ya historia na mambo mengine. Lakini vile vile wengine wanakuja Zanzibar kwa ajili tu ya ustaarabu wa watu historia ya Zanzibar vipi inazungumza. Mimi ningependa kutoa ushauri wangu leo tunakuta mtu anatembeza mgeni ndani ya nchi yetu, lakini yule anaetembeza mgeni anavuta unga, anakunywa viroba ambavyo vimepigwa marufuku, huyo mgeni wenyewe anakuwa na wasi wasi hata kufuatana na yule *tour guide.* Ningeomba sana suala hili na suala hili halipo mjini tu, liko mpaka mabarini Nungwi, Paje hawa mapapasi na ma-*beach boys* wamejaa wanauliza wageni masuala ya bangi, masuala ya unga, masuala ya pombe ambazo haziruhusiwi na vitu vyengine. Na sisi lengo letu kwamba Zanzibar tulete utalii wenye kipato cha juu. Mimi naweza kusema Zanzibar tayari tunao utalii zamani tu wakipato cha juu sababu hoteli za Zanzibar ni *very expensive.* Hoteli za Zanzibar ukikaa *Serena, Hyatt* chumba cha chini Dola mia mbili hamsini kwenda juu, wakati ukenda Dubai na nchi nyengine chumba cha Dola mia ni *four star hotel* kwa *five star hotel* unakaa.

Wakati Zanzibar kuianzia *three star, two star* unaanza unakuta Dola mia. Sisi tayari wageni wa bei kubwa tunawapata zamani tu lakini ninachoomba kwamba nchi yetu kwanza tuzidi kuzidisha usafi kwa sababu mtu anategemea kwenda nchi alipe fedha nyingi nchi iwe safi, iwe na ulinzi mzuri hasa katika maeneo ya ufukwe, wale mapapasi wanaokera kera watu na mambo mengine wapungue. Vile vile miundo mbinu iwe mizuri leo, tunakuta kwenye mahoteli nyingi ukienda Nungwi na sehemu nyengine, njia za kuingia ndani mgeni kama anaumwa na mgongo basi hata akifika taabani uti wa mgongo, njia mbovu, zimejaa mashimo ambavyo ni vipande vidogo vidogo na kuna watalii unakuta wengine wenye mahoteli wapo tayari kuchangia zile njia ili wasipate usumbufu, lakini huku nyuma walichangishwa wakaliwa fedha zao na *still* hakujafanyika chochote kama *Double ...., Hilton* na hoteli nyengine waliwahi mpaka kuchangishwa, masuala ya mambo ya *oil* na masuala mengine karibu milioni ishirini, walinambia wenyewe Meneja nilizungumza nao.

Sasa masuala ya miundo mbinu iwe mizuri. Leo unakuta hoteli zinanunua maji kama *Serena Hyatt* juu ya uzuri wao wanunua maji kila siku gari tatu, ukipiga

hesabu kwa mwezi karibu milioni tisa wanatumia kununua maji ya kutumia ndani ya hoteli. Hili suala nchi yoyote ambayo zilizoweka *free zone* ambazo hasa za *investment* mnatakiwa masuala yale ya *infrastructure* muwe mushayapeleka maji, umeme na miundo mbinu mengine ambayo ya barabara inakuwa imeshafika, ndipo mgeni anaweza aka-*invest* kwa njia nzuri. Lakini hivi tunavyokwenda sisi, mgeni tunampa eneo, tunampa masharti haujafika umeme halijafika maji wakati kuna vitu vyengine ni wajibu wenu Serikali kuvikamilisha kama suala la umeme kupeleka sio watalii tu au wafanya biashara, hata kwa wananchi ni wajibu wenu kupeleka nyinyi pamoja na maji na masuala mengine, leo unakuta maji mahoteli wananunua, kila kitu kuna matatizo.

Lakini tukenda kwenye suala hilo hilo la utalii leo, tuna sehemu nyingi za *Museum* ndani ya Zanzibar. Kuna pale Mtoni kuna kuja jengo lile, kuna Beit el Ajaib lile. Ningeomba sana Serikali mbali ya kwamba wanaruhusu wageni kila siku waingie kuangalia mazingira ya historia, basi maeneo yale tafuteni *brand* zile hoteli kama *Sheraton Inter-continental, Park, Hyatt, Kempinski* ziungeni nao mkataba waziendeshe zile wafanye mahoteli ya *expensive room in the world*, kwa sababu tunaona kuna mahoteli duniani kuna chumba mpaka Dola elfu hamsini kwa siku. Sasa Beit el Ajaib na yale masuala mengine majumba ya kihistoria tutapofanya hoteli zile *luxury hotels* kwa zile ambazo *brand* kubwa duniani *management* ambazo zinaendesha, kama hapa tunapoona *Serena* na *The Resident*s, mkimpa jina kubwa basi ataweza kukodisha kwa pesa nyingi na Serikali inaweza kupata kipato kwa njia ya kuunganishana yaani *between* huyu mmiliki wa hizo kampuni pamoja na serikali.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, sisi Zanzibar tungeomba sana mngependelea kwa sababu Zanzibar bado kuna vitu hatuna, kama alivyoeleza Mhe. Simai masuala ya *sky diving* hatuna, masuala ya *Water and World Park*, kama vile Dar es Salaam. Bakhresa anajenga lakini ndio anaendelea kwenye *process* vile vitu ambavyo kuna wageni kama nilivyozungumza wanakwenda sehemu kwa ajili ya kitu kimoja tu. Lakini tushukuru kwa vile Zanzibar kwamba tuna mahoteli, lakini mahoteli yetu yenyewe ukiangalia mengine hayako katika hali nzuri. Vile vile ningeomba sana Mhe. Waziri hivi vitu angalau siku moja ungepata kwenda kutembelea na masuala mengine ungepata kuyaona.

Mheshimiwa nitaendelea kwenye suala la Wizara ya Wanawake na Watoto. Suala la watoto Mheshimiwa wanaonyanyaswa katika Kisiwa chetu ni wengi na hili suala sasa hivi Zanzibar kushakuwa na jina baya sana kwa masuala kama haya ya unyanyasaji. Lakini ndio kama tulivyosikia kwenye suala la

Kamati mimi nilishaanga sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kulizungumzia kwamba nilishituka, sio nilishangaa kwamba kuna mtu kamkimbiza mtoto huyo, huyo mtu sijui nimwite jambazi au mwizi au yeye akikimbizwa na yeye atakubali ni masuala ambayo hayaingii akilini mtu kumkimbiza mtoto kwa njia ambayo haifahamiki lakini nisiende huko.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala la unyanyasaji ni kubwa sana watu wanabakwa, wanatumiliwa hasa ambao wengine hawana akili wenye ulemavu wa akili pia wanabakwa, na hizi kesi haziendi isitoshe wale wazee ambao watoto wao wanabakwa unakuta vile vile wao ndio wa kwanza kwenda kuzifuta zile kesi hawana huruma wala hawana fikra. Lakini jambo ambalo siku hizi jambo kubwa sana linazidisha hawa waliotuletea haya masuala ya mipira ya kinga kwa kizungu *condom* wanaita.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Nadir malizia dakika moja muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy Mhe. Naibu Spika, nafikiri mimi nimeangalia *time* namaliza dakika hamsini, labda umekosea angalia vizuri dakika zako.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Nadir acha ulalamishi dakika moja, mimi saa ninaiona pale, endelea dakika moja malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, walioleta mipira ile ya kuzuia kinga wanafanya makusudi na hii inawapa watoto kuwapa akili kwamba ala kumbe kuna mpira, basi tukafanye tu na suala la usalama. Mimi ushauri wangu suala la mpira wa kinga lipigwe marufuku hasa kwenye maduka yote ambayo yanauzwa kiholela, ili suala hili la mambo ya zinaa yapungue na ziuzwe kwenye *pharmacy* ambazo mtu anakwenda na cheti kama atatakikana kutumia kwenye masuala muhimu kama watu ambao wameandikiwa na daktari lazima atumie apewe. Lakini leo zinauzwa utafikiri biskuti na masuala haya tukiwaendekeza hawa watu ambao waliotengeneza hivi vitu, tutakuwa hatufiki popote. Hili suala ambalo ndio linazidisha zinaa, lakini kukiwa hiki kitu hakipo sana pia watu wataweza kupunguza kufanya zinaa kwa sababu watakuwa wanaogopa lakini wanajiamini kwa sababu hivi vitu vimejaa.(*Makofi*)

Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kumalizia dakika zetu tunaonewa sisi tumekuja kufanya kazi, hatukujaja kucheza kwa nini mnazipunguza tuko tayari kutoka saa kumi za usiku humu.

Mhe. Naibu Spika: Haya kaa kitako muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Aah**!**

Mhe. Naibu Spika: Kaa kitako. Mhe. Omar Seif Abeid baadae atafuata Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika na mimi nashukuru kunipa muda wa kuzungumza kidogo kuchangia katika Ripoti ya Kamati ya Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mheshimiwa mimi moja kwa moja naanza kwenye mambo ya utalii. Utalii Mheshimiwa tukiingia katika *page* namba 3 sambamba na *page* namba 9 inayozungumzia mapato au makusanyo ya utalii kwa upande wangu mimi yananitia wasi wasi, kwa sababu hayaoneshi vizuri naomba kunukuu kidogo.

Kwamba wanasema kwenye hiyo *page* namba 3 mapato "Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla shilingi bilioni mbili, milioni mia tano arubaini na saba mia mbili sitini na nane (2,547,268,000/=). Wizara ikiwa ni hizo shilingi bilioni mbili milioni mia tano arubaini na saba mia mbili sitini na nane (2,547,268,000/=) na shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=) kwa upande wa Kamisheni ya Utalii".

Lakini hadi kufikia Disemba jumla ya shilingi milioni mia moja hamsini na moja mia tatu ishirini na tisa na sitni na mbili zimekusanywa (151,329,062/=) zimekusanywa kwa upande wa Wizara, ikiwa ni sasa na asilimia 27.65 kwa makadirio kwa upande wa Kamisheni ya Utalii wameweza kukusanya mia moja thamanini na nane milioni laki saba arubaini tisa mia nane na tisa (188,749,809/=), kati ya shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=). Milioni mia moja thamanini na nane mia saba arubain na tisa mia nane na tisa (188,749,809/=) kati ya shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=) walizokadiriwa ambazo no sawa na asilimia 9.

Jambo hili Mhe. Naibu Spika linalipa wasi wasi mkubwa mimi lakini nataka nimuulize Waziri swali langu. Jee, kwa mwaka huu au kwa msimu huu wa utalii wageni wetu wameongezeka au wamepungua, kama wamepungua, kitu gani kilichosababisha wageni wetu wapunguwe. Lakini kama kiwango chetu cha uingiaji wa wageni wapo na wameingia ni kwa sababu gani kwenye kipindi hiki ambacho ni *season* ya kuitegemea tumekusanya asilimia tisa tu ya makadirio ambayo tumejiwekea.

Lakini sambamba hilo ukienda kwenye hiyo *page* ya 9 kuna jambo ambalo Kamati naishukuru wameliona wamesema, "Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya wageni wanalala katika mikahawa na mahoteli ambayo hayatambuliwi kisheria au haina kibali cha kulaza wageni", hilo ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunategemea hapa ili tupate mapato, Serikali tunazungumza mambo mengi lakini mengi ya mambo tunayoyazungumzia tunahitaji fedha lakini ikiwa hili lipo kuna mahoteli yanalaza wageni hayana vibali, wanalaza wageni bila ya kutambulika hili tatizo. Sijui Kamisheni pamoja na wakusanyaji kodi wamejipanga vipi na wameliona vipi tatizo hili na wamelichukuliaje.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wangu mimi nasema na naiomba sana Kamisheni ya Utalii ikishirikiana na *ZRB* kwenye suala la utalii waliangalie sana, tunapokosea kukusanya mapato kwenye sekta mbili hizi, siku zote nazungumza karafuu na utalii hapa tutapoteza lengo letu. Ni vyema kabisa tukaelekeza tukajikita hasa katika sehemu mbili hizi kuzitunza na kuziendeleza ili ziweze kuzalisha zaidi. Mheshimiwa huyu siye ndio ng'ombe wetu wa maziwa tunayetegemea kumkama ili tukapata maslahi, wananchi wanatutegemea kuwapelekea huduma zote elimu, afya zote serikali zinahitaji fedha, iwapo tutakwenda na mwendo huu mimi nasema usioridhishwa hatutofika pahala hilo ni moja.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spka, lakini kwa upande mwengine mimi naomba kwamba wao wenyewe wamiliki wa mahoteli wawe ni waaminifu, binadamu muaminifu hana haja ya kusimamiwa, wafanye *operation* ya makusudi. Mimi natoa wito kufanyika *operation* ya makusudi na kuwabaini wale wote ambao wanafanya biashara kinyume na utaratibu wachukuliwe hatua ikiwa pamoja na kuwafungia kabisa leseni zao au kuwapa leseni kwa masharti mazito kabisa ambayo wakipatikana na kosa mara ya pili wasiweze kupewa tena vibali kwa sababu wanaturudisha nyuma Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nende tena katika Wizara ya Habari, mwenzangu Mhe. Simai Mohammed Said katika *page* 5 hiyo, tumezungumzia juu ya mapungufu ya mashirikiano katika Taasisi zetu na mimi wakati tulipokwenda kule tuliyakuta baadhi ya mambo kidogo kidogo. Lakini nashukuru kwa busara ya mratibu wetu wa Ofisi kule ya Uratibu iliyoko Tanzania Bara ameweza kuyaweka sawa. Natoa wito kwa ile Ofisi ya Uratibu iliyoko Dar es Salaam pamoja na Wizara ya Habari kupitia vyombo chetu hiki cha *ZBC* waonekane kwamba wote ni Wazanzibari, hakuna haja yakubaguana, sote sisi ni Wazanzibari. Lakini nina swali moja nataka niulize. Wale wanaishi Dar es

Salaam walipwa mshahara wa kiwango cha Zanzibar lakini tunaona hali ya maisha ilivyo Dar es Salaam na Zanzibar ni tofauti. Jee, Wizara imechukuliaje imewangalia vipi hawa vijana au watumishi wetu walioko kule kimaslahi. Natoa wito na naomba kwamba kwenye bajeti hii inayofuata Wizara zinazohusika ziangalie mambo hayo kwa kuwapa motisha zaidi wale watumishi wetu ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa kuipenda kazi yao, najua wanafanya kazi kwa upendo lakini naomba wazidishiwe ili na wao wapate moyo zaidi wa kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine tuliyoikuta ambayo iko wa wote ni changamoto ya vitendea kazi. Mheshimiwa vitendea kazi waandishi wa habari vitendea kazi vyao ni kamera, ikiwa kweli hata kamera hawana, kazi hizo watafanya vipi, hawawezi kufanya kazi. Kwa hivyo naomba sana na natoa wito kwa wizara kwamba kwenye bajeti hii litengwe fungu maalum kwa ajili ya kuwapatia watumishi wa *ZBC* walioko hapa Zanzibar na walioko kule vitendea kazi wawe na sehemu maalum, kuwe na posho maalum au sehemu maalum kasma iliyowekwa kwa ajili ya vitendea kazi vya wafanyakazi wetu kwa Idara ya Habari Maelezo na mambo mengine na Taasisi nyengine.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hili la *scheme of service* nimeshalizungumza. Kwa hivyo sasa naingia katika Baraza la Kiswahili. Mhe. Naibu Spika, katika Baraza la Kiswahili lugha yetu ya Kiswahili si Zanzibar ilikuwa ndio nchi ya kwanza watu wote walikuwa wakitaka kujifunza Kiswahili wanakuja hapa Zanzibar. Lakini leo tumeanza kuona kwamba sisi Zanzibar tunaonekana hatujui Kiswahili, kuna watu wanaojua Kiswahili wanatufundisha. Mfano kama juzi kuna maneno mengi ambayo yanaingizwa yana mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza linatafutwa neno, kuna maneno mengine kama hayo juzi tunayaona hatujui yalikotoka ugatuzi, sijui nini na nini. Mimi naomba kuwe na utaratibu wa kuyaenzi maneno yetu ya Kiswahili ya zamani.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa dakika moja umebakiza.

Mhe. Omar Seif Abeid: **L**eo wanafunzi wetu wanafeli zaidi kwenye Kiswahili kulikoni hata kwenye hicho Kiingereza. Kwa hivyo naiomba Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Habari washirikiane ili kukitunza Kiswahili.

Lakini la mwisho ni Baraza la Vijana Mheshimiwa. Baraza la Vijana ni Baraza ambalo tumeliunda kwa mujibu wa sheria, lakini jambo la kusikitisha ni kwamba Baraza hili haliwezeshwi kufanya kazi, vipi wataweza kufanya kazi kama hatujawezesha. Wito wangu kwamba Wizara ya Kazi kwenye bajeti inayokuja wajipange na waone iko haja sasa ya kuliweza Baraza hili ili liweze

kufanya kazi vizuri kwa mujibu liweze kutimiza lengo tulilokusudia. Kwa sababu bila ya kuliwezesha hawataweza Mhe. Naibu Spika, kufanya lililokusudiwa.

Baada ya haya natamka rasmi kwamba naiunga mkono ripoti hii ahsante sana Mhe Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hidaya Ali Makame baada ya Mhe. Hidaya Ali Makame atafuata Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza ya kuchangia juu ya Ripoti hii ya Kamati ya Utalii, Uwezeshaji, Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nianze kwa kuwapongeza na kuwashukuru sana Wajumbe wa kamati hii kwa kazi ngumu na kubwa waliyonayo. Lakini pia kwa changamoto nyingi ambazo wanakumbana nazo katika wizara zao wanazozitendea kazi, mimi niwaambie wasivunjike moyo na waendelee kuifanya kazi kilillahi na wazidi kuifanya kazi hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanza na mimi nianze kuichangia ripoti hii moja kwa moja nianze kwenye suala la vijana. Naanza kwenye Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto juu ya suala la vijana.

Mhe. Naibu Spika, vijana ndio muhimili mkubwa ndani ya nchi yetu hii, lakini pia kama wizara imelifahamu hilo kwamba vijana ndio ambao mpaka sasa hivi kwenye Tanzania yetu hii ndio watu ambao wenye kundi kubwa na ndio watu ambao wanaoisukuma hii Tanzania kwa mawazo, michango na fikra. Ijapokuwa tunaonekana ni vijana wadogo lakini nina uwezo wa kusema hivyo kwamba vijana ndio dhamana ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, lakini vijana hawa hawa walipoonekana kwamba tayari wapo wengi, lakini kazi za kufanya wao ni nyingi pia, ila zimekuwa kidogo kutokana na wingi wao. Hawa vijana waliwekewa chombo maalum ambacho kinaitwa ni Baraza la Vijana, chombo hicho ni kwa ajili yao vijana kueleza kero zao lakini pia kutatua na matatizo yao na changamoto mbali mbali ambazo zinawakabili.

Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi chombo hiki hatujui malengo yake ni nini, na chombo hiki labda hawa vijana wameletewa kweli kwa ajili yao au

kimeletwa tu kwa ajili ya watu kuja kujinufaisha. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Baraza la Vijana lilikabidhiwa kwenye Wizara ya Uwezekezaji, Wanawake na Watoto, lakini mpaka hivi ninavyokwambia vijana hawa hawana ofisi, ambayo ofisi hiyo wanaweza wakaitumia kwa kazi zao zote zilizowazunguka ndani ya nchi nzima. Vijana hawa wanapata tabu sana, wanahangaika sana hali ya kwamba baba yao ambaye aliiweka hii Kamati ya Vijana kwenye Baraza la Vijana aliangalia mbali na akaona kwamba hiki kitu kinaweza kikawasaidia vijana na kikawaweka pahala pazuri.

Lakini bado vijana hawa kifupi wamepuuzwa kwa sababu kama ingekuwa tayari imeanza kufanya kazi hili Baraza la Vijana, basi kwa muda mchache tu ambao lilikuwa limeshawekwa na chaguzi zake na kila kitu kimeshatimia, basi tayari kimoja wapo kingekuwa kimeshajuulikana. Kwa sababu kazi wanafanya nzuri na tunaziona na tunazisikia, lakini bado wamekabiliwa na mambo mengi ambayo yanawakwaza na yanawaathiri kutokana na hii hali iliyokuwepo. Wakitizama jambo hili aliyeliweka ni mtu mzima ambaye tayari ameshaona kwamba kuna mazuri ndani yake, lakini bado kuna watu ambao wanalipuuza kwa kutokulifanyia kazi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kamati imeona hapa kwamba uwepo wa idadi kubwa ya vijana ndani ya Baraza hayo ya vijana kwenye Wilaya na kwenye Shehia. Mhe. Naibu Spika, lakini kuna changamoto nyingi sana ambazo zimewakabili vijana hao ukitoa hizo za ofisi, na pia kutokuwa na bajeti yao ambayo inawasimamia wao vijana katika kufanya kazi zao hizo, watazifanyaje kazi hizo bila ya kuwa na bajeti yao inayowasimamia. Ningeiomba wizara kwenye suala hili la vijana hiki kifungu cha bajeti ambacho kinawasimamia vijana wenyewe ni taasisi inayojitegemea liwepo hili fungu la bajeti ambalo litaweza kuwasaidia kwenye kazi zao zote zilizowazunguka na bila ya kumtegemea Mwakilishi, Mbunge wala Mkuu wa Wilaya kwenye masuala yao ya uendeshaji.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije kwenye suala la filamu za kiutamaduni. Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba nchi yetu hii ya Zanzibar ni nchi ya kiutamaduni na Mzungu au mwekezaji au mgeni anapotoka huko kwao anapokuja hapa anakuja kwenye nchi ya Zanzibar, ili kuja kuangalia utamaduni wa Mzanzibari. Tunaona sasa hivi utamaduni huo haupo umetoweka kabisa, lakini utamaduni huu umetoweka tangu kwenye majumba yetu mpaka huko kwenye hizo filamu ambazo tulikuwa tunaziangalia hapa na zilizokuwa zinatuburudisha zinatuweka katika sehemu tofauti.

Mhe. Naibu Spika, filamu za kiutamaduni wa Mzanzibari zimetoweka si kwenye redio wala si kwenye *TV,* hatuzioni siku ambayo labda kitawekwa

hicho kipindi hukifahamu kimeanza vipi wala kinaelezea kuhusu nini, kwa sababu ni filamu tayari ambazo zimekwishaharibika maana hazifuatiliwi wala haziko. Na kama ziko basi ziwekwe ili vizazi vyetu vipya vilivyopo vijue kweli Mzanzibari na yeye anaweza kufanya hayo masuala sio hao wanaokuja sasa hivi na filamu zao za *season* zisizofahamika mwanzo wala mwisho, ambazo ziko tofauti na maadili yetu ya Mzanzibari. Kuna filamu nyingi ambazo zinapotosha wala hazifahamishi mpaka zinasababisha sasa hivi mpaka wanafunzi wetu hawana hata amani ya masomo yao wala kujua nini wanafanya, wao wapo tu wakiingia Chakorie wakitoka Chakorie.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hili suala kwa kweli sasa hivi limeshakithiri hasa juu ya hizi filamu, tunaomba sana Wizara ya Habari ilifuatilie suala hili la filamu za utamaduni. Tumuone Mzanzibari jinsi anavyovaa kanga, tumuone Mzanzibari jinsi anavyoandaa vyakula vyake, tumuone Mzanzibari jinsi anavyoandaa mambo yake ya kwenye shughuli zake za ndoa na shughuli zake za kutafuta maisha pia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nije pia kwenye suala la kumbukumbu na mambo ya kale. Mhe. Naibu Spika, kumbukumbu hazipo zinapotea zilizobakia ni chache lakini pia nazo zinaweza zikapotea kama hatutozishughulikia, kwa sababu washughulikiaji ndio sisi lakini tunazipuuza na tunazidharau. Waliobakia huko nje kidogo sana ambao wanajua umuhimu wa hizi kumbukumbu, lakini wao watapata motisha wapi kwa sababu sisi ambao labda tunakuwa wengi kuweza kuzihifadhi kumbukumbu zile hatuzifanyii kazi, na kwa yule ambaye anataka kuzifanyia kazi anakosa hata ile hamasa ya kuweza kuifanya kazi ile kwa ajili ya kuifadhi ile kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, kuna makumbusho mengi ndani ya nchi yetu hii ambayo sasa hivi yanapotea ukitoa hizo nyumba, na ukitoa sehemu nyengine za vivutio kama hizo za Mwana wa Mwana, Minara na majumba makubwa ya Makumbusho ambayo yapo sasa hivi yanavunjika na yanapotea.

Mhe. Naibu Spika, mambo ya kale kwa hapa kwetu Zanzibar ndio kivutio kikubwa cha watalii wetu. Jee, tujiulize hawa watalii ambao wanaingia sasa hivi kwa idadi kubwa ndani ya nchi yetu hii wanakuja kwa lengo gani? Na kama tutalifahamu hilo lengo ambalo wanajia basi tujitahidi ili hawa watalii wasije wakapotea wakatoweka ndani ya nchi yetu ya Zanzibar ili wazidi kuja watalii hawa basi tuyaenzi haya makumbusho na tuuenzi utamaduni wetu ili watalii hawa wazidi kuja hapa petu. Kwa sababu Kamati wametwambia hapa kwamba kuna idadi kubwa ya watalii ambao wanaingia ndani ya nchi yetu, ijapokuwa hayo mapato yanayoingia juu ya watalii hawa hayaonekani lakini

watalii tunajua kwamba wanaingia siku hadi siku, ndege kubwa kubwa zinaingia, meli za kila aina mtu hajawahi kuliona anajua jumba tu limelala pale baharini kumbe ile ni meli zinakuja na watalii hao. Lakini watalii hao mwisho watapotea kutokana na wao wanatoka huko kwao kuja kutizama utamaduni wa Mzanzibari. Mzanzibari wenyewe akifika hapa Mzungu anamkuta amevaa sawa sawa na yeye au kuliko yeye Mzungu. Jee, tujiulize mtalii huyu kweli atakuja? Yeye anakuja kuangalia utamaduni wa Mzanzibari, Mzanzibari wenyewe hamkuti si huko vijijini sasa hivi wala si huku Mjini. Kwa kweli utamaduni tunaupoteza na tunauondoa wenyewe.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nije tena kwenye suala *ZBC TV* na *ZBC Radio*. Mhe. Naibu Spika, kamati imetwambia kwamba kuna changamoto nyingi ambazo wamekutana nazo kwenye vyombo vyetu hivi vya habari vya *ZBC* kuhusu suala la usafiri. Usafiri kwa kweli ni changamoto kubwa juu ya wafanyakazi wetu hawa, kwa sababu tunajua kwamba wanafuatilia habari mbali mbali, lakini matukio mbali mbali wanayafuatilia lakini bila ya usafiri hawatoweza kuzifanya kazi hizo. Pia hawatoweza kufika hizo sehemu za matukio kwa ule muda ambao tunataka wafike, kwa sababu kama tukio tayari limeshatokea sasa hivi huwezi kumtoa mtu kule kama hana usafiri mpaka apande daladala au ampigie simu boda boda aje amchukue muda huo umeshapita na lile tukio pengine tayari limeshakwenda na muda.

Mhe. Naibu Spika, niiombe sana wizara iliangalie suala hili na waweze kuwasaidia hawa wafanyakazi wetu wa *ZBC-TV* na *ZBC-Radio* waweze kufatilia matukio yetu mbali mbali yanayotokea katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie suala la mwisho kwenye suala udhalilishaji. Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji tunajua kwamba sasa hivi imekuwa *too much* katika nchi yetu. Kwa hivyo niiombe wizara ifunue macho lakini na masikio, pia na miguu yao sasa hivi waiweke *smart* kwa ajili ya kufatilia kazi hizi. Mhe. Naibu Spika…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha, malizia.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naiunga mkono ripoti hii asilimia mia moja na Mwenyezi Mungu awabariki wote. Ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir, baadae atafuatia Mhe. Hassan Diaspora.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache katika taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuchangia kidogo katika kamati hii.

Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na kwa kuanzia naomba nianze kwa kunukuu Kanuni zetu ambayo Kanuni ya 4(1) inasema kwamba:

"Kutakuwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye atachagulikuwa na kushika madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni hizi".

Lakini ukiangalia maana ya Spika katika tafsiri ya Kanuni hizi unakuta maana yake ni Spika wa Baraza isipokuwa kwamba Naibu Spika, Mwenyekiti wa Baraza au Mwakilishi mwengine yeyote aliyechaguliwa kwa ajili hiyo anapokuwa anakalia kiti cha Spika katika kikao chochote cha Baraza au anapokuwa akitekeleza shughuli yoyote ambayo ni kazi ya Spika atakuwa na madaraka na mamlaka yote ambayo amekabidhiwa kwa Spika kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni hizi. Na ukiangalia kifungu cha 67 Mhe. Naibu Spika kinasema" "Spika atawajibika kutilia nguvu kanuni zote za Baraza".

Mhe. Naibu Spika, imenibidi ninukuu Kanuni hizi kwa sababu kumekuwa na mwendelezo ama kumekuwa na *trend* ya uvunjwaji wa Kanuni katika Baraza hili. Ambayo sasa hivi *trend* hii inaelekea kama ni kawaida yanatokea matukio kama kawaida katika Baraza ya kuvunja hizi Kanuni. Na kila siku Mhe. Naibu Spika, haya mambo yanapotokea nakuwa najiuliza Ofisi ya Spika inakuwepo wapi katika kulinda hizi Kanuni za Baraza.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nitaje matukio mawili matatu ambayo yametokea kipindi cha nyuma na yamepelekea maana yake kama kustaajabu *as if* hakuna Ofisi ya Spika ambayo inafanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia naanza *issue* ya mavazi ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye alipigwa Kanuni na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, wakati hili linatokea nilijiuliza wasaidizi wa Mhe. Spika walikuwa wapi…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Wanu unachangia ripoti au unaanza kutoa darasa la Kanuni?

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, *I don't mean* kutoa darasa la Kanuni lakini utangulizi wangu nilitaka kugusia haya masuala…

Mhe. Naibu Spika: Kwa maelekezo yako dakika 10 hizo utazitumia katika kutoa maelezo ya Kanuni nina hakika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Hamna tatizo Mhe. Naibu Spika…

Mhe. Naibu Spika: Lakini sijakusimamisha kwa ajili ya hiyo Mheshimiwa, nimekusimamisha kwa ajili nafikiri mjadala hapa katika *order paper* tunajadili Ripoti ya Mwenyekiti, ndio *order paper* inavyosema Mheshimiwa, na wewe unavunja Kanuni sasa. Tunajadili Ripoti ya Mwenyekiti, sasa niambie wewe mwenyewe uko sawa wapi?

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba unilindie muda wangu ambao umeutumia, lakini pili hotuba inakuwa ina sehemu tatu nilivyofundishwa, *Intro, Body* na *Conclusion*, hii ilikuwa *just my introduction* lakini kama Mhe. Naibu Spika, unaona inakugusa nitakwenda moja kwa moja kwenye hoja yenyewe.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi katika hii ripoti nilikuwa nataka kuchangia kuhusu suala la udhalilishaji wa watoto, sijaona jengine lolote la kuchangia kwa sababu hili suala la udhalilishaji wa watoto ndio kadhia kubwa katika jamii yetu hivi sasa iliyopo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kugusia kwenye suala la udhalilishaji wa watoto na ninavyoona hivi sasa ni kwamba serikali, ama wizara, ama taasisi ambazo zinahusiana na kushughulikia hili suala zinaanza kushindwa kulishughulikia hili suala kwa sababu tayari imeshakuwa *too much* katika jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la udhalilishaji lina mapungufu mengi katika ushughulikiaji wake, na mapungufu haya, taasisi zimekuwa zikirushiana paka wa uso. *DPP* anasema Polisi, Polisi anasema *DPP*, Polisi na *DPP* wanasema Mahakama, Mahakama wanasema *DPP*. Kwa hivyo, haijuulikani hasa hili tatizo liko wapi pamoja na kwamba pia kuna tatizo ambalo linahusiana na jamii kutokuwa na uelewa mzima wa haya masuala.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niishauri serikali kwa moyo safi kabisa na wala sitowi *directives* lakini naomba niishauri kwamba iundwe Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia hili suala, kwa sababu sasa hivi imeshakuwa tatizo kubwa taasisi hatuzielewi zinasemaje, kila mmoja anamtupia mwenzake mpira. Kwa hivyo, iundwe Kamati ya Kitaifa ikimpendeza Mhe. Rais ili ishughulikie

hili suala na ije na ripoti ambayo itazungumzia mapungufu yaliyopo katika hii kadhia nzima ya udhalilishaji, lakini pia baadae waje na mapendekezo ambayo ndio itakuwa kama muongozo kwa wizara na taasisi husika za kuzifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, nina mengi yakuzungumza lakini najua kuna hoja binafsi ya Mhe. Mjumbe ambayo inakuja kuhusiana na kadhia hii nitakuja kuzungumza huko. Sasa naomba nikae kwa heshima yako na naomba ni-*conclude* kwamba naunga mkono hoja na nawaomba Wawakilishi wenzangu wengine waunge mkono hoja taarifa hii.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Wanu. Mchangiaji anayefuate nimesema ni Mhe. Hassan Diaspora, baadae atakuja atachangia Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia ikiwa ni saa 12:20 nitajitahidi nitajitahidi nitumie mpaka saa 2:30 katika kumaliza muda wangu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza nchi hii kwa hekma na busara kubwa hadi hii leo. (*Makofi*)

Pia napenda kunukuu maneno ya *Paramaunt leader* wa India, Hayati Mahatma Gandhi alisema kwamba: *"The role of the Government is to work for the people and the role of politician is to serve the people"*. Maana yeke nini, maana yake ni kwamba wanasiasa na serikali sote tunafanya kazi moja, tunajenga nyumba moja ya kuwaletea maendeleo wananchi. Mhe. Naibu Spika, jukumu hasa la Baraza hili la Tisa ni kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima wana Mapinduzi wa nchi hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua naomba kuchangia nikiwa ni Mjumbe wa Kamati hii, naanza na Shirika la Utangazaji. Naomba sana kuchukua fursa hii kumpongeza Mkurugenzi dada yangu Iman Due kwa kazi nzuri anayoifanya katika Shirika hili la Utangazaji, sote tumeona, tumekuwa mashahidi sote hali ya utangazaji wa redio na televisheni mambo yameongezeka na yako mazuri kuliko yalivyokuwa kabla. Lakini taasisi hii inakabiliwa na changamoto ya madeni inazidai taasisi za serikali, naziomba sana taasisi hizo zilipe madeni yake ili shirika hili liweze kufanya kazi zake kwa vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nitaingia Shirika la Magazeti. Shirika la Magazeti lina jukumu hilo hilo la kusambaza sera za serikali kupitia magazeti,

lakini niwapongeze watendaji wa shirika hili pamoja na watendaji wa wizara hii. Tulipokuwa tunafanya kazi ya kamati tulitembelea wakatupa ripoti kwamba wanataka kufanya *repair* jumba lao lililokuwa la Mhe. Spika wa zamani kwa kutumia shilingi 270 milioni tukakataa kama Wajumbe wa Kamati, tukasema haiwezekani. Lakini baada ya mjadala mkubwa wamefanya *repair* jumba hilo kwa shilingi 150 milioni na shilingi 120 milioni za serikali zimekuwa zimebakia.

Baada ya hapo nitakwenda katika Kamisheni ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, bila ya kutafuna maneno Kamisheni ya Utalii ina jukumu kubwa la kututafutia watalii nchini na watalii ndio uti wa mgongo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayotutilia mapato makubwa ya serikali. Lakini Kamisheni ya Utalii ina uzembe ambao kuna mahoteli mengi yanafanya kazi ya utalii na zile *guest house*, lakini Kamisheni ya Utalii hawajui, kutokujua kwao na uzembe wao kunaifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupoteza mapato makubwa. Naomba sana uzembe huu usitokee tena. Tulipokuwa tunafanya kazi ya kamati tuliugundua uzembe huu mwingi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nitakwenda Tume ya Utangazaji. Tume ina jukumu la kudhibiti shughuli zote za utangazaji Zanzibar, wale wote wasiofanya vizuri, wasiofuata sheria na taratibu za utangazaji jukumu la Tume ni kuwadhibiti. Tume hii inakabiliwa na changamoto kubwa ambayo ni kudai taasisi za serikali zimekuwa pesa ni nyingi tayari Tume hii inaanza kushindwa kufanya kazi zake kutokana na madeni.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nitakwenda Wizara ya Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Wizara hii ni muhimu imekusanya wanawake, wazee, watoto, vijana na mambo mengine. Katika wizara sitaki kuingia hii kadhia iliyozungumzwa sana iliyozusha mjadala hapa ya mtoto Ibrahim. Lakini naomba kusema yote haya yametokezea kutokana na kutokuwa na ushirikiano na Mhe. Waziri na Kamati. Mimi ni Mjumbe wa Kamati tumeona jinsi gani Mhe. Waziri *may be she was busy with another stuff*, lakini ushirikiano haukuwa mzuri na kamati ndio maana haya yote yametokezea. Namuomba sana Mhe. Waziri ni mama yangu, dada yangu, watoto wake kina Joel Castico nilisoma nao *tuition* pale kwa Babu, asifanye hivi ashirikiane na Kamati. Kamati ndio uti wa mgongo wa wizara yoyote ile kwani sisi ndio tunaokuja kuiombea bajeti. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakwenda katika pencheni ya wazee. Napenda sana kuchukua fursa hii kimapinduzi kabisa kutangaza wazi wazi kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa

kufikiria mpango huu wa kuwalipa wana Mapinduzi wetu wazee wetu shilingi 20,000 kila mwezi. Nchi nyingi zilizoendelea ndio zinafanya kazi hii, lakini na sisi Zanzibar na umaskini wetu Mhe. Rais ameweza kufanya lakini niliyoyagundua Mhe. Naibu Spika, naomba kuyatangaza hapa leo hadharani.

Mhe. Naibu Spika, tulipokutana na watendaji hawa hesabu za pencheni ya wazee hasa kinachobaki kwa wale wazee waliotangulia mbele ya haki kwa siku mbili zilikuwa hazijakamilika wala hazikamiliki. Ni wazi panatakiwa kutupiwa macho mawili na sio mawili ni macho sita, panaonesha wazi wazi hapako sahihi hesabu hazikai sawa kwa siku mbili pia hesabu zilikuwa hazikai sawa, pesa zinazorudi hazionekani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba kwenda katika yumba za kulelea wazee. Kuna nyumba tatu za kulelea wazee Zanzibar, nazi ni Welezo, Limbani-Pemba na Sebleni. Mhe. Naibu Spika, tuliyoyagundua Limbani panalipwa shilingi milioni moja na laki tano wako wazee wanane, Welezo shilingi milioni tano wako wazee 34 na Sebleni wako wazee 31 wanalipwa shilingi milioni saba na nusu. Kwa masikitiko makubwa tulikwenda mpaka kufungua vyungu Mhe. Naibu Spika, wale wazee hawalishwi chakula kizuri, serikali inalipa pesa nyingi lakini wazee wale walishae chakula kisichoridhisha.

Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Afya tulikwenda tukatizama pale *Mental Hospital* wanalishwa chakula kizuri kule Mheshimiwa, lakini kule hawalishwi *balance diet,* wanalishwa kama wafungwa, wanalishwa maharagwe na wali, mkate kwa chai tu, pesa serikali inalipa nyingi lakini kazi haifanyiki mpaka mapembe tuliyakuta katika stoo ya vyakula ya wazee wale. Wale wanatakiwa kula *full diet* mayai, mchicha, maziwa, vyote hivi hawapewi na serikali inalipa pesa nyingi. Tunaishukuru serikali kwa kuhakikisha inawalipia wazee wale lakini hawapati chakula kinachostahiki. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kadhalika uchafu katika nyumba zile, uchafu umezidi, lakini cha kusikitisha zaidi kule Limbani Pemba tuligundua jengo limefanyiwa *repair* kwa zaidi ya shilingi milioni mia moja na kitu, lakini tuliyoyakuta kule ile *floor* pia imetiwa kiraka. Naomba kusema marekebisho yaliyofanywa Limbani Pemba na pesa zilizolipa serikali hayaendani. Naiomba taasisi husika iingilie kati *CAG* na wengine wakafanye upembuzi yakinifu wa matumizi ya pesa zile na kazi iliyofanyika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nakwenda katika Wanawake na Watoto. Mhe. Naibu Spika, kila mtu ni shahidi Zanzibar imekuwa kadhia kubwa tumechoka kila siku kuambiwa mtu huyu kabakwa, mtu huyu hivi, tumechoka.

Naomba sana iundwe Kamati kama alivyosema mwenzangu ya kulishughulikia suala hili tushachoka. Kila siku watoto wetu hawako salama tutakuja kusababisha mtu kuuwa hapa kwa sababu mtoto wake kabakwa na itakuwa tumesababisha wenyewe. Kwa hiyo, kiufupi tumechoka.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuna kesi ya ndugu yangu Omar Ali Omar siku ya tarehe 29 Kampuni ya *Eastern Construction Ltd* ilimuuwa. Kampuni hii imeajiriwa pale *Mtoni Marine* kwa Bakhresa ilileta mizigo kupitia kontena, kila *tiles* moja ilikuwa ina uzito wa kilo 125 zimefungwa nne nne zimo ndani ya kontena, walipokuwa wanashusha zile *tiles* huyu mfanyakazi zilipomzidi wafanyakazi wenzake wakenda mbio.

Mhe. Naibu Spika, sheria za kimataifa uzito ule wa *tiles* zinatakiwa zishushwe na *forklift* au mashine nyengine sio mtu, wakenda mbio kwenda mbio *tiles* zile zikamuangukia maskini ya Mungu akafariki. Kampuni imekataa Mhe. Naibu Spika, hata kutoa bima yake au *insurance* wake kutoa. Naiomba serikali iliingilie kati marehemu ana watoto watatu, ana kizuka, watoto wake wamebakia tu, kampuni imeuwa ilisema hata si mfanyakazi wake. Kwa sababu Idara ya Usalama na Afya Kazini ipo katika wizara hii. Naomba kusema serikali naiomba sana iliingilie kati suala hili, imemuuwa hayati Omar Ali Omar naomba sana serikali kampuni hii ifukuzwe kama inakataa bado kutoa mpaka *insurance* kumlipa, *customer liability insurance*.(Makofi)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo naomba kuwaombea Baraza la Vijana. Kwanza namsifu sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuanzisha Baraza la Vijana katika kuwafanya vijana kuwa *cooking pot* katika kuchangia maendeleo ya nchi hii. Lakini naomba kusema vijana hawa bila ya kuwawekea bajeti yao katika ile wizara na wakawa na bajeti yao wenyewe wanafanya wenyewe wanavyotaka, lile lengo mahususi la kuwataka vijana kutoa mchango na lile Baraza la Vijana hatutofika. Naomba sana hawa vijana tuwapatie bajeti yao na kila kitu chao ili waweze kufanya mambo yao wenyewe. Pana matatizo ya kifedha ambayo wanalalamika kuwa fedha hawapati hata Pemba hawajafika tangu Baraza lile limeanzishwa, kazi zao zinakuwa hazifanyiki kwa sababu wanasema hawapati pesa.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kwa heshima na taadhima kubwa naomba kuunga mkono hoja hii, taarifa hii tuliyoileta sisi nikiwa mimi Hassan Khamis Hafidh mkwezi na mkulima kutoka Jimbo la Welezo na kamati yangu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi na baada ya hapo atafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuichangia Ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Kwanza nichukue fursa hii kuweza kuipongeza sana kamati hii kwa ripoti yao nzuri iliyosheheni mambo mbali mbali yanayohusiana na sekta hii. Zaidi nimshukuru na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Ali Suleiman Ali maarufu Shihata, Mwakilishi makini wa Jimbo la Kijito Upele.(*Makofi*)

Vile vile nichukue fursa hii ya kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wote ambao wamenitangulia katika michango yao mizuri.

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba michango mingi imechangiwa na mimi nilikuwa nina hiyo hiyo wamenifilisi kwa kiasi. Lakini kwa sababu na sisi tunastahiki kukazia nielekee katika Sekta ya Habari. Kwanza niushukuru uongozi mzima wa Wizara ya Habari, Utalii na Michezo na hususan nimshukuru sana Mkurugenzi Mkuu wa *ZBC*, kutokana na ufanisi na mabadiliko ya haraka katika sekta au taasisi hii aliyokabidhiwa. Nimshukuru sana.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, *ZBC* ina kazi ngumu na wenzangu wameshaieleza na inapaswa kupewa mwega ili shirika hili liwe ni shirika la mfano katika Tanzania na nina imani kwamba inawezekana kutokana na hali inavyokwenda. Ina changamoto nyingi niiombe serikali iweze kuwaongezea bajeti yao kwa kipindi hiki ili iweze kupiga hatua, kwani taasisi hii inakabiliwa sana na madeni. Wamerithi madeni makubwa lakini vile vile wanawadai taasisi mbali mbali. Wenzangu wameshazungumza hilo tumuombe sana Waziri wa Fedha na Mipango aweze kuwasaidia zile taasisi ambazo zinadaiwa na *ZBC* basi kuweza kuzikaba na kuweza kulipa madeni hayo ili taasisi hii iende kwa ufanisi.

Vile vile katika uendelezaji wa matangazo ya *ZBC* niipongeze kwa kuweka wakalimani wa lugha ya alama. Ni jambo zuri kwa sababu linawapa fursa wenzetu kuweza kufahamu taarifa mbali mbali zinazotokea katika nchi hii na ulimwenguni kwa ujumla. Niliombe tu shirika kuweza kufanya mipango yake katika bajeti hii kuweza kuwaajiri vijana wale watatu ili kuweza kuona kwamba wanajisikia kuwa ni wafanyakazi wa kudumu wa shirika letu. Lakini

vile vile kwa sababu kuna changamoto ya wataalamu ningeomba sana serikali na hususan wizara hii kuweza kuwapa mafunzo kutokana na mabadiliko haya kutoka analogia kwenda digitali, ili kuweza kuona kwamba wanaendana na wakati na wanakabiliana na zile huduma zinazotakiwa zitolewe katika shirika hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuondoka hapo sasa nije katika *ZBC* kwenye kitengo cha Dar es Salaam. Ukweli tumefarajika sana kwamba hivi sasa ukitizama taarifa ya habari katika televisheni yetu tunazipata taarifa mbali mbali kutoka upande wa wenzetu, inatia moyo na inatupa hamu kuweza kuzitazama taarifa za habari zetu. Ningeomba sana kitengo hiki kiongezewe uwezo. Changamoto tumeziona wafanyakazi wamesema wapo wanne wakati sekta ziko tatu, kuna gazeti, redio na televisheni. Ni vyema sana kitengo hiki kiongezewe wafanyakazi ambao wanaweza kufanikisha zaidi vyombo vyetu vya habari hususan *ZBC* kuweza kupata habari mbali mbali sio za Dar es Salaam tu, lakini hata za mikoa mengine. Inashangaza kuwa tunaambiwa hawana gari ya uhakika, huwezi ukatafuta habari bila ya kuwa na usafiri wa uhakika.

Vile vile maslahi yao. Maslahi yao lazima yatizamwe wanafanya kazi kwa bidii sana. Mimi ninafuatilia sana toka kipindi cha magazeti asubuhi lakini hata zile zinazorushwa kwa njia ya televisheni. Kwa hiyo, niombe wafanyakazi hawa wafikiriwe, wapewe nyezo na waweze kufanya kazi ya kutuletea taarifa mbali mbali ili vyombo vyetu viwe na mvuto kwa sisi wenyewe kuweza kuvisikiliza.

Mhe. Naibu Spika, nielekee kwenye Shirika la Magazeti. Shirika hili lina hali mbaya, kwanza kutokana na vifaa vyake hata ofisi ambayo wanatumia. Ofisi wanayotumia kama utaitembelea pale Shirika la Utangazaji, Rahaleo itakutia huzuni, wafanyakazi karibu ya kumi wako ndani ya chumba kimoja lakini ukitizama hizo kompyuta zao utakuta karibu ya asilimia 90 ni mbovu. Sasa huwezi kufanya kazi za gazeti ukiwa na vifaa duni kiasi hicho, yule sekretari wa mkurugenzi kakaa kama yuko katika kibanda cha mitaani, kwa kweli haipendezi, hawa watu watayarishiwe jengo vizuri nao wajisikie kwamba wana taasisi nzuri ya kuweza kufanya kazi vizuri.

Kwa upande mwengine gharama za gazeti hili kwa sababu wenzetu wanachapisha Tanzania Bara gharama ni kubwa na gazeti letu lazima tukubali halina mvuto wa kibiashara. Kwa hivyo, hii itaweza kuleta kwamba gazeti hili liwe linakwenda kwa hasara na ndio maana wenzetu wanatuomba sisi Wawakilishi basi tununue magazeti 15, 10 kwa mwezi kutoka kwao ili kuongeza hili soko. Sasa kitu kilicho kizuri hakilazimishwi mnunuaji kinajiuza

wenyewe. Kwa hivyo, niombe sana gazeti hili liwe na wabunifu na liwe na mvuto.

Vile vile taasisi yetu hii inayoshughulika na uchapaji basi tuone kwamba gazeti hili linachapishwa kwetu kwa gharama ambazo zitakuwa ni nafuu na kuweza kuleta tija kwa gazeti hili. Pamoja na kwamba wanalo soko katika Mikoa ya Tanzania Bara, vile vile hili tulifikirie itakapokuwa gazeti hili tutalichapisha hapa, inawezekena pia masoko yale ya Tanzania Bara tunaweza kuyakosa. Kwa hiyo, ni kitu ambacho serikali ikae na hususan Wizara hii ya Habari kuweza kuona kwamba inaratibu vizuri ili gazeti letu hili liwe ni gazeti ambalo lina tija kwetu na shirika hili linaendelea kudumu.

Mhe. Naibu Spika, nielekee katika Sekta ya Michezo, nipongeze uongozi wa Waziri mahiri ndugu yangu Rashid Ali Juma amejitahidi sana kugeuza katika sekta hii na ajitahidi kuweza kuleta mabadiliko ili kuweza kuona sekta hii inapiga hatua. Lakini nimuombe tu Mhe. Waziri akae na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuweza kulitizama suala la michezo. Huwezi ukawa na maendeleo makubwa ya michezo bila ya kushirikisha vijana na watoto na hao tunawapata katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, somo la elimu kwa michezo katika skuli zetu kutokana na kutofundishwa ipasavyo hii inadhorotesha sana kuweza kuleta maendeleo ya michezo katika skuli zetu na nchi kwa ujumla. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo kukaa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuweza kuona changamoto mbali mbali zitakazoweza kusaidia wao kwa pamoja kuweza kuona kwamba elimu ya michezo inaanza kutolewa katika ngazi ya maandalizi vizuri na najua na nina imani kwamba mitaala ipo lakini utekelezaji wake ndio tatizo, kama hatujaanzia huko chini tusitarajie kwamba tutakuwa na wanamichezo wazuri na kupiga hatua kubwa katika sekta hii.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Habari kwa kutumia juhudi yake na ubunifu wake. Nchi hii toka 1964 haina ukumbi wa michezo ya ndani wa kitaifa. Hii kwa upande mmoja haileti sura nzuri, huwezi ukawa na maendeleo mazuri ya michezo wakati huna mikumbi ya ndani ya michezo. Nchi hii ilisifika sana kwa michezo midogo midogo kama michezo ya *table tennis*, ilikuwa inang'ara sana kwa nchi za Afrika Mashariki, tulikuwa na vijana wazuri sana katika michezo hiyo. Nchi hii ilisifika sana kwa michezo ya *bedminton* michezo hiyo hivi sasa inafifia siku hadi siku. Nchi hii ilisifika sana kwa masuala ya kuogolea, hivi sasa hali hiyo imefifia.

Nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba nchi hii inahitaji kuwa na ukumbi wa kisasa wa michezo ya ndani ambayo itasaidia kuweza kukuza vipaji sio katika mpira wa miguu kuna maeneo mengi na nchi hii ilingara lakini tumeyapoteza, kwa sababu mtu anaenda Haile Selassie katika ukumbi wa skuli anaambiwa hapa haiwezekani anaenda Ben-bella anaambiwa kuwa haiwezikani na kwa sababu serikali haina ukumbi wa michezo.

Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri hili tulitizame kwa kina litatisaidia sana kuweza kukuza michezo mengine midogo midogo ambayo hapo nyuma ilikuwa inaleta tija na sifa kubwa kwa taifa hili.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nielekee katika suala la Utalii.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili malizia.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika , kuna suala hili la Utalii wa Makundi. Mhe. Naibu Spika, Utalii wa Makundi unapoteza pesa nyingi sana katika nchi hii, watalii wanalipa kwao na hii tulipita mpaka kwenye Bodi yetu ya Mapato bado halijapata ufumbuzi. Ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa sababu hii ni sekta tuliyoitarajia sana ili iweze kuongeza mapato basi akae na wenzetu wa *ZRB* kuweza kuona kwamba linapa ufumbuzi na mapato haya yanaweza kupatikana.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, katika suala hili la utalii kwenye miaka ya 1980/1990 kama kumbukumbu zangu ni nzuri tulikuwa na michezo ya Zanzibar *Marathon* na *Triathlon* hii michezo ilileta sifa sana na ilikuwa inaongeza wageni kuja katika nchi. Nijiulize sijui hali ile ilienda wapi. Nimuombe sana Mheshimiwa alifuatilie lile suala lilikuwa na tija sana kwa taifa kwa upande wa wageni, lakini vile vile kuweza kukuza vipaji vya michezo hii kwa vijana wetu.

Nimalizie Mhe. Naibu Spika, kutokana na suala la *ZBC* karibuni nilikuwa naona kuna *channel* ya *ZBC II* na nilikuwa mtazamaji sana wa ile michezo ya Afrika iliyofanyika nchini Garbon kama sikosei. Kwa kweli tulifarajika sana kuweza kupa mechi hizi *live*. Lakini baada ya uchunguzi wangu nikaona kwamba *ZBC* ilikuwa inashirikiana na *AZAM TV,* sijui kuna mikataba gani ambayo ilikuwa inaleta tija kwetu.

Ningemuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutoa ufafanuzi tumefurahi lakini inawezekana vile vile ikawa kuna ....

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naipongeza tena Kamati na naunga mkono asilimia mia kwa mia ripoti hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Sasa atachangia Asha Abdalla Mussa na baadae atafuata Mhe. Masoud Abrahman Masound.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache kuchangia ripoti hii ya Wizara ya Mifugo, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na Wajumbe wenzangu ambao wamechangia mambo mengi kuhusiana na ripoti hii. Mhe. Naibu Spika, mambo mengi ambayo niliyotaka kuyazungumzia ameyagusa sana Mhe. Hassan Hafidh lakini na mimi nitayatilia mkazao hususan suala zima la Kamisheni ya Kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na Kamisheni ya Kazi tulipotembelea katika mahoteli yetu baadhi yao tumeweza kukuta changamoto kubwa ambayo inayohusiana na wafanyakazi ambao wamefanyakazi kwa muda mrefu hawana mikataba yoyote. Wafanyakazi hawa inafika pahala wawekezaji au makampuni wanawafukuza kazi kiholela na wao baada yake hawana pakwenda kukimbilia. Mhe. Naibu Spika, naomba sana kupitia ripoti hii watakapokuja kutoa ripoti yao mwezi wa Septemba basi tuhakikishe kwamba wafanyakazi hawa wanapewa mikataba.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie suala zima la wazee. Kuna nyumba za kulelea wazee kwa hapa Unguja Sebleni na Welezo. Lakini tulipokwenda kutembelea katika sehemu ya kulelea wazee Sebleni kulikuwa na utata. Mhe. Naibu Spika, tuliambiwa kuwa kuna jumla kwa Unguja wazee 61 kwenye ripoti zao, lakini cha kushangaza tulipokwenda Sebleni tuliambiwa kuna wazee 31 lakini ukijumlisha wazee 31 wa Sebleni Mhe. Naibu Spika, ukienda na Welezo kuna wazee 34 kwa kweli tunapa utata, hatujui wazee hao wengine wamefichwa sehemu gani, na tulipoenda kutembelea hatukuwakuta wazee wote, tumepelekwa tu kwa baadhi ya wazee kama watano tu. Lakini tuna wasi wasi kamati kwamba hawa wazee tulitajiwa humu kwenye ripoti hizi jee, ni kweli wazee hawa wapo 61 au 65.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wanawake na Watoto haya yote yametokea kwa sababu yeye mwenyewe pamoja na Katibu wake hawakuwepo na inaonesha kwamba baadhi ya watendaji wake walipotuletea ripoti wameturipulia. Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri akakae kwa kina aweze kuhakikisha kwamba wanatuletea ripoti ambayo iliyokuwa sahihi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kuunga mkono Wajumbe wenzangu hususan Mhe. Hassan Hafidh, tulipokwenda kutembelea tuliona kwamba pencheni ya wazee wa miaka 70 mahesabu yao ya matumizi hayakuwa ya uhakika na tulipohitaji maelezo kwa kina baada ya siku nyengine hatukupata maelezo hayo kwa kina, bado tuna wasi wasi na mimi naungana mkono na wenzangu kwamba iundwe Kamati ifuatilie matumizi mazima ya pesa za wazee lakini pia ifuatilie suala zima la matumizi ya pesa ya watoto ambao wanaishi katika nyumba Mazizini pia hatukupata maelezo kwa kina.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda na wenzangu wanataka kuchangia suala zima la hali halisi la udhalilishaji wa wanawake na watoto tumepewa kwa uhalisia wake na tumeona mapungufu, lakini kwa suala hili jinsi lilivyotugusa tumeamua kwamba kama mimi mwenyewe Mjumbe ambaye niko katika Kamati ya Uwezeshaji Wanawake na Watoto basi tutaleta hoja rasmi katika Baraza hili tukufu, ili tuweze kujadili kwa kina na tuone serikali kwamba nayo kwa upande wake inachukua hatua kupitia masuala mazima ya udhalilishaji.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Asha. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Masoud Abrahman Masoud na baadae atafuata Mhe. Dkt. Makame Ussi.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, mimi moja kwa moja niende kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii ambao wametuandalia taarifa nzuri chini ya Mwenyekiti wao Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri au Mawaziri wote walitupatia taarifa hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mie niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Utalii. Mimi niseme tu kuwa kuna malalamiko mengi kwa wafanyabiashara ambao wanapatiwa tenda kwenye mahoteli mbali mbali. Mhe. Naibu Spika, watu hawa ni wanyonge wakati mwengine huwa wanaweka nyaraka zao za mashamba au

majumba wanapopata tenda, lakini kwa bahati mbaya inapofika wakati pengine wameshapata fedha yao zaidi miezi sita au saba, baada ya kuona mfanyabiashara yule anakwenda na biashara yake vizuri, basi huwa wakati mwengine wanapobadilishana mameneja kwenye yale mahoteli basi huwa baadhi ya wafanyabiashara wanadai pesa zao mameneja wale wanakwenda likizo kwao Ulaya hatma yake wafanyabiashara wale hawapati pesa zao. Kwa hivyo, niombe Mhe. Waziri suala hili alifuatilie kuna wafanyabiashara wengi ambao bado wanadai kwenye mahoteli na wanazungushwa zungushwa na hawapati haki zao za msingi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye mikataba ya wafanyakazi hawa wanaofanyakazi kwenye mahoteli. Kwa kweli mikataba inakuwa ni tatizo, anafanyakazi mtu miezi mitatu anaambiwa nenda kapumzike nyumbani baada ya muda uje uombe tena kazi, kwa hiyo anafanyakazi miaka kumi lakini muda wote huo hapati mkataba kwenye mahoteli yake. Kwa hivyo, naiomba serikali ili kuhakikisha watu wetu wanapata haki zao za msingi basi serikali isimamie ili waweze kupewa mikataba katika mahoteli hayo.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende moja kwa moja kwenye Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Mhe. Naibu Spika, katika taarifa hii inaonekana kamati ilitembelea mpaka maeneo ya Mkamandume. Lakini katika maelezo yao inaonekana maeneo yale tayari kumbukumbu ile ya Mkamandume inaondoka, pale palikuwa na Msikiti na Msikiti haupo umejengwa Msikiti wa kisasa, kulikuwa na msingi mkubwa ambao unatoka hapo kwenye maeneo ambayo kunako Msikiti mpaka baharini, msingi huo tayari wote umeshajifukia. Lakini kulikuwa na kisima cha wake wawili ambao walikuwa na wivu waliokuwa hawaonani, sasa hivi kumbukumbu hiyo nayo imeondoka. Kwa hivyo, niseme kumbukumbu zinaondoka hawa watalii wanaokuja itafika wakati kumbukumbu kama hizi watakuwa hazipati.

Mhe. Naibu Spika, zamani huko Mkamandume kulikuwa wale watu wa Pemba baadhi yao wanaweza wakachukua ng'ombe wanaondosha nadhiri kwenye Msikiti ule, anachukuwa fedha anakwenda kuweka kwenye Msikiti ule wa zamani anaweka kama kuondoa nadhiri yake. Lakini sasa hivi kitu hicho hakipo kuna Msikiti wa kileo ule wa kumbukumbu ya zamani umeshaondika. Niombe sana Mhe. Waziri na yeye apate nafasi ende huko kwa Mkamandume ili ende akaone hiyo hali halisi ya ambayo sasa hivi ipo.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la ukusanyaji kodi kwenye maeneo ya historia. Bahati nzuri kwenye jimbo langu kuna maeneo ya Kijichi pamoja na Kizimbani. Mhe. Naibu Spika, katika maeneo haya huwa

kunakusanywa kodi kwa watalii wote wanaoingia pale. Sasa makusanyo hayo hatujui yanakwenda wapi na baadhi ya maeneo ya kwenye majengo ya mahoteli maeneo mbali mbali huwa wanakijiji kwenye Shehia husika wanajengewa skuli, wanajengewa hospitali lakini sisi bahati nzuri eneo letu la Kizimbani tunapata watalii wengi na inaingiza fedha nyingi kwenye serikali. Lakini eneo la Shehia hatuna msaada wowote tunaoupata. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri eneo la Kizimbani analijua watalii wengi wanaingia kwenye *spice* pale angalau na Shehia nayo ipate fedha kwa ajili ya kuingiza kwenye Kamati ya Maendeleo ambayo na sisi tutakuwa tunafaidika kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, unyanyasaji wa kijinsia. Mimi niko katika Kamati ya Ustawi wa Jamii sio hii maana yake majina yamebadilika. Lakini kamati ile tulitembea na viongozi wa Wizara ya Elimu kwa kweli wakati wanatoa majumuisho tulisikitika sana, wanasema kuna baadhi ya maeneo hasa Kaskazini Pemba unaweza ukapita kwenye skuli watoto wadogo kabisa wa kiume tayari wanafanyiwa vitendo vibaya. Mhe. Naibu Spika, sasa zamani nilipokuwa mimi mdogo ilikuwa ukimkuta mwanamme alikuwa anafanyiwa vitendo vibaya, basi huwa tunakusanyika watu tunamuangalia heee! yule ndio anafanyiwa hivyo. Lakini sasa hivi Mhe. Naibu Spika, inaonekana kama ni kitu cha kawaida. Sasa tusipoziba ufa kwenye skuli tutakuja kujenga ukuta. Mhe. Waziri anayeshughulikia Wanawake na watoto, mimi nahisi sio Pemba peke yake mpaka hapa Unguja tufanye kazi ya kuhakikisha tunapita kule skuli, kuna viongozi wa skuli wanayajua haya mambo kwa sababu sisi tuliambiwa na viongozi wa Wizara ya Elimu, tukae sawa tukaangalie "tusipoziba ufa tutajenga ukuta".

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye suala la mikopo. Mhe. Naibu Spika, vikundi huwa vinapatiwa mikopo baada ya kuangaliwa kuwa vina uwezo wa kurejesha mikopo hiyo. Lakini kuna masikitiko makubwa yalioko kwenye taarifa hii wanasema kumbukumbu ya mikopo inayotolewa haijulikani. Sasa katika wizara zote au taasisi zote kuna ma-*cashiers* ambao wanashughulikia masuala ya fedha. Lakini leo ukiambiwa kumbukumbu hazipatikani sina uhakika hapa akamatwe nani. Lakini niombe sana serikali maeneo haya ambayo kamati imeainisha kuwa hakuna kumbukumbu nzuri, yafuatiliwe kwa karibu sana ili zijulikane hizi fedha zilizotolewa hawakupeana shangazi na mjomba? Kwa sababu kama zinaonekana zimepeana shangazi na mjomba ndio maana unaambiwa kuwa kumbukumbu hazionekani.

Lakini kama kuna vikundi ambavyo vimesajiliwa kwenye Afisi ya Vyama vya Ushirika utajua wa kumkamata na kama serikali imetoa pesa kupeleka ngazi ya

Wilaya lazima inajua. Kwa hivyo, tusiambiwe kuwa hakuna kumbukumbu kwa hiyo inasababisha kuona viongozi wanaosimamia maeneo haya hawako makini sana. Kwa hivyo, niombe serikali iwafuatilie kwa karibu ili tuone fedha hizi zinakwendaje.

Mhe. Naibu Spika, nipongeze kwenye suala zima la pencheni ambayo wanapatiwa wazee shilingi ishirini elfu kwa mwezi. Mhe. Naibu Spika, pesa hii ni ndogo sana mimi pamoja na wewe na watu wengine tuliokuwemo ndani ya jengo hili, asubuhi ukiondoka nyumbani ukiacha shilingi ishirini elfu, kwa kweli inaonekana ni pesa ndogo. Kwa hivyo, niipongeze serikali kwa kuanza na kima hichi lakini ikiwezekana basi ziongezwe kidogo, fedha hizi bado ni kidogo sana.

Mhe. Naibu Spika, kwenye hili sisi kama viongozi wa Majimbo tunapata tatizo kwa sababu kuna watu ambao hawajatimia miaka 70 pesa hizi wanazipata, lakini kuna watu wana zaidi ya miaka 70 pesa hizi wazipati. Kwa hivyo, niiombe sana serikali ifanye uhakiki mpya kuhakikisha alietimia miaka 70 anapata haki yake na yule aliyekuwa hajatimia apunzime asijisogeze miaka kabla ya miaka yake 70 haijafika. (Makofi)

Mhe. Naibu Spika, niombe sana serikali wazee hawa ukipitia kwa Wajumbe wa Sheha basi utawapata. Lakini ikiwezekana kama uwezekano upo tukiona kasoro hizi zimetokezea kwa Wajumbe wa Sheha iundwe Kamati ifuatilie kila Shehia ili tuhakikishe wale wazee waliokuwa hwanatakiwa kupata haki hii ya elfu ishirini kila mwezi wanaipata.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niwapongeze Wajumbe wa kamati hii kwa kazi nzuri walioifanya lakini pia niwapongeze na Waheshimiwa Mawaziri kwa usimamizi mzuri wa wizara zao. Naunga mkono taarifa hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. (Makofi).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa Mhe. Dkt. Makame karibu.

Mhe. Dtk. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu na mimi niweze kuchangia kwenye ripoti kama ilivyo kawaida.

Kwanza kabisa nirejee kukushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na pili niipongeze hii kamati. Hii kamati kwa kweli imefanyakazi nzuri, wameeleza mambo mengi ambayo pengine mengine yalileta utata kidogo, yakielezwa maelezo na

Mwenyekiti alikuwa makini akatulia watu wakajadiliana, alipokubaliwa kuendesha akaendesha kama kawaida.

Halafu la pili naipongeza hii kamati kwa sababu imezingatia *gender*. Ukitizama hawa wako kumi na mbili, sita wanawake na sita wanaume. Kwa hivyo, hawa wote wameshirikiana kuleta kitabu hiki kizuri kabisa, narudia kuwapongeza. Sasa nikienda kwenye kuchangia, nasema haya ninayoyasema nimeyatoa au nimeyakokotoa kutoka kwenye maelezo ambayo ameyatoa Mwenyekiti alipokuwa anaeleza na mimi nilipokisoma hiki. Kwa kuanza nitaanza na Wizara ya Habari na mambo mengine yote yaliyomo kwenye wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwa mujibu wa maelezo habari ni muhimu sana katika kuelimisha, kuhamasisha na kurekebisha na mambo mengine. Lakini habari huambatana na lugha, unapotoa habari lazima utatumia lugha, ama Kiingereza au Kiswahili, Kichina, Kijerumani na kadhalika. Pia unaweza kutoa ile lugha ya kiashiria ambayo inaitwa lugha ya alama, pia hiyo inatumika katika kutoa habari.

Mhe. Naibu Spika, habari kwa kupitia lugha huwezesha utambulizi. Tunajua hata kama kuna chumba ndani kuna Mchina, hata akizungumza Kiingereza basi utamjua huyo ni Mchina, yaani ina- *express* ile *identity* ya mtu, yaani ukipata habari utajua, unakaa hapa unaeleza sisi hapa tuko Zanzibar na Wazanzibari wawili ama kwa simu au kwa *internet* wote wanajua kwamba hao ni Wazanzibari na wako Zanzibar. Kwa hivyo, tunarithishana mila zetu, desturi, utamaduni kupitia habari. Ukiangalia nyuma wazee wetu wamefanya nini tukisoma habari utajua walikuwa wanaishi vipi, walitumia majiti kulima au walitumia nini, ukiangalia sasa hivi tunajua *generation* hii ya sasa ikoje kwa kutumia habari. Ukiangalia pia mbele huko kwenye *future* tunajua huko, kwa habari tunajua kutatokea nini, kutakuwa na nini na vipi tukakabiliane na yatakayotoea.

Kwa ufupi, kujifanya jamii iwe ya kisasa iwe *up to date*, kwa kuweka tayari kuendelea kwa mujibu wa mahitaji ya sasa, yaani ile *modernization* na kumtayarisha mwanadamu kukabiliana na majanga au furaha au majanga. Maana yake unaweza kumueleza mtu habari ya furaha au ya majanga. Habari huleta amani utulivu, lakini pia chuki. Sasa kuna mtindo, upo zamani lakini sasa upo, kuna mtindo wa kupotosha habari. Jambo linafanyika vilivyo kwa kufuata sheria, kanuni na kila kitu lakini wengine wakapotosha habari watu wakaanza kubadilika mawazo na wakakosa imani na sehemu waliyokuwa wanaipenda kabisa moyoni.

Mhe. Naibu Spika, changamoto kubwa kwa watu ambayo inaweza kutoa cheche zile za moto, maana moto huanza cheche, inaweza kutoa cheche za ugomvi, cheche za matatizo ya kutokuelewana. Maana yake Wazungu wanasema, ugomvi huanza maneno, maneno huanza fujo, sasa zile fujo wanaziita *violent*, sasa *violent ex-connect violent.* Sasa inakuja mwisho wa *violence* tena inakuja vita. Sasa nashauri sana Wizara ya Habari, Utalii na Michezo, yaani wizara zinazohusika na usalama wa nchi, tuziangalie sana hawa wanaopotosha habari, hawawezi kupotosha habari tukawaachia. Hawa wakipotosha habari basi na sisi tuna vyombo vya habari tuyaeleze yaliyo ya kweli, kwa maana wasije wakatuweka mahali ambao kwa kweli hatutopenda tuwe. Ni vyema sana vyombo vya habari visishiriki katika kupotosha habari, kwa kueleza au kutoa taarifa ambazo hawana uhakika nazo au wana uhakika nazo ni za kupotosha, kwa hivyo wao watoe habari ambazo hazitapotosha. Sio vibaya kuwachukulia hatua wale wote wanaopotosha habari.

Aidha, changamoto za usafiri kwa sababu habari lazima uifuate huko iliko, uifuate uiandike upeleke. Bajeti inakusudiwa kupatikana habari, ni ule uhali wa bajeti finyu na uhaba wa wataalamu na vitendea kazi, basi hayo mambo yarekebishwe ili tuweze kupeana habari nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwenye habari basi naingia kwenye utalii. Utalii ni moja ya sekta zinazokuwa sana duniani. Uko utalii wa aina mbili, nadhani sote tunaujua utalii wa ndani wananchi wetu wanakwenda Makunduchi, Nungwe na kwengineko wanakwenda kuona na kusoma mambo yaliyopo na kuna utalii wa nje wageni wanakuja kutoka nje. Ili watalii waje kwa wingi hata hawa wa hapa ndani wafanye utalii kwa wingi, basi ni lazima tuimarishe vivutio vya utalii. Kama haya mahoteli basi yawepo yanayostahiki kwa aina zote za watu wetu.

Vile vile tuimarishe na vivutio vile vya asili, kama Msitu wa Kiwengwa una mapango ya kuvutia basi tuyaimarishe ili yazidi kuvutia, kama kuna *nature track* tutengeneze ili watalii wapite kwa urahisi

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiza dakika tatu.

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: Ooh! sawa. Basi kwa hivyo itabidi niruke niende kwenye michezo.

Michezo tunajua kuna George Wear, kuna akina Pele sijui nani hao, wote hawa walitoka katika jamii kwenye majimbo au kwenye vijiji. Huku katika majimbo yetu na vijiji vyetu kuna vipaji vingi sana vya michezo, tena michezo hii ya kisasa, kama, athletics pamoja na hizo karata na mabao na kadhalika, ni

michezo ya kiutamaduni, yote hiyo wapo watu wenye vipaji na ukiyakuza haya basi yanaweza kuleta furaha na kuleta utajiri na kila kitu, kwa sababu tunajua kuna baadhi ya wana michezo wamekua matajiri wamepata ajira. Kwa hivyo, naiomba sana Wizara yetu adhimu hii ya Habari iibuwe vipaji hivi kutoka vijijini, majimboni ili tuweze kupata wachezaji bora na wasanii bora watakaoweza kuiletea maendeleo Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, umeniambia dakika tatu, naomba nimalizie kwa kutaja vyama vya ushirika. Vikundi vya ushirika vipo vingi sana. Mtopepo pale sisi tuna vikundi havipungui 50 vya ushirika vilivyosajiliwa na vilivyokuwa havijasajiliwa. Kwa hivyo, nashauri sana hivi vikundi vinaweza kuchangia sana kuondosha umaskini. Kwa hivyo, naiomba Wizara husika ya Uwezeshaji wavipitie vikundi hivi na wavisome vizuri sana, wavipatie nyenzo ili viweze kufanyakazi wanayotaka kuifanya kwa ufanisi zaidi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakuheshimu sana sitaki niipoteze hata dakika yako moja. Kwa hivyo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Abdalla Ali Kombo. karibu mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia ruhusa yako.

Mimi Mhe. Naibu Spika, nitagusia kidogo kadhia ya mtoto wetu Ibrahim Abdalla. Mhe. Naibu Spika, katika taaluma zangu moja ni maendeleo ya jamii. Nathubutu kusema.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Abdalla Ali Kombo hili jambo bora ungeliachia kwa sasa, na umeona wajumbe wengi hawajalichangia na wewe tumia busara hiyo, hili jambo lisije likaleta mfarakano humu ndani ya Baraza. Hiyo ni busara yangu, sawa na limeshachangiwa sana limeshafahamika. Hiyo ni busara yangu, ungeliacha ukachangia vitu vyengine.

Mhe.Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nakuheshimu tu lakini leo unanionea, sawa. (*Makofi*).

Lakini labda nitowe neno moja tu, hilo naomba uniruhusu, neno moja tu kwa wizara hii. Naomba wizara ifahamu na ifanye biashara ambayo ina wateja

katika soko lake. Ninachotaka kuzungumza hapa Makunduchi asilimia 99 hawatumii kenge, lakini soko la kenge hapa Unguja lipo.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye utalii ambao upo kwenye ukurasa wa 10, umezungumzwa habari ya mapato na kamati ina wasi wasi sana kwamba mapato kidogo hayapatikani vizuri. Kwa hivyo, mimi ningewaomba wahusika kama leo au mwezi wa Septemba, waje watusaidie idadi ya watalii wanaoingia Zanzibar sio wageni watalii, kuanzia mwaka 2012 mpaka 2016, watalii sio wageni idadi yao.

Halafu naomba atakayehusika au anayehusika atutajie aina za hoteli, nyota ngapi, nyota nne, nyota tano. Hao watalii wanaokuja katika hoteli hizi ni wangapi walikaa pamoja na pesa zao. Mhe. Naibu Spika, katika ulimwengu wa kisayansi kuambiwa tu watalii wengi, ndege zimeingia nyingi, safari za uwanja wa ndege nyingi hazitusaidii. Tunachotaka sisi kujua pesa ambazo zimeingia katika nchi yetu. Kwa hivyo, naomba sana muhusika anayekuja atuambie nyota tano ya Kiwengwa kuna watalii kadhaa wamekuja na Dola ni kiasi gani. Hii itatusaidia Mhe. Naibu Spika, kujua ni aina gani ya hoteli katika nchi yetu inapendwa na tuifanye, badala ya kwenda kujenga vituturi kila pahala ambavyo havina maana, basi naomba suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, msione tabu kutaja pesa ambazo tunazipata zetu na bajeti tunapitisha hapa. Wenzetu Bara kila kitu wanataja, tunapata hiki na hiki. Uwanja wa Taifa kulikuwa na Simba na Yanga juzi, sijui kama leo au kesho utasikia pesa zimepatikana hizi. Kwa nini sisi tunakuwa wagumu kutaja pesa ambazo tunazivuna katika nchi yetu. Hapo nimemaliza.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nakuja tena kuna wafanyakazi ambao walikuwa ni wa Hoteli ya Bwawani, wengi wao ambao ni wastaafu wanalalamika kuna haki zao hawakupewa. Sasa nawaomba wahusika kama kweli ziko basi watafutiwe ili tuwasaidie, hali yao kimaisha sasa hivi sio nzuri.

Mhe. Naibu Spika, nakuja tena kwenye mambo ya redio. Mheshimiwa redio zetu nyingi za *FM*, mimi ni msikilizaji mzuri sana wa redio. Kuna vipindi vizuri tu vya wazee kama sisi, wanasema zilipendwa, wazee wakumbukwe, hizi nazo ndizo. Humo utapata vitu vingi, hasa baada ya kanyakanya kama hii. Hapa Unguja nakumbuka kulikuwa kuna Mkude Ngoma, Sokomile Tulivu, Kibakora, Msondo Ngoma, Sokomoko. Sasa redio hizi sasa hivi wenzetu wamechukua wateja wengi sana. Sisi tumebakia na kile kipindi cha ngoma za Kimanga siku ya Alhamis, toke enzi hizo na hizo. Sasa wikiendi zote wenzetu wote sasa hivi wanakwenda kwenye *FM*. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naomba Redio Zanzibar na sisi tuwe na kipindi ambacho wazee watakaa kitako wakumbuke nyimbo kama hizi. Nafahamu kwamba wengi wetu, hasa hawa vijana ambao wako kwenye Redio Zanzibar umri wao ni mdogo sana hawakumbuki hizi nyimbo, lakini kwetu sisi ni muhimu sana. Kwa hivyo, namuomba Waziri na watendaji wake wote tuwe na kipindi na sisi *week end* ambacho tutaburudika na kusahau kanyakanya kama hizi unazoniambia nisizungumze. *(Makofi).*

Jengine Mhe. Naibu Spika, Gazeti la Zanzibar, kuna kitu kinachosha. Maana ingekuwa chakula mtu angesema basi. Vikatuni kwenye gazeti ni ujumbe tosha ni *message* na magazeti yote huwa yana vikatuni. Sasa tatizo la Gazeti la Zanzibar muna bingwa mule, bingwa huyu huwa hana mpya. Wiki nzima ujumbe ndio huo huo, mwaka mzima ujumbe ndio huo huo. Mimi nina ombi langu, kama hawana kikatuni, hawana ujumbe wafute. Ujumbe ni kitu muhimu sana, nazungumza tena wale ambao kidogo umri wao umekuja juu, kulikuwa kuna ujumbe wa akina Polo, Bushiri, Chakubanga mpaka leo tumefanyia kazi. Lakini bingwa huyo, nakupenda kama sikudanganyi, hiyo hiyo mwaka mzima. Kwa hivyo, naomba kama hawana ujumbe mwengine, hii Mhe. Naibu Spika, waondoshe hiki kipindi.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimpishe Mhe. Rashid Waziri wa Habari, Utalii na Michezo ili atowe ufafanuzi kidogo.

Waheshimiwa Wajumbe, tunajua kwamba masuala yetu mengi tuliyoyauliza yatajibiwa mwezi wa Septemba. Kwa hivyo, Mhe. Mawaziri kwa ufupi tu watatoa ufafanuzi, lakini majibu halisi yatakuja kutoka mwezi wa Septemba. Kwa hivyo, tumpe nafasi mheshimiwa aeleze yale ambayo anahisi ni muhimu kwa wakati huu kuyaeleza. Mheshimiwa karibu sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru wewe kwa muongozo ambao umeweza kutuelekeza.

Lakini mimi pamoja na wizara yangu, watendaji wote, uongozi pamoja na wahudumu katika sekta zote napenda kutoa shukrani zetu za dhati kabisa kwa kamati ambayo hapo zamani ilikuwa inajulikana ni kama Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi. Lakini sasa pamoja na jina jipya la Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii naishukuru sana kwa kazi yao kubwa waliyoifanya na kwa mashirikiano makubwa ambayo

na sisi wametuonesha mpaka kufikia leo kuwezesha kuwa na taarifa hii ambayo imewasilishwa.

Vile vile tunawashukuru sana wachangiaji wote ambao wamefika karibuni 17 waliochangia Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Vile vile siwezi kusahau kumshukuru sana Mhe. Spika pamoja na uongozi wake kwa kuiongoza Kamati na kuweza kufanya kazi zao kwa utulivu kabisa, kufuatilia kwa kina na hatimae kutusaidia sisi kutupa michango ambayo itatupa hamasa na kutuelekeza katika kusimamia vyema majukumu yetu ambayo yanatukabili siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika nafasi hii uliyonipa sikusudii kujibu hoja, kwa kweli michango iliyotolewa ipo michango ambayo ni ushauri, yapo masuala yenye kutaka majibu, yapo mambo yenye kutaka kufahamishwa na kwa wakati huu kama tungeweza kuyafanyia kazi hizo basi natumaini kwamba ingekuwa ni muda mrefu unaohitajika kufanya kazi hiyo. Lakini kwa vile umetupa fursa na sisi kuchangia yale muhimu basi na mimi naomba kuungana na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopita nyuma kuweza kuwaambia Wajumbe kwamba majibu kamili michango yao waliyoitoa, maelekezo kamili kwa michango yao waliyoitoa na yale yote yaliyotolewa kama ni masuala basi yatapata majibu yake ifikapo Septemba mwaka huu wa 2017/2018.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ilikuwa nieleze machache tu katika kutoa ufafanuzi wa mambo mengi ambayo yalichangiwa, na ufafanuzi wangu nitaupeleka katika mtindo ule ule wa muundo wa Wizara. Kuna mambo mengi yaliyochangiwa kwenye sekta ya habari lakini kwa ufupi wake kulikuwa kuna mambo mawili matatu ambayo yaligusiwa sana katika suala zima hili la habari. Suala kubwa ilikuwa ni wafanyakazi waliopo katika Kitengo cha Habari kule Dar es Salaam inaonekana kwamba wafanyakazi kule wapo wachache na ni kweli pengine maslahi wanayopewa kule yanalingana na mwenendo wa *ZBC* ya Zanzibar. Lakini vile vile wafanyakazi wale wana uchache au hawana usafiri wa kudumu wa kufuata zile habari ambazo kuzitafuta habari ndio kuendeleza Wizara yetu hii kupata habari nyingi zinazotoka upande wa pili.

Nataka niwaambie kwamba Wizara imo katika jitihada ya kulibadilisha Shirika kama walivyoshukuru wengi kama walivyotoa faraja wengi kufarajika na mwenendo wa mabadiliko yanavyokuja hivi sasa *ZBC*, mambo haya yote kwa kifupi chake tumeyazingatia na natumaini Wajumbe wenzangu ndio watakuwa wapitishaji wa bajeti itakayofuata siku chache zijazo ya mwaka 2017/2018. Kwa hivyo ni vyema wakaona ufinyu wa bajeti tuliokuwa nao hivi sasa na wakaweza kututilia mkazo bajeti ijayo ili mambo haya yawekwe sawa. Sisi

kama wasimamizi tutasimamia bajeti ambayo wataipitisha na kwa kile pale patakapopangiwa kufanyika mambo haya basi tutayafanya kwa ukamilifu wake.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hata sisi tunaona kuna umuhimu huo habari za Dar es Salaam kupatikana sambamba na habari zinazotokea huku, ile ni Tanzania moja ni sehemu kubwa sana ya nchi zaidi ukilinganisha na nchi yetu. Kwa hivyo habari zake zinahitajika kwa upeo vile vile, kama tunavyoendeleza kufanya Shirika letu kuwa bora zaidi ndivyo tutakavyokwenda sambamba kufanya kitengo kile kilichokuwa Dar es Salaam nacho kuwa bora zaidi na kifanye kazi vizuri zaidi.

Nizungumzie suala zima la magazeti, ni kweli kwamba wafanyakazi sehemu wanayofanyia kazi hivi sasa mazingira sio mazuri na utendaji kazi. Lakini nataka niwathibitishie katika kipindi kifupi wajumbe wenzangu kwa jitihada kubwa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayofanya kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Micheo hivi karibuni wafanyakazi wetu watapatiwa jengo lao lenye mazingira mazuri na sehemu ile inaweza ikatumika katika hayo mambo ambayo yamechangiwa na yamependekezwa.

Kuhusu vifaa vile vile tunaishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuliona hili si upande wa gazeti, lakini vile vile hata *ZBC*, Serikali imeona kwa jicho la huruma imeweza kutupatia vifaa vingi sana vipya ili tuweze kubadilika na natumaini katika kipindi kifupi kijacho Waheshimiwa Wajumbe wananchi kwa jumla wataona hayo mabadiliko.

Kwa upande wa uchapaji wa gazeti letu kweli bado tunaendelea kuchapa gazeti letu Tanzania Bara, lakini kwa mazungumza tunayoyafanya kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais basi tunaweza kutumia muda wowote vifaa na zana za kisasa ziliopo hapa kwetu Zanzibar na ni azma ya Serikali yetu kuhakikisha kwamba Gazeti la Zanzibar Leo ambalo limeonekana lina muono unaobadilika hivi sasa litachapwa hapa Maruhubi, hapa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mchango mkubwa umetolewa kwenye utalii lakini kwenye utalii kumeonekana kuna masuala na kuna mambo ambayo yanahitajika maelekezo kidogo, imeonekana kwamba mapato yanayokusanywa kwenye utalii ni machache. Lakini nataka niwaeleze wazi Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuunga mkono kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliyoitoa jana. Mhe. Rais wa Zanzibar jana alieleza kwamba kipindi alichoingia yeye mapato yalikuwa yapo katika wastani wa bilioni 14 lakini hadi mwaka huu mapato yapo kwa wastani wa bilioni 45 na tunaendelea mbele kwa mwezi. Makusanyo

haya yote yafahamike kwamba kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na sekta ya utalii.

Lakini sekta iliyoelezwa hapa na mapungufu yaliyoelezwa hapa yanaonekana kwamba Wajumbe hawajaweza kuchanganua vizuri ujumla wa makusanya ya mapato yanayotokana na utalii. Namshukuru sana Waziri wa Fedha katika masuala mengi anayojibu hapa mbele yetu huwa anatoa mchanganuo kwamba mapato ya utalii yanaweza yakakusanywa kupitia *VAT* ambayo yanakusanywa kwa taasisi ya *ZRB,* yanaweza kukusanywa kwa kupitia njia ya *Hotel levy* ambayo yanakusanywa kwa *ZRB* na yale mapato ambayo yanakusanywa na Kamisheni ya Utalii basi yale ni mapato yanayotokana na ile *fee* ndogo ndogo, inawezakana kuwa ni ada za leseni ndio zinazokusanywa pale, vibali vya kutembezea wageni ndio vinavyokusanywa pale. Kwa hivyo ndio maana hapa inaonekana idadi ya mapato kutoka utalii yanaonekana machache. Lakini kwa ujumla wake mapato ya utalii yanakusanywa kupitia sekta nyingi sana. Mapato yanakusanywa Serikali za Mitaa, yanakusanywa kupitia vyombo vyetu vya ukusanyaji kodi na kwa ujumla wake mapato hayo hivi sasa ndio tegemeo ambayo tunayategemea hapa kwetu.

Kuhusiana na suala zima la kuongezeka kwa watalii na kupungua kwa watalii. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hivi sasa utalii Zanzibar umekua. Kipindi cha miaka mitano iliyopita utalii ulikuwa unaweza kufikia wageni wanaoingia hapa nchini idadi ya laki mbili mpaka laki mbili na hamsini, lakini hivi sasa watalii wanaoingia nchini ni watalii laki tatu na sitini kwa hesabu ya mwaka jana. Hilo ni ongezeko kubwa ukilinganisha na lengo tulililoliweka kwa mwaka 2020 kufikia idadi ya watalii laki tano. Ni wazi kwamba kwa kasi tunayokwenda nayo idadi ya watalii laki tano kwa kuliongezea pato la nchi yetu watafikia kabla ya mwaka 2020, Mwenyezi Mungu atusaidie mipango iende sawa kwa hili.(*Makofi*).

Vile vile katika utalii kulikuwa kuna malalamiko makubwa ya kuonekana kwamba wanyonge ambao wanafanya biashara na mahoteli yetu haya, basi hawa kuna kunakobadilishwa uongozi wa utalii, wale ambao wana madeni unapoingia uongozi mpya madeni yao hayalipwi. Wizara inafanya jitihada hizo kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanahusika na biashara za utalii wanatakiwa kunufaika na utalii kwa wote, na kwa jitihada tunazozichukua tunawahakikishia wajumbe kwamba tuko pamoja na wale wanaofanya biashara hususan *suppliers* na kwa muda mfupi kamati iliyoundwa ya kuwashughulikia wafanya biashara wanaofuatilia madeni yao basi itakomboa masuala yote yale ambayo yanaonekana ni matatizo katika biashara wanazozifanya.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikizungumzia suala la utamaduni lakini kabla ya hilo labda nizungumzie kidogo suala la *package tour*. Inaonekana suala hili lilikuwa linaonekana kwamba linapoteza sana mapato, lakini nataka niwahamishe na nichukue fursa hii kutoa maelezo kwamba mfumo wa *package tour* ni mfumo wa mwanzo ambao tumeutangaza kwenye utalii wetu, na kwa mtazamo mfumo huu unaweza kuwa unachangia mapato mengi zaidi kutokana na kodi iliyowekwa. Hivi sasa wale wote wanaokuja kwa *package tour* wamewekewa kulipa Dola tisa kwa mgeni, ukitizama kodi hii inaweza ikawa kubwa katika ukusanyaji wa mapato kuliko yule ambaye anasajiliwa kwenye kodi ya *VAT* akalipa kwa asilimia kumi na nane lakini bei yake ikiwa ndogo zaidi ya kufikia zile Dola tisa.

Hivyo nataka niwathibitishie wazi kwamba *ZRB* wako mahiri katika kuliona suala hili, suala hili limefanyiwa utafiti tangu miaka ya 1990, limefanyiwa utafiti mnamo mwaka wa 2007 na hatimae wameweza kuja na mbinu kuhakikisha kwamba wapo watalii ambao watatozwa kodi kwa kutumia hii kodi ya *Fixed* na wako watalii ambao wanawezwa kutozwa kodi kwa kutumia *percent* . Kwa hivyo ni vyema sasa hivi kweli *ZRB* ikashirikiana na kitengo chetu cha Kamisheni ya Utalii, Wizara ya Habari Utalii, Utamaduni na Michezo kulipitia tena suala hili kuona namna gani Serikali inaweza ikabana mapato zaidi.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba sana nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na mambo ya utamaduni. Kama nilivyosema sikusudii kujibu hoja lakini ningependa kujibu yale ambayo yanaonekana kidogo yalikuwa yanachangia yote kwa upande mmoja yanagusa hapo, na yanaonekana kwamba kama ni kikwazo. Kwa maana hii Mhe. Naibu Spika, si vibaya sasa basi ukaiomba hii Ofisi yako ikashirikiana tena na Bodi ya Mapato ikaweza kuwapa semina Wajumbe wakajua namna gani mapato ya utalii yanaweza kukusanywa na namna gani Kamisheni yetu ya Utalii inavyoweza kutoa nayo taaluma kwa kushirikiana na *ZRB* kujua namna gani utalii unakuzwa.

Kama nilivyosema mwisho kabisa ilikuwa nizungumzie suala la utamaduni, imezungumzwa hapa kwamba mambo ya kale yanaonekana kupotea, magofu mengi sasa hivi yanayoyoma lakini vile vile kuna masuala mazima ya makumbusho ambayo nayo yanaporomoka. Nataka niseme kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imeona umuhimu wa vivutio vya utalii hapa Zanzibar. Moja katika vivutio vikuu vya utalii tunakiri kwamba ni haya mambo ya kale, jitihada zinafanywa kubwa sana kuhakikisha kwamba yale majumba ambayo yanavutia watalii hususan yale ya kifalme na ambayo yamo

katika hifadhi ya Mji Mkongwe, tunakamilisha taratibu za kukubaliana na Mji Mkongwe ili majumba yale yapate ruhusa za kutengenezwa.

Lakini kwa majumba yaliyokuwepo maeneo ya nje ya mji na mengine yaliyokuwepo Pemba kama Mkamandume yaliyotajwa, basi tatizo ni lile lile tu la ufinyu wa bajeti, lakini kwa pale bajeti zitakaporuhusu basi Kamisheni kwa kupitia Wizara hii ya Habari Utalii, Utamaduni na Michezo, Kitengo chetu hichi cha Utamaduni, Mambo ya Kale kitatumia jitihada zake zote kuhakikisha kwamba inarejesha haiba zile za makumbusho.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamezungumzwa lakini kama nilivyosema huu si wakati wake mkubwa sana wa kusema kwamba sasa hivi nichukue nafasi hii nitoe majibu ya hoja baada ya hoja, lakini kama nilivyokuomba bado Wizara nayo inaona ina umuhimu kuona kwamba kwa vile Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ina sehemu kubwa ya mchango wa pato la nchi hii, basi si vibaya kabisa tukapata hata semina ya kuweza kuwajuilisha Wajumbe wetu wakaweza kuyafahamu haya mambo kwa upeo wake. Lakini kwa yale yote ambayo yatahitajika kujibiwa kwa mwezi wa Septemba na kuelekezwa kwa mwezi wa Septemba majibu yake tutayatolea huo mwezi wa Septemba. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa yote hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumebakiwa na wachangiaji wawili yaani Waziri pamoja na Mwenyekiti, na nahisi muda hautotosha hivyo naomba nimuombe Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili,

Wajumbe: Muda bado upo.

Mhe. Naibu Spika: Haya tunaendelea basi.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kwanza nichukue sana nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kusema bwana apewe sifa. Na pia napenda nimshukuru Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein ambaye wenzetu wana majimbo lakini sisi tuna jimbo la uteuzi, kwa nafasi aliyotupa kwa uteuzi aliamini tutafanya kazi ya kumsaidia na tulikuwa tunajitahidi kufanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo mpaka pale Mungu atakapoona kwamba inatosha.(*Makofi*).

Napenda nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ambaye amekuwa karibu katika kutuelekeza mambo mengi kila tunapohitaji hasa kwa Wizara yangu ambayo ni nyeti sana, pia na Waziri wangu msaidizi ambaye mara nyingi nikiwa sipo anakuwepo Mhe. Mohammed Aboud ambaye imetokezea siku hizi imetokezea wengine wanamtania mama Castico, sio mama Castico yeye ni Mhe. Mohammed Aboud.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia Mawaziri waliochangia, wananchi wasiklizaji na sisi sote tulioko humu tunajua yote haya tunafanya kwa nia nzuri na Mungu aendelee kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, nimepata Wajumbe waliochangia kama nitakavyowataja wanafika kumi na sita kama ifuatavyo.

1. Mhe. Jaku Hashim Ayoub Jimbo la Paje.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa huna haja ya kutaja majina ya wachangiaji wote.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Unasema sina haja!

Mhe. Naibu Spika: Huna haja ya kutaja majina ya wachangiaji wote ni kutoa maelezo tu au ufafanuzi wa yale ambayo waheshimiwa wameyazungumza.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Sawa nashukuru basi nimechangiwa na Wajumbe kumi na sita, naomba niwashukuru sana kwa michango yao ambayo imekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wizara yangu, na ninaamini yote waliyochangia yatatusaidia na tutayafanyia kazi na kwa kuwa majibu mengi yanatakiwa mwezi wa Septemba, ni kwamba mwezi wa Septemba tutakuwa tumejipanga vizuri na Mungu akituweka salama tutakuwa na majibu mengi ya kutosha yenye vidhibiti na uhakika wa mambo mengi.(*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Niabu Spika, katika suala lililozungumzwa mwanzoni kama lilivyo hatuwezi kusema kitu kwa sababu liko Mahakamani. Pia jambo la pili lilikuwa limezungumzwa la mtoto kubakwa katika nyumba ya watoto ambalo nalo lipo Mahakamani, ni bahati mbaya tu kwamba mazingira yaliopo katibu na nyumba ya watoto ndio yaliyosababisha vitendo hivyo kwa sababu watu wananunua matunda jirani wamefikiwa katika mazingira hayo. Ningependa

sana kuwaambia wananchi kwamba wawe bado na imani na nyumba ya kulelea watoto kwa sababu ndio nyumba pekee ambayo iko chini ya mamlaka ya Serikali na itawalinda siku zote za maisha ya Serikali zilizoko.(*Makofi*)

Lakini pia nataka kuwahamasisha kwamba hivi karibuni tutaweka kapu la kupokea watoto pale nje, kwa sababu watoto wengi wanaonyesha bado wanakuwa *displace* lakini wakipata mahali pa kuwekwa, wengine wanaona haya kuwaleta watoto mahali pale, patakuwa na kapu la kupokelea watoto kwa siri. Kwa hivyo ukiona unakereka na mtoto nyumbani usimuache akahangaika mlete pale na atapokelewa na atatunzwa katika hali ya uzima.(*Makofi*).

Mheshimiwa kuna masuala mengi yamechangiwa ambayo nahisi kwamba yataletwa siku nyengine. Lakini pia kulikuwa na suala la pencheni. Mhe. Naibu Spika, juhudi zinafanyika na bahati nzuri haya waliyochangia Wajumbe tumeyaona hasa baada ya kuanza kulipwa. Siku zote suala linapohusiana na pesa watu wanapoteza uaminifu. Lakini pamoja na maagizo ya Mhe. Rais siku aliyokuwa anafanya Pemba ya Siku kuu ya Sherehe ya Wazee aliagiza hili suala. Suala hili liko mikononi mwa wakaguzi wa hesabu kutaka kutusaidia jinsi gani tunaweza kuboresha suala hili. Ongezeko lao kwamba wanaongezeka kila siku wanakufa nayo pia taarifa zipo. Tutawaleteeni kwa uzuri zaidi tutakapokuwa tumepata kuweka salama.

Masuala ya ujasiriamali tunayapokea na tutayashughulikia na tumeyapokea vizuri mijadala iliyokuwepo na tutaendelea kuyafanyia kazi na kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Wizara ya Biashara pamoja na Wizara zote zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, suala la ajira mahotelini ni suala ambalo linafanyiwa kazi. Hivi sasa wizara ipo katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na *data base* na kunakuwa na taratibu na sheria maalum itakayohakikisha kwamba inalinda ajira ya mtoto wa Kizanzibari. Mikataba hiyo itawekwa wazi kwamba ajira zote zitakazokuwa zinaanzishwa nchini ni lazima kuna nafasi maalum ya watoto ambayo wanapaswa vijana ipo katika Sheria Nam. 16 ya mwaka 2013. Nataka wananchi watoe hofu kwamba suala hili linafanyiwa kazi na ni suala la kisheria linakubalika dunia nzima. Lipo katika suala la *apprenticeship* ambalo ni *ILO* na tayari tumeshaanza kufanya utafiti bahati nzuri linaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna suala linalohisiana na mishahara ambalo walidhani kwamba wamehamishwa kutoka Wizara ya Afya lakini wamekuja wizarani kwetu, ni kwamba hii mishahara inaingia kwenye mishahara yao moja

kwa moja pamoja na maposho yao kwenye mishahara. Inawezekana hawajayafatilia vizuri wakajua kwamba tayari wanalipwa.

Mhe. Naibu Spika, suala la Baraza la Vijana, bajeti iliyokuwepo ya mwanzo ilikuwa ni kwa ajili ya kuanzisha Mabaraza. Sasa hivi Wizara inafanya inafanya jitihada ya kuhakikisha kwamba vijana wanapangiwa mpango maalum wa kuanza kupewa misaada kama ni mikopo na kuanzisha *program* itakayofaa. Nitawaombeni sana mtakapokuja kwenye bajeti mtuongezee, Wizara yetu inahitaji pesa nyingi sana hasa kwa vijana. Vijana hawa Waheshimiwa nadhani wanatoka majimboni mwenu, tushirikiane pamoja katika kuwasaidia.(*Makofi*)

Kwenye masuala yanayohusika na udhalilishaji wa watoto. Kama nilivyokwishakusema suala hili la udhalilishaji wa watoto sio la Mhe. Castico, wala sio suala la Mhe. Rais, wala sio la Serikali ni suala la tabia ya wananchi wenyewe. Wananchi wakikubaliana kuacha suala hili hakutakuwa na sababu ya kesi wala hakutakuwa na mambo yoyote yale. Hata haya masuala tunayoyazungumza ya *DNA* inawezekana ikawa hakuna sababu. Kwa sababu masuala ya upotevu wa ushahidi hata kukiwepo *DNA* itatunzwa na binadamu. Lakini kwa kuwa kuna umuhimu wa kuthibitisha ni suala ambalo litachukuliwa, tutalipeleka na majibu yatakuja kipindi kitakachofaa.

Mhe. Naibu Spika, hapa hapa napenda nitoe wito kwa akina baba, wabakaji wanaobaka ni wanaume, hakuna mwanamke aliyekwenda kubaka akasema wanawake kadhaa wanabaka. Kwa hivyo nawaombe wanaume kokote mliko mnakonisikiliza hebu anzeni Chama cha Wanaume muwajadili wanaume wenzenu wanaobaka mpaka watoto wachanga. Mtoto mchanga wa miezi sita anabakwa mpaka anakufa, mnatafuta nini? Mnasingizia nguo kwenye pempasi kuna nguo gani. Mambo yapo kwenye akili hapa, tukishinda ufahamu wetu tutaweza kudhibiti hayo mashawishi mengine. Naomba Mhe. Naibu Spika, Chama cha Wanaume kianzishwe, wakae wajadili kokote watakapokuwepo. Hata tukipanga kitu gani madamu hawajataka kubadilika hatutoweza kufanya kazi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la Marehemu Omar ambalo suala hili lilitokezea kwa *accident* limefuatiliwa na Wizara. Bahati nzuri ameshalipwa milioni tisa na laki tisa na bado linafuatiliwa kuhakikisha kwamba ajali ilitokezea mwaka 2016, Kampuni imelipa fidia ya gharamia kwa milioni hizo tisa na laki tisa, na wafanyakazi wengine walioumia wamepewa matibabu na taratibu nyengine za kisheria zinafuata na kuhakikisha kwamba kampuni inakuwa na bima ya magari.

Mhe. Naibu Spika, kwenye suala la Welezo na suala la makaazi ya wazee wetu. Welezo inatunzwa na watu wengi ambao wanatoka nje, ambao kuna ma-*sisters* wapo pale. Bahati nzuri wanajitahidi sana kufanya kazi kwa bidii. Kama walivyoona Waheshimiwa wenyewe wanaweza kukubali kwamba jitihada inayofanyika ni kubwa. Suala la Limbani wametolewa kwenye jengo la zamani sasa hivi wamepelekwa kwenye jengo jipya. Kwa hivyo masuala ya ukarabati bado yanaendeleo na bahati nzuri napenda kusema kwamba tayari wameshajengewa wigo.

Mhe. Naibu Spika, na kuhusu suala la kusema wazee wanapewa *diet* mbaya. Nataka kusema tu kuwatia moyo watu wasichoke kwa sababu inawezekana kuna wazee wengine wapo majumbani wanawacha kuja Sebleni wakaona hawalishwi. Hapa Mhe. Naibu Spika, asubuhi wanakula milo mitatu kwa siku; asubuhi wanakula mikate, chai, siagi na mayai. Siku ya pili ya asubuhi wanakula uji na maandazi, mchana wanakula vyakula mchanganyiko, wali siku tatu, mseto siku moja, ugali siku moja na vyakula vya matunda, mihogo, ndizi siku mbili kwa wiki. Vyakula hivyo huambatana na samaki, nyama, kuku kwa baadhi ya siku mboga mboga na matunda mengine.

Mheshimiwa kama hili halijatimizwa nitalifuatilia kwa ukaribu na nilete taarifa inayofaa zaidi. Kwenye suala la pencheni…

Wajumbe: Mhe. Naibu Spika, muongozo wako tunaomba.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf: Hata wanawake wanabaka hivyo hivyo sio wanaume peke yao.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Kamati imesema kwamba wale watu hawapewi chakula kizuri ndiyo walichokisema. Sasa Mheshimiwa inaonyesha unakana maneno ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa ungelitumia busara ukahakikisha kwanza hayo unayoyasema, kwa sababu Kamati imeyasema leo leo na wewe unayasema leo leo, ili kuondosha sitofahamu Mheshimiwa hilo nenda kalifanyie uchunguzi.*(Makofi).*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa Kanuni ya 63, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tumeshalimaliza hilo, Mheshimiwa anaendelea na jengine. Mhe. Hassan, Mhe. Hassan ...

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kuhusu utaratibu..

Mhe. Naibu Spika: Aaa! kuhusu utaratibu sitaki, nimeshalimaliza nimemwambia Mheshimiwa aende akalifatilie hilo...

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Tumeundiwa Kanuni tuzitumie Barazani Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimesemaje kuhusu utaratibu mnachokisema Mhe. Nadir kasema kwamba Waziri anachokizungumza sio sahihi. Ndio utaratibu ambao mnautaka nyinyi si ndio? Ninachokisema nimemwambia Mhe. Waziri wa Wanawake kwamba kauli yako inapingana na kauli ya Kamati ndivyo nilivyosema. Na nimemtaka Waziri aende akafanye uchunguzi tena arudi na taarifa sahihi. *(Makofi)*

Sasa hapa pana tatizo gani, nimemtaka..Waheshimiwa Wajumbe mkae mkijua Kiti kina uwezo wakumwambia Waziri, Waheshimiwa wajumbe nisikilizeni. Nataka mnisikilize tena kwamba Kiti kina uwezo wa kumtaka Waziri atoe maelezo sahihi. Na mimi hicho ndicho nilichomtaka. Nimemtaka Waziri atoe maelezo sahihi ndicho nilichomtaka hakuna tena mjadala hapa, aendelee Waziri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa nilichokuwa nnasoma hapa ni *diet* ambayo tunategemea wazee wetu wapewe. Nimesema baada ya hapo tutafuatilia kwa ukaribu na nimeshaisifu sasa, Wizara kwamba imetusaidia kuweka mambo wazi tumelipokea na tutalifanyia kazi.

Waheshimiwa Wajumbe: Aaah!(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Endelea endelea, endelea na kitu chengine.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niombe nishukuru kabisa Kamati na kwamba nina kamati nzuri sana ambayo ina watu wengi ambao ni wakereketwa ambao wataendelea kutusaidia na sisi kwa siku zijazo, hatutotakwa kuulizwa hayo isipokuwa tutafanya vizuri na ushirikiano wao nitakuwa pamoja 100% ninapokuwa sipo ni bahati mbaya tu!

Ahsante kwa ushirikiano wako. *(Makofi).*

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo katika kupitisha taarifa yetu hii ya Kamati ambayo kwa bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imechangiwa na Wajumbe 40, kati ya hao kumi na tisa wamechangia moja kwa moja na ishirini na moja wamechangia kwa maandishi. Nachukua fursa hii Mheshimiwa kuwapongeza kwa dhati kabisa, naamini kwamba uchangiaji wao umeleta uimara katika utendaji wetu wa kazi kama wajibu wetu kazi yetu kuungana kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Naomba niwataje kwa ruhusa yako. Waliochangia moja kwa moja ni:-

1) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
2) Mhe. Miraji Khamis Mussa
3) Mhe. Nassor Ali Jazira
4) Mhe. Ali Salum Haji
5) Mhe. Abdalla Maulidi Diwani
6) Mhe. Suleiman Saharan Said
7) Mhe. Simai Mohammed Said
8) Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
9) Mhe. Omar Seif Abeid
10) Mhe. Hidaya Ali Makame
11) Mhe. Hassan Khamis Hafidh
12) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
13) Mhe. Rashid Makame Shamsi
14) Mhe. Asha Abdalla Mussa
15) Mhe. Masoud Abrahman Masoud
16) Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
17) Mhe. Abdalla Ali Kombo
18) Mhe. Rashid Ali Juma (Waziri wa Habari, Utalii,Utamaduni na Michezo)
19) Mhe. Moudline Cyrus Castico (Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Waliochangia kwa njia ya maandishi:-

1) Mhe. Saada Ramadhan Mwenda
2) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
3) Mhe. Ussi Yahya Haji
4) Mhe. Said Omar Said (Karatu)
5) Mhe. Riziki Pembe Juma

6) Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
7) Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
8) Mhe. Suleiman Ali Makame
9) Mhe. Ame Haji Ali
10) Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
11) Mhe. Shamata Shaame Khamis
12) Mhe. Bahati Khamis Kombo
13) Mhe. Tatu Moh'd Ussi
14) Mhe. Khamis Juma Mwalim
15) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
16) Mhe. Mgeni Hassan Juma
17) Mhe. Maryam Thani Juma
18) Mhe. Zaina Abdalla Salum
19) Mhe. Mihayo Juma N'hunga
20) Mhe. Ali Khamis Bakari
21) Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati - Salha Moh'd Mwinjuma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya mahojiano mazuri na taarifa nzuri ya Waheshimiwa Wajumbe mimi nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza zima la Wawakilishi kuanzia Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Mnadhimu wetu, Mwanasheria wetu, Mheshimiwa Mkuu wa Shughuli za Serikali Makamu wa Pili wa Rais, kwa hali halisi iliyojitokeza katika Baraza hili nimeridhika na nimeamini, kwamba Kamati ilifanya kazi yake kilillahi taalla na ilifanya kazi kwa uwezo wake wote, ilifanya kazi mpaka usiku wa manane haikujali wakati. Lakini lengo na madhumuni ni kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kutokana na Kanuni zetu na taaratibu zetu.*(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nafikiri mengi Waheshimiwa Mawaziri wameyajibu, sisi kama Kamati tutangojea mwezi wa Septemba, yatayokuja hapa tutashirikiana nayo. Lakini pamoja na hayo niseme kwamba kubwa ninaloliomba mimi kupitia Kamati yetu ushirikiano katika wizara zetu.*(Makofi).*

Mheshimia tulokuwemo humu mote wote Wawakilishi wote wa vyama vyote, tuko baba mmoja mama mmoja, lengo letu kujenga, lengo letu kuelezana. Kwa hivyo Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anapokwenda pahala kutafuta kazi asionekane adui. Na aniamini kwamba Mheshimiwa anapokwenda kutafuta kazi wewe Waziri anakupunguzia, kwa sababu mimi wajibu wangu nikilipata siyo nije nilitowe hapa nikueleze kwanza huko ili wewe upate faraja ya kulifanyia kazi vizuri. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza zima tuwe na uwiano tuwe na kazi ya pamoja, lengo letu kujenga si kubomoa. Ninaloliomba Mhe. Naibu Spika, kwa kuendeleza hili, kuna mambo mawili matatu kwa ufupi sana Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba niseme kwa ajili ya kuweka sawa shughuli zetu hizi.

Mhe. Naibu Spika, nimetanguliza la kwanza mashirikiano, la pili ninaloliomba yale yote yaliyozungumzwa na Wajumbe ambayo tunayo yote tutayafanyia kazi kama Kamati na kuyafanyia kazi ni ripoti ije hapa. Waheshimiwa Mawaziri tutashirikiana kuhakikisha michango ile isipotee bure, kwa sababu tunategemea yaje yajibiwe hapa ili wale wenzetu isiwe kama wamepoteza muda wao bali walikuwa katika kazi inayostahiki.

Mhe. Naibu Spika, jengine watendaji wetu wa Mawizara wao ndiyo roho katika nchi yetu na wao ndiyo roho ya kuwasaidia Mawaziri, siridhiki kumuona mtu fulani akiwa Katibu, Naibu Katibu, Mkurugenzi anakwenda nje ya taratibu, ninaloliomba mimi ni mashirikiano. Waziri huyu hapa linalofanyika huko halijui, tunaweza kumtupia kombora hapa Katibu Mkuu, yupo juu au Naibu Katibu Mkuu yuko kule hajibu kitu wanamwachia kazi mwenzake. Kwa hivyo yale yaliyozungumzwa Mheshimiwa niseme kwamba tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Lakini kubwa na la mwisho nimuombe Mhe. Waziri wangu mpya Waziri wa Kazi, tumsaidieni sana, kwa sababu hapa tunazungumza utekelezaji wa shughuli zetu na hapa ikija Kamati ndiyo yenye mamlaka ya kuzungumza, Waziri wewe tunakusaidia wewe kwa upande mmoja. Kwa hivyo usiwe na mambo ambayo kidogo ukasema utatamka moja kwa moja na kama unaweka sawa ni hatari. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, sina haja kuendelea na mazungumzo mengi lakini nitasema machache. Suala la nyumba za wazee. Sisi kama Kamati tunamuomba Mhe. Waziri sana atuamini na ndio maana tunataka kunapokwenda sisi na Waziri aende. Tunapokwenda katika kamati na Waziri waende. Mimi katika kamati zangu naomba sana Waziri wa Habari, Utalii na Naibu wake yule pale Bi. Chum tulikuwa nao mpaka Pemba, tulikuwa naye mpaka kwenye ile hoteli ya baharini sote mheshimiwa hatukujali mawimbi hatukujali upepo. Kwa hivyo niseme kwamba lengo la Kamati ni kufanya kazi na Waziri au Wizara, wewe mwanasiasa mwenzetu watendaji ndio wana mambo. Kwa hivyo tukishikana sisi faida itapatikana, tukilumbana sisi tutaumizana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache kwa kuwa na taarifa rasmi ya mwezi wa Septemba nasema mimi binafsi na kwa niaba ya kamati yangu tumeridhika na utendaji wa Wizara zetu mbili, hatuna ubaya na Waziri, hatuna

ubaya na Katibu Mkuu, hatuna ubaya na yeyote. Lakini tunalosema tunaloelezana hapa liwe ni somo katika utendaji wetu wa pamoja.(*Makofi*).

Baada ya hayo mimi niko chini ya Wizara zote na kama wizara zote Mawaziri wote...

Mhe. Naibu Spika: Toa hoja Mheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Natoa**.** Nipo chini ya Wizara zote na kama Mawaziri wote baba mmoja, mama mmoja tusaidiane. Baada ya hayo kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mwenyekiti ametoa hoja wanaokubaliana na hoja, wasiokubali, wanaokubali wameshinda. Waheshimiwa Wajumbe nina tangazo moja kesho mnataarifiwa kwamba kutakuwa na kamati. Kamati itakayojadiliwa kesho ni Kamati ya *PAC.* Kwa hivyo mnatakiwa nyote mjitayarishe kwa Kamati ya *PAC.*

Baada ya kusema haya machache Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana kwa mashirikiano yenu mema na utulivu wenu, naahirisha kikao hadi kesho saa tatu asubuhi.(*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 2:00 za usiku kikao kiliahirishwa mpaka
tarehe 28/2/2017 saa 3:00 asubuhi)